Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 11 Oktoba, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi cha tarehe 2/10/2017, Mhe. Hidaya Ali Makame Nafasi ya Wanawake aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Afya na Mhe. Naibu Waziri wa Afya aliahidi kujibu kwa maandishi. Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Afya asome jibu la swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Mjumbe huyo. Mhe. Waziri wa Afya karibu sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika kwa kutupa nafasi hii nashukuru, kama tulivyoahidi naomba kuwasilisha jibu hilo wakati Mhe. Naibu Waziri anajibu swali Nam. 126 aliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Hidaya Ali Makame ambaye alitaka kujua ni wanafunzi wangapi waliosomea fani ya uuguzi tokea mwaka 2012 ambao hadi sasa tayari wameshapatiwa ajira.

Mhe. Spika, ufafanuzi wa maelezo hayo kwa sababu lilikuwa ni swali linalohusu takwimu zaidi, wizara kupitia Tume ya Ajira nchini imekuwa ikiajiri wafanyakazi wa kada za uuguzi kutoka vyuo tofauti vilivyopo hapa Zanzibar, Tanzania Bara na nje ya Tanzania. Wizara kuweza kujua idadi ya wanafunzi wanaosoma fani ya uuguzi kwenye vyuo hivyo ni vigumu ila kwa sababu ni vyuo vingi, kwa ndani yake humo wamo waliokwenda chuoni wakati tayari wameshaajiriwa lakini pia wapo ambao wametoka skuli moja kwa moja na kujiunga na chuo kimoja kimoja.

Wizara imekuwa ikijuwa idadi ya wauguzi waliosoma Chuo cha Taaluma za Afya za Mbweni tu, ambacho hivi sasa kipo chini ya SUZA. Hata hivyo, idadi ya wauguzi walioajiriwa na Wizara ya Afya tokea mwaka 2012 hadi hivi sasa ni 276. Ahsante Mhe. Spika,

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) kwa mwaka 2016/2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kaw ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani ya Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Mwaka wa Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*) kwa mwaka 2016/2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Rashid Makame Shamsi (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*): Mhe. kwa idhini yako naomba kuweka hati mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na

Mashirika (*PAC*) kuhusu Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) kwa mwaka 2016/2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Suleiman Sarahan Said (Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano naomba kuweka hati mezani kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*) kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 93

Uteuzi wa Masheha Wapya na Nyenzo za Kufanyia kazi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Serikali ya Mkoa wa Mjini Magharibi kupitia Mkuu wa Mkoa wake Bwana Ayoub Mahmoud Mohammed inastahili pongezi kwa kufanya uteuzi wa Masheha wapya kwa Shehia za Wilaya za Mjini na Magharibi "A" na "B" kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, Masheha hao wanaingia ofisini wakiwa na changamoto kadhaa za kuongoza shehia hizo.

(a) Je, serikali imejipanga kiasi gani kuhakikisha kuwa Masheha wanakuwa na majengo ya ofisi za kufanyia kazi badala ya kufanya kazi za serikali majumbani mwao, jambo ambalo ni hatari kwa siri za serikali.

(b) Je, mipaka ya baadhi ya mitaa ambayo haijafafanuliwa vizuri, imesharekebishwa ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi wa shehia mpya na zile za zamani.

(c) Wizara imejipanga vipi kuhakiksha kuwa Wajumbe wa Sheha wanachaguliwa kwa kuzingatia majukumu ya kisheria aliyopewa Sheha katika Sheria mpya ya Tawala za Mikoa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 93 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nakiri kwamba Masheha wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa ofisi zinazoendana na wadhifa na majukumu yao, jambo linalopunguza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Changamoto hiyo inawakabili takriban Masheha wote na sio wa Mkoa wa Mjini Magharibi pekee. Kwa kuwa utatuzi wa changamoto hii unahitaji fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa takriban ofisi 387 za Masheha nchi nzima, katika hatua ya awali serikali imewaagiza Masheha wote kuanza kuainisha maeneo ya ujenzi wa

ofisi hizo ili hatua ya kuwaomba wahusika wengine kuunga mkono juhudi za serikali katika ujenzi wa ofisi hizo ziweze kuchuliwa.

(b) Mhe. Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inashirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Idara ya Upimaji na Ramani ili kuandaa Mpango Maalum wa kuyatambua na kuyapima maeneo ya kiutawala katika ngazi ya Shehia, Wilaya hadi Mkoa ili kurahisisha shughuli za kiutawala pamoja na kuondoa utata wa kiutawala wa mipaka katika maeneo hayo. Aidha, katika kufanikisha utekelezaji wa mpango huu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 imetenga jumla ya shilingi 128 milioni kwa ajili ya kazi za kuweka mipaka katika maeneo ya kiutawala yaliyotajwa hapo juu.

(c) Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 25(1) na (2) cha Sheria ya Tawala za Mikoa Nam. 8/2014, Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Shehia (*Shehia Advisory Council*) wanateuliwa na Mkuu wa Wilaya kwa kushauriana na Sheha wa Shehia husika. Hivyo basi, kwa sasa serikali haioni haja Kamati hiyo ya Ushauri ya Shehia kuchaguliwa badala ya kuteuliwa kama ilivyo kwa mujibu wa sheria ilivyo hivi sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kukiri na huu ndio uungwana kwa masheha wetu kuwa wana changamoto za muda mrefu. Serikali imekuwa ikijua tatizo hili ni la muda mrefu sana kwa masheha wetu lakini kumekuwa hakujatokea dalili yoyote ya kuwajengea ofisi. Kama hakuna dalili kwa nini serikali haijipangi hivi sasa kila mwaka ikaweka fedha angalau kila wilaya ikaanza kujenga ofisi tano, angalau masheha wetu wakajua kuna harufu inanukia vizuri. Hamuoni kama wizara wa kujenga kidogo hii keki watu wakakatiana kidogo ikajenga ofisi tano kila wilaya. Mtoto akizaliwa haendi mbio hutambaa, akakweta mpaka akachanganya. Hilo la kwanza.

La pili, kwa kuwa waziri sasa amekimbilia mipaka umetenga karibu shilingi 128 milioni haoni hao masheha hawawezi kufanya kazi sasa bila ya kujua mipaka yao na wakati umefika na itawachanganya hivi sasa kabla ya kuwajengea ofisi na kugawa mipaka kwa muda huu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayouba swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza nataka niseme kwamba serikali katika kulishughulikia jambo hili ndio maana mwaka huu wa fedha imetenga jumla ya shilingi 128 milioni kwa ajili ya kubainisha maeneo kama tulivyowaagiza masheha. Sasa kuhusu suala la kujenga angalau ofisi tano na kuweka kwenye bajeti, nadhani suala lake ni zuri na naona serikali tunalichukua ili twende tukalifanyie kazi. Inawezekana tukajenga ofisi tano, inawezekana tukajenga zote na inawezekana tukajenga nusu ya ofisi hizo. Ahsante sana.

La pili, nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba masheha wanayaelewa maeneo yao, kilichobakia ni kuweka *demarcation* ili kuwa na uhakika zaidi wa yale maeneo ya kiutawala ambayo yametangazwa na Mhe. Rais. Lakini kuelewa maeneo gani masheha wote wanaelewa

maeneo hayo, isipokuwa tutakapoweka ile mipaka na kuweka *demarcation* ndipo tutakuwa na uhakika zaidi wa masheha kufanya kazi zao vizuri, lakini jambo lake nadhani tunalifanyia kazi kama nilivyosema katika jibu mama. Ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri akiacha changamoto za ofisi za masheha, masheha wanakabiliana na kazi ngumu katika shughuli zao za ufuatiliaji.

Je, wizara haioni ipo haja ya kuwapatia vyombo vya usafiri japo kwa njia ya mkopo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Nakubaliana naye kwamba masheha wanafanya kazi nzito na muhimu katika nchi hii. Lakini kwa sasa serikali imeamua kuwajengea maeneo ya kufanyia kazi kwa maana ya ofisi, tutakapomaliza mpango huo wa kuwajengea maeneo yao ya kufanyia kazi ndipo tutakapokuja na mpango wa pili wa kuona ni kwa jinsi gani tunatafuta namna ya kuwawezesha kuwapatia vyombo vya usafiri. Lakini kwa sasa serikali ina mpango wa kuwajengea ofisi badala ya kuwatafutia vyombo vya usafiri. Ahsante sana.

Mhe. Shaibu Said Ali: Mhe. Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri na mimi nina swali dogo la kumuuliza Mhe. Waziri. Kwa kuwa Mhe. Waziri kuna mgongano mkubwa wa kikazi kati ya masheha na madiwani hususan vijijini kutokana na imani zao za kisiasa inavyotokezea. Je, Mhe. Waziri analielewa hilo, kama analielewa ni hatua gani amechukua ili kuondoa mgongano huo wa kikazi kati ya madiwani na masheha.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Kwa faida ya Baraza hili tukufu la Wawakilishi na faida ya wananchi hakuna mgongano wowote kati ya masheha na madiwani. Kwa sababu masheha wanafanya kazi kwa mujibu wa Sheria Nam. 8 ya mwaka 2014 ya Tawala za Mikoa na madiwani wanafanya kazi kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014. Hata hivyo, ofisi yangu ilichukua juhudi kubwa sana katika kutoa taaluma kwa masheha na madiwani ili isije ikafika pahala kukatokea mgongano, ninachoamini hivi sasa hakuna mgongano kila mmoja anafanya kazi kwa mujibu wa sheria yake ambayo ipo na inamuongoza vizuri. Ahsante sana.

Nam. 94

Usumbufu wa Watendaji wa Baraza la Manispaa Wanaofunga Gari

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Kumekuwa na tabia isiyopendeza kwa watendaji wa Baraza la Manispaa wanaofunga gari zinazoegeshwa nje ya maegesho rasmi kuwasumbua madereva wanaofungiwa gari zao. Tabia hiyo imekuwa inawasumbua madereva ambapo mara baada ya gari hizo kufungwa vyuma kwenye matairi, watendaji hao huwa wanaondoka kwenye eneo hilo muda mrefu na kumsumbua dereva ambaye huwa tayari kulipa faini ili aondowe gari yake.

(a) Je, kwa nini watendaji wanaofunga gari vyuma kwenye matairi hawakai kwenye vituo vyao muda wote ili kuepusha usumbufu kwa madereva.

(b) Je, kwa nini watendaji hao huzifungia gari nyengine ambazo huwa hazipo kwenye maegesho yasiyo rasmi na badala yake huwa zinasimama kushusha mtu na kuondoka.

(c) Kutokana na usumbufu wanaopata madereva kwa watendaji hao, ni hatua gani wanapaswa wachukuwe pale ambapo mtendaji amefunga gari na kuondoka eneo lake huku dereva akisubiri muda mrefu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 94 lenye vipengele (a), (b) na (c) na kabla sijamjibu swali hilo naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya mwaka 2014 kifungu cha 94 na Kanuni ya 76 (a), (b), (c) na (d) kifungu kinapiga marufuku uegeshaji wa vyombo vikiwemo gari, vespa na mikokoteni katika maeneo yasio rasmi. Katika udhibiti wa uegeshaji holela wa vyombo hivyo, Baraza la Manispaa linawajibika kuwachukuliwa hatua za kisheria wamiliki wa vyombo vinavyoegeshwa katika maeneo yasio rasmi kwa kuviwekea vizuizi hadi hapo wahusika watakapolipa faini kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 94 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa watendaji wa Baraza hawana uhakika kuhusu muda ambao mmiliki wa chombo husika atarejea katika eneo la tukio, watendaji hao wanalazimika kuondoka ili kuzunguka katika maeneo mengine ya jirani kuhakikisha kuwa hakuna vyombo vyengine vinavyoegeshwa katika maeneo yasiyoruhusiwa. Hali hii ya watumishi kuondoka katika eneo la tukio inasababishwa na uhaba wa wafanyakazi ukilinganisha na ukubwa wa eneo ambalo wafanyakazi wanatakiwa kulifanyia kazi.

(b) Mhe. Spika, gari zinazowekewa vizuizi ni zile ambazo zimeegeshwa katika maeneo yasiyoruhusiwa au zinazosimama kwa kushusha abiria katika maeneo yasioruhusika. Hatua hizi zinachukuliwa ili kupunguza msongomano usio wa lazima ambao huleta usumbufu mkubwa na hata ajali kwa watumiaji wengine wa barabara hususan katika eneo la Darajani.

(c) Mhe. Spika, kwa wale wamiliki ambao vyombo vyao vitakuwa vimewekewa vizuizi huku wafanyakazi wa Baraza wakiwa hawapo, mmiliki wa chombo husika anapaswa kutoa taarifa ya kuwekewa kuzuizi katika Ofisi ya Baraza la Manispaa ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa ikiwemo ya mmiliki huyo kulipa faini ya kosa alilofanya kabla ya kizuizi hicho kuondolewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kwa nini kwanza wasijipange kutafuta wafanyakazi wa kutosha kwanza kwa ajili ya kuendesha zoezi ili kuweka vizuizi badala ya kuwa na wafanyakazi wachache ambao wamekuwa wakileta usumbufu na wengine kufika hata kutoa risiti wakaanza kupatana shilingi 5,000 au 10,000. Hilo la kwanza.

Pili, kwa nini serikali imeshafika wakati isitangaze *tender* kama vile Tanzania Bara ili kuepusha usumbufu huu ili watu wapate kujituma kufanya kazi na kwa nini sababu nyengine gari za serikali hazifungwi wakati za wawakilishi zikawa zinafungwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub suala lake kama ifuatavyo:

(a) Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba serikali kujipanga katika suala la Utumishi ni suala la kawaida katika shughuli za serikali. Kwa sababu kila mwaka serikali inakwenda na mahitaji Wizara ya Utumishi wa Umma kuona ukubwa wa utumishi ambao upo kulingana na mahitaji ya wakati ule. Kabla ya kuwepo kwa vyombo vingi vya usafiri katika Mkoa wa Mjini Magharibi na ndani ya Zanzibar wafanyakazi waliokuwepo walikuwa wanatosha.

Lakini kwa sababu wa wimbi la uingiaji wa vyombo vingi vya usafiri ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi, serikali ndio maana ilikuja kwanza na kuandaa sheria na kanuni katika kudhibiti mambo hayo. Hatimae kwenye mwaka wa fedha wa 2017/18 au 2018/19 tutakuja na mpango wa kujua idadi ya watumishi ambao wanaweza wakakidhi haja kwa shughuli za Manispaa kwa ujumla.

(b) Mhe. Spika, suala kama nilivyojibu suala langu juzi kwenye Baraza hili kwamba hivi sasa tuko katika utaratibu wa kuweza kuitisha tenda na taratibu za tenda tayari hivi sasa ziko kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupata ushauri ili kuondokana na kuweza kukusanya au kudhibiti shughuli hizi sisi kama Baraza la Manispaa na baada yake shughuli hizi ziweze kufanywa na wakala ambaye atakuwa anazifanya kwa njia ya *electronic*. Ahsante sana.

Nam. 52

Kukamilisha ujenzi wa Madarasa katika Skuli za Unguja na Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid– Aliuliza**:**

Kwa kuwa dhamira ya Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni kuboresha elimu kwa kumaliza ujenzi wa madarasa ya skuli mbali mbali kwa Unguja na Pemba ambayo yameanzishwa kwa nguvu za wananchi sambamba na kupunguza tatizo la upungufu wa walimu ambalo kwa sasa linaonekana ndio tatizo kubwa.

Je, Wizara ina mpango gani wa kumaliza jengo la madarasa ya skuli ambayo yalijengwa kwa nguvu za wananchi sambamba na kupeleka walimu kwa skuli za visiwani hasa Fundo, Kokoa na Uvinje pamoja na kuongezea walimu skuli ya Mkiang'ombe.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 52 kama hivi ifuatavyo: -

Kwa mwaka wa fedha wa 2017/18 Wizara yangu ina mpango wa kumaliza madarasa 200 yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Kati ya hayo, madarasa 143 yatakamilishwa na serikali na yaliyobakia yatakamilishwa na wahisani wetu wakiwemo "*GPE*" na *"Zanzibar Milele Foundation".*

Sambamba na hilo, wizara imeajiri walimu 324 katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Septemba 2017. Kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 wizara imepanga kuajiri wafanyakazi 700 wakiwemo walimu 258, wakutubi 200, watunza maabara 200 na maafisa 42 wa fani mbalimbali. Aidha, wizara imeshawasilisha maombi ya nafasi 113 za kujaza wafanyakazi waliostaafu kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Juni 2017, maombi zaidi ya nafasi za wastaafu yatawasilishwa Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, pamoja na majibu ambayo hayakukamilika kwa Mhe. Naibu Waziri natamka hivyo kwa sababu mimi nilimuuliza maswali na nikaainisha maeneo. Lakini kwenye jibu lake hakunitajia skuli ambazo nimemuuliza.

Sasa nataka aniambie ni lini watafanya na utaratibu gani wa kuwapeleka walimu kwenye skuli ambazo nimezitaja na nimeziainisha ya Fundo, Kokota, Uvinje pamoja na kuongeza walimu katika Skuli ya Mkia Ngombe. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali napenda nimjibu Mhe. Omar Seif Abeid suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Ni kwamba katika skuli ambazo amezitaja ni kwamba skuli hizo walimu wapo. Isipokuwa ni kwamba hawatoshelezi kama ambavyo hawatoshelezi katika skuli nyengine. Nieleze kwamba katika Skuli za Pemba peke yake Msingi kuna upungufu wa walimu 869 si Mkia wa Ng'ombe peke yake wala Fundo wala Kokota na tuseme kwamba tika skuli alizozitaka yeye kuna unafuu fulani kuliko skuli nyengine. Kwa mfano kuna skuli ambazo zina mikondo mitatu Skuli ya Mwambe na Skuli ya Shindi.

Kwa hivyo, hata hivyo nataka nimuhakikishie kwamba katika zoezi la ajira sasa hivi ambalo linakwenda tutajaribu kuzingatia skuli alizozitaja. Lakini pia bado tutazingatia uwiano wa upungufu. Ahsante sana.

Mhe. Khadija Omar Kibano: Nashukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii nikapata suala moja la nyongeza.

Kwa kweli serikali inajitahidi sana kujenga maskuli na kusaidia elimu kwa wananchi. Mimi nataka kumuuliz waziri katika skuli nyingi zilizotajwa hapa ni skuli hafifu tu. Lakini kuna maskuli mengine bado yanataka kuongezwa madarasa hasa skuli wanazosadia wananchi, katika jimbo langu kuna Skuli ya Uondwe imejengwa na wananchi.

Je, katika bajeti yenu ya mwaka huu mmeipanga vipi katika skuli hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali napenda kumjibu Mwakilishi suala lake kama ifuatavyo:

Katika kuzikamilisha skuli ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi kwa upande wa Mikoa ya Pemba wizara imejipanga kuzingatia zaidi Mkoa wa Kaskazini Pemba ambapo Skuli hii ya Uondwe nayo ipo huko huku. Kwa hivyo, tuseme kwamba ajenge matumaini *inshaallah* nayo tutaifikia katika mwaka huu wa fedha. Ahsante sana.

Nam. 78

Changamoto za Kiwanda cha Sukari Mahonda

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kabla ya kuliondo suala langu namba 78 nimpongeze wa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Dr. Ali Mohd Shein kwa suala hili kulitolea maelekezo. Lakini nimuombe waziri tu walifatilie kulitekeleza muwekezaji huyu Rais keshalitolea maelekezo kwenye vyombo vya habari naomba kuliondoa.

Mhe. Spika: Ahsante suala limeondolewa wizara inayofata.

(Swali hili la Mjumbe ameliondoa)

Nam. 43

Maslahi ya Watumishi katika Sekta Binafsi

Mhe. Shehe Hamad Mattar - Aliuliza**:**

Kwa kuwa Serikali ilibadilisha Sera yake ya Afya ya kutoa huduma za Afya nchini na kuruhusu huduma hii kuendelea kutolewa na wawekezaji binafsi au mashirika yasiyokuwa ya Serikali hapa Zanzibar.

(a) Je, ni mikakati gani iliochukuliwa juu ya ajira wanazotoa wawekezaji binafsi jinsi wanavyozingatia maslahi na usalama wa watumishi wao.

(b) Je, Serikali imefatilia kujua kwamba wafanyakazi wa sekta binafsi hasa ya Afya humu nchini kuwa maslahi yao yamezingatiwa kama vile Serikali ilivyofanya.

(c) Je, ni mara ngapi Mhe. Waziri umeshawahi kukutana na wawekezaji kwa sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya Afya kama Hospitali ya Al-rahma, Global, Bububu Jeshini, KMKM ziliopo hapa Zanzibar kwa lengo la kujiridhisha kama taratibu za kazi kwa sekta binafsi zinafuatwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeruhusu huduma za afya kutolewa na Wawekezaji binafsi na mashirika yasiyokuwa ya Serikali hapa Zanzibar. Pamoja na ruhusa hiyo kutolewa, utekelezaji na uratibu wa suala hili bado unasimamiwa na Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto katika Idara ya Usalama wa Afya Kazini.

(a) Mhe. Spika, mkakati uliochukuliwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto juu ya ajira wanazotoa Wawekezaji binafsi jinsi wanavyozingatia maslahi na Usalama wa Watumishi wao ni kuona kwamba ajira hizo zinafuata Sheria, Kanuni, miongozo na matoleo ya Kisheria. Wakaguzi Kazi wamekuwa wakizikagua taasisi hizo kama taasisi nyengine kwa mujibu wa Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005. Wakaguzi wa Usalama na Afya Kazini wanaendelea kuzikagua taasisi hizo kama inavyoelekeza Sheria ya Usalama na Afya Kazini Nam. 8 ya mwaka 2005. Masuala ya maslahi na Usalama wa Watumishi wa taasisi hizo yanalindwa na Sheria hizo na Wakaguzi wanafuatilia kuona kuwa yanatekelezwa ipasavyo.

(b) Mhe. Spika, Serikali imefuatilia kujua kwamba wafanyakazi wa sekta binafsi hasa ya Afya humu nchini kuwa maslahi yao yamezingatiwa kama vile Serikali ilivyofanya. Baada ya Tangazo la Kisheria kutolewa kuhusu kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi. Wizara kupitia Kamisheni ya Kazi imefuatilia ili kuona kuwa marekebisho ya mishahara yanafanyika kulingana na tangazo hilo.

(c) Mhe. Spika, ndio, Wizara imetembelea na kukutana na Uongozi na Wafanyakazi wa Hospitali mbali mbali za binafsi ikiwemo Al-Rahma, *Global* na Mina. Pia, imekutana na Jumuiya ya Waajiri ambayo inawakilisha waajiri wakiwemo wa taasisi hizi na Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi ambalo linawakilisha wafanyakazi wakiwemo wa taasisi hizi. Hii ni kwa mujibu wa utaratibu wa Ushirikiano wa Utatu katika Masuala ya Kazi.

Mhe. Spika, zaidi Mhe. Waziri ndie mie niko tayari kukutana na kumsikiliza mwajiri au mfanyakazi yeyote wakati wowote. Ikumbukwe kuwa kuna tofauti ya ushughulikiaji wa maslahi ya wafanyakazi kwa taasisi binafsi na zile za umma za serikali. Hospitali za Al-Rahma na Global ni za binafsi wakati Hospitali ya Jeshi Bububu inamilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania na hospitali ya KMKM inamilikiwa na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo zikiwa Taasisi za Serikali. Wizara imeshafanya mawasiliano ya kuzitembelea Taasisi hizo. Ahsante.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa ruhusu ya kuuliza swala la nyongeza.

Kwanza niruhusu nitoe shukurani kwa Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na mwanana aliyonipa. Lakini pia nitoe pongezi kwa hospitali binafsi kwa mchango wao katika taifa letu. Pamoja na majibu mazuri naomba niulize swali la (a) na (b) la nyongeza.
Pamoja na kuwa na masuala ya maslahi ya usalama wa watumishi katika taasisi hizo yanalindwa na sheria. Lakini ikimbuke sheria iko katika vitabu.

(a) Je, hao wakaguzi wanapofika katika taasisi hizo kukagua wanakutana na viongozi au wanakutana na wafanyakazi husika.

(b) Je, Mhe. Waziri anafahamu kuwa wafanyakazi katika hospitali ya binafsi zilizopo Pemba kama wale madaktari au manesi wananyanyasika wakati bodi zinapofika kufanya ukaguzi wakati wakakuta leseni hawana wakati ziko huku Unguja kwa ajili ya kufanyiwa *renew* wanapata tabu na hospitali wakati mwengine kufungwa kwa sababu leseni hawana pale wakati imo ndani ya *process*. Je, Mhe. Waziri unalifahamu hili na kama unalifahamu kwa nini hawawekewi kitengo cha kupasisha leseni kule kule Pemba. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mheshimiwa naomba nimjibu la pili japokuwa inakuwa ngumu sana kusikiliza wakisema kule.

(b) Nianze na jibu la pili ni kwamba ahsante kwa taarifa ulitupa kuhusiana na masuala la Pemba tutahakikisha kwamba tunafatilia kwa karibu na kuangalia upungufu wowote uliopo ili tuweze kuufanyia kazi japo kuwa wamekuwa wakienda watu wa usalama inawezekana hawajafanyakazi ya kutosha.

(a) Tunapokwenda katika sehemu za mahospitali tunalazimika kukutana na uongozi na pia wafanyakazi japo kuwa mara nyingi viongozi wanaokuwepo wanatukimbia wanatupa watu ambao hawawezi kujibu maswala na sisi suala hilo tumeliangalia na hatutalinyamazia itabidi tuwafatie na wengine tayari tumeshawaandikia *notes* ya kuhakikisha kwamba wanaleta mapema iwezekanavyo. Vyenginevyo hatua za kisheria zitachukuliwa. Ahsante.

Nam. 119

Kutengwa kwa Bajeti kwa Maendeleo ya Vijana

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma - Aliuliza**:**

Katika bajeti ya 2017/2018 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limetenga Bilioni 15 kwa ajili ya ukuzaji ujuzi kwa vijana wa Kitanzania na moja kwa moja imelenga vijana kwa kujiendeleza kimitaji na mambo mengine.

Je, ni lini serikali yetu itaona umuhimu kuiga jambo hilo jema kwa manufaa na maendeleo ya vijana wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 119 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utaratibu uliofanywa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutenga jumla ya Shilingi Bilioni 15 kwa ajili ya Ukuzaji wa Ujuzi kwa Vijana wa Kitanzania ili kujiendeleza Kimtaji na mambo mengine ni mzuri sana na nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa linastahili kuigwa. Hivyo, Wizara yangu italiwasilisha wazo hili serikalini kuangalia namna ya utekelezaji wake na ikiwezekana ipeleke ujumbe Afisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu ili kujifunza zaidi namna bora ya kulisimamia suala hili. Hata hivyo, wizara yangu ina "*program*" inayofanana na hii ya Mfuko wa Uwezeshaji ambao huwa unatoa mikopo kwa Vijana, Wanawake na Wazee katika kuwaendeleza kutimiza na kukuza biashara zao.

Mhe. Spika, pia napenda kuliomba Baraza lako tukufu kulisimamia suala hili kama ambavyo Bunge limefanya kwa Maendeleo ya Vijana. Lakini pia nipende kusema tu suala hili Wakuu wa Mikoa wengine tayari wameshaanza kutenga asilimia 2 za sehemu yao ya mapato ya Mkoa kwa ajili ya kufanya kazi hii na Mkoa huu ni Mkoa wa Mjini Magharibi ambao wameanza kutenga asilimia 2 ya mapato yao kwa ajili ya vijana. Ahsante.

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake yenye ukakasi. Lakini pili na mimi napenda kumuuliza maswali ya ngongeza yenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Waziri katika majibu yake ametwambia kwamba hizi programu ni mbili tafauti na katika Afisi yake imeandaa mfuko maalum yaani Programu ya mfuko maalum ambayo inatoa mikopo kwa vijana wanawake na watoto. Lakini katika Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni programu maalum kwa ajili ya vijana pekee hakuna wanawake, hakuna wazee wala hakuna watoto.

Sasa nimuombe sana Mhe. Waziri atwambie ni lini serikali na wizara yake itakaa pamoja ili kuona jambo hilo wanalitekeleza kwa amani na salama. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba suala hili ni wazo zuri la kuiga kutoka Tanzania Bara licha ya kwamba tunatoa mikopo kwa ajili ya wanawake na watoto na vijana na wazee pia.

Lakini suala zima la kuweza kupanga kwa ajili ya vijana peke yake lipo na tutaendelea kuhakikisha kwamba linafanyika kwa sababu ni wazo zuri tunapaswa tuliige. Kama nilivyosema kwamba kwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi tayari ameshaanza kutenga kwa ajili ya vijana tu. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu niseme mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize suala dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri mikopo hii ya uwezeshaji hawapewi mtu mmoja mmoja wanapewa watu kwa vikundi wanaojiunganisha vikundi. Je, huoni kwamba ni tatizo hili wengine hawatopata fursa hii.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, napenda kumjibu Mheshimilia aliyeuliza kwamba hili sio tatizo na ni jambo sahihi kwa sababu kwa kawaida mikopo yote inayolewa ya mabenki na watu binafsi inatolewa ukiwa una dhamana ya kitu fulani, wengine wanakuwa na dhamana ya nyumba, mashamba na mali. Kwa sisi hatuna dhamana nyengine zaidi ya wana kikundi wenzio kwa sababu ukimkopesha mtu mmoja, una namna ya kumfuatilia na kumdhamini inakuwa ni shida. Ni pesa nyingi sana ambazo zimeshawahi kutolewa huko nyuma kwa msingi huo unaosema hazijaweza kurudishika kwa sababu namna ya udhibiti unakosekana.

Nam. 102

Kupungua kwa Baadhi ya Ndege wa Asili Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny: Mhe. Ali Suleiman Ali) - Aliuliza:-

Zanzibar ina ndege wa asili aina ya Korongo na Shakwe kwa upande wa maeneo ya bahari, na kwa maeneo ya shambani kuna ndege wa aina ya Yange Yange.

Kwa kuwa ndege hao wametoweka kwa wingi hapa Zanzibar, Je, ni kitu gani kilichopelekea kutoweka kwa ndege hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 102 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba wizara yangu inatambua kuwepo kwa ndege wa aina ya Korongo, Shakwe na Yange Yange, kwenye maeneo mbali mbali yakiwemo ya nchi kavu na kwenye maeneo ya baharini hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, wizara yangu haijafanya utafiti wa kina kuhusu sababu za upotevu wa ndege hawa. Hivyo, hatuwezi kuthibitisha kwamba ndege hao wamepotea au laa, kwa vile hakuna taarifa za kiutafiti za kufahamu ukweli wa jambo kama hilo.

Mhe. Spika, hata hivyo, ni lazima tukubali kwamba katika miaka ya hivi karibuni nchi yetu imeshuhudia uharibifu mkubwa wa mazingira ikiwemo ukataji wa miti ovyo, uchomaji moto na uharibifu wa misitu ambayo ni makaazi muhimu ya aina mbali mbali za ndege.

Mhe. Spika, ongezeko la kunguru weusi ambao huyala mayai na makinda na mabadiliko ya tabianchi nayo pia yanaweza kuhusishwa na upotevu wa ndege waliotajwa na ndege wengine wengi wenye asili ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, inachukua juhudi kadhaa kuhakikisha raslimali za ndege na wanyama pori wengine hazipotei, ili kizazi kijacho kiweze kurithi utajiri huu. Kwa upande wa kupambana na kunguru, wizara yangu ilitekeleza mradi wa kuangamiza kunguru, kuanzia 2012/2013 na jumla ya kunguru 500,000 waliangamizwa. Mradi huo umemaliza muda wake na wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inaandaa mradi mwengine wa kuangamiza Kunguru hao.

Mhe. Spika, katika juhudi za kuhifadhi Misitu isiendelee kupotea ambayo ndio inayohifadhi wanyama pori na ndege hawa. Wizara yangu imekuwa ikishiriana na wanajamii katika kuhifadhi Misitu yao. Mpaka sasa jumla ya Shehia 57 za Unguja na Pemba, zimewekeana mikataba na Idara ya Msitu na Maliasili Zisizorejesheka, kusimamia Misitu ya Asili iliyomo katika maeneo yao. Aidha, Misitu mengine ya Jambiani-Muyuni, Pongwe-Ufufuma katika kisiwa cha Unguja na Msitu wa Malilini katika Kisiwa cha Pemba imepandishwa hadhi na kuwa Misitu ya Hifadhi.

Mhe. Spika, wizara yangu inawaomba Waheshimiwa Wawakilishi waendelee kushirikiana na wananchi majimboni mwao kuhamasisha uhifadhi wa misitu, wanyama pori pamoja na ndege kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu kwamba hatuwezi kuthibitisha kuwa ndege hao wamepotea au vile hakuna taarifa. Kazi yake ni nini Mhe. Naibu Waziri.

a) Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata kauliza swali ndani ya chombo hiki, hakuuliza Kijitoupele kauliza ndani ya chombo hiki na kwa mujibu wa Kanuni mnastahiki kujibu. Maana yake ndio tunapowaambieni mawaziri na manaibu waziri hamjawa tayari kujibu.

(b) Ni hatua gani mlizochukua hao ndege mlipowaweka hivi sasa ili wananchi wapate kuwaona mlipowahifadhi hao ndege waliokuwa hawajapoteza mwelekeo wa kuhama katika nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, katika jibu langu mama nilisema kwamba taarifa hii hatuwezi kuitolea majibu vizuri kwa sababu inahitaji utafiti zaidi kufahamu ni kweli hawa ndege wamepotea ama wapo. Vile vile nikasema kwamba kama wamepotea basi nikasema nini sababu ya kupotea kwa ndege hawa. Namuomba Mhe. Mwakilishi atuachie tukafanye utafiti ili tuwe na jibu la uhakika zaidi ili tuweze kumletea. Hilo ni jibu lake (a)

(b) Mhe. Spika, kama nilivyomuambia bado katika Idara yetu Misitu na Maliasili Isiyorejesheka kuna kitengo cha wanyamapori. Kitengo hiki cha Wanyamapori kinashajihisha wanajamii kufuga ndege hawa au kuwaenzi ndege ambao tunao ili tusiwe na upungufu wa ndege hawa. Kwa upande wetu sisi kama wizara bado hatuna sehemu ya kusema kwamba labda waje watu waangalie ndege hawa. Ahsante.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake mama alisema kwamba ukiachia masuala ya ndege alizungumzia kuwa wanawashajihisha wanajamii katika kuhifadhi misitu yao ya asili, ili ndege hao waweze kupata vioto waweze kuishi na kuongezeka.

Je, kwa wale wananchi ambao wanayo misitu ya asili wanahifadhi wenyewe. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inachukua juhudi gani katika kuwaendeleza au kuwapitia na kuwapa ufahamu zaidi wa kuitunza misitu hii. Ni juhudi gani wanazofanya kwa wale wanaohifadhi misitu yao ya asili watu binafsi.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe samahani hili swali ni jipya, swali mama linahusu ndege na sio misitu.

Nam. 114

Usumbufu wa Ofisa wa Maliasili kwa Madereva wa Gari za Mizigo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, nimuambie tu Mhe. Naibu Waziri hili swali kabla ya kuleta sisi Waheshimiwa Wawakilishi, tunalileta kabla ya mwezi mmoja hapa Barazani halafu mlifanyie kazi.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe naomba uulize swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naomba serikali ijibu swali langu namba 114.

Madereva wa gari za Mizigo ya maliasiali kama vile mchanga, kokoto, kuni n.k wamekuwa wakitarazaki kwa kazi hizo muda mrefu. Mwishoni mwa mwezi wa Julai, 2017 kuna madereva wanne eneo la Jozani na Paje walisimamishwa na mtu aliyejitambulisha kuwa ni Haji wa Haji akiwataka walipe faini ya fedha ya shilingi 100,000/= bila kuwapa risiti kwa madai kuwa

wamepakia kuni mbichi, wakati huo huo baadhi ya madereva wakiachiwa waendelee na kazi bila ya usumbufu kama huo.

(a) Je, kwanini ofisa huyo anatoza faini madereva bila kutoa risiti, huu si ubadhirifu na wizi wa fedha za serikali.

(b) Kwanini Madereva wengine wamekuwa wakisamehewa na wengine wakitakiwa walipe faini zisizo na risiti, je, huu si ubaguzi unaopingwa na Katiba ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 114 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba nichukue fursa hii kulifahamisha Baraza lako tukufu kwamba Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka ndio yenye dhamana ya kusimamia Maliasili za Misitu, Wanyama pori na Mimea chini ya Sheria Nam. 10 ya 1996.

Kwa mujibu wa Sheria hii, Mkuu wa Misitu yaani Mkurugenzi wa Idara ya Misitu amepewa mamlaka kamili ya kusamehe makosa au kupiga faini kwa utaratibu maalumu uliofafanuliwa katika kifungu 98 (1-3) cha Sheria Nam. 10 ya 1996.

Mhe. Spika, utaratibu huu unajumuisha, pamoja na mambo mengine, kwa mtuhumiwa kukiri kwa maandishi na kuomba shauri lake limalizwe nje ya mahakama. Aidha, Sheria ya Misitu na kanuni zake imeainisha adhabu na faini mbali mbali za makosa yanayohusu maliasili za misitu. Kwa mujibu wa Sheria ya Misitu kiwango cha chini cha faini ni Sh. 500,000 na cha juu kabisa ni Sh. 1,000,000.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu haijapokea malalamiko yanayohusiana na madai hayo. Kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Nam. 10 na kanuni zake haina kosa lenye faini ya Sh.100,000/-. Aidha, naomba kuwafahamisha madereva ili sheria ya kusamehewa kupelekwa mahakamani ni lazima ukiri kosa kwanza na uombe kwa maandishi kwa Mkuu wa Misitu kwamba shauri lako lisikilizwe nje ya mahakama. Kwa bahati mbaya jambo hilo halikufanyika.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Misitu na Kanuni zake, kosa la kusafirisha kuni bila ya kibali adhabu yake ni Sh. 700,000 na tunamwomba Mhe. Mwakilishi atupatie jina na anuwani ya dereva huyo ili utaratibu rasmi wa kusamehe uanze. Aidha, ningependa kusema kuwa fedha za serikali zina utaratibu wake wa kutoa na kupokea. Fedha hubadilishwa na risiti. Kwa kuwa hakuna kiwango cha faini cha Sh.100,000/- katika Sheria na Kanuni za Misitu, wizara yangu inaomba kupata vielelezo kuhusiana na fedha ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

(b) Mhe. Spika, naomba kulifahamisha Baraza lako tukufu sio kila kosa lazima liadhibiwe, wahusika wanaweza kupewa onyo na pia wanaweza kupewa elimu itakayowafanya wasilirudie kosa hilo kwa mara ya pili. Ama kwa wale wengine wanaolipishwa faini bila ya risiti, ningependa kusema kuwa iwapo kweli kitendo hiki kimetokea basi wote wawili wamo makosani kwa mujibu wa sheria. Katika nchi hii, ni kosa kutokutoa risiti na pia ni kosa kutodai risiti.

Mhe. Spika, kama madereva hao wamenunua huduma bila ya kupewa risiti na pia wao hawakudai risiti basi mtoaji na mpewaji huduma wamo makosani na ingelipendeza kama Mhe. Mwakilishi kwa vile wahusika wanajulikana basi wangeripotiwa Kituo cha Polisi ili Sheria ifuate mkondo wake. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na majibu ya kusikitisha ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali dogo tu ya nyongeza lenye (a) na (b).

Mhe. Naibu Waziri ni sababu gani iliyopelekea mwanzo ukaambiwa ukapakie kwanza kifusi cha vumbi la kokoto, kuni au mawe ndipo ukate risiti. Walichokuwa wakihofia mwanzo usiende ukapakia mchanga au kokoto mpaka akione.

Hivi sasa utaratibu umebadilika je, kuna sheria mloipitisha humu kwenye Baraza hii au ni utaratibu wenu tu. Maana yake kumekuwa kuna watu na nimekutajia mahali na tarehe na tukio lilipotokea na niliripoti wizarani misitu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe lifanye fupi kidogo hilo swali lako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub:

(a) Ni sababu gani zinazopelekea madereva au wananchi kusumbuliwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Mwanzo walikuwa wakiambiwa wakapakie bidhaa kwanza ili ionekane ndio wakakate risiti, lakini sasa wametegwa wanapakia huko huko hawajatoka njiani wanakamatwa. Usumbufu huu au unyanyasaji huu utakwisha lini katika wizara yako na hasa huyu Haji wa Haji.

(b) Sio kila kosa linasamehewa. Hili limetia uchungu walikuwa ni wanne waliokamatwa wenziwe watatu wakasamehewa mmoja akajiacha peke yake. Hata ungekuwa na watoto wako watatu au wanne ukampendelea mmoja wale wengine wangejihisi vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, mnamo tarehe 04/10/2017 nilijibu swali la namna kama hii na swali lake lilikuwa namba 113.

(a) Vile vile Mhe. Mjumbe nilikuambia kwamba waheshimiwa hawa ni lazima wakakate kibali kwanza ndipo wapakie maliasili ya aina yoyote, hiyo ndio sheria yetu na si vyenginevyo. *(Makofi)*

(b) Hatuna nia ya kuwasumbua wananchi wetu, wote tunawatendea haki sawa. Kama nilivyosema kwamba kama umekosea na umekubali kosa na ukaomba samahani, basi unaweza ukasamehewa na ukaendelea na safari yako au ukaenda zako misitu ukamaliza zile taratibu ambazo zinatakiwa kufanyika. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikamuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongez kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba kwa mujibu wa sheria Mkurugenzi wa Misitu amepewa mamlaka ya kuweza kutoza faini kwa makosa mbali mbali, lakini vile vile kuna makosa mengine anaweza kupelekwa Mahakamani.

Sasa swali langu nalijenga kwamba, hivi karibuni yalikamatwa magari mengi pale yaliyobeba michanga pale Maruhubi na miongoni mwa makosa hayo likiwemo hilo alilolizungumza Mhe. Jaku Hashim, lakini vile vile wale ambao walioambiwa kuwa wamepata risiti *fake* kutoka benki. Swali langu liko hapa.

Je, mpaka sasa hivi na kwa kuwa Mhe. Waziri alituahidi hapa Barazani kwamba wanawafuatilia wale ambao waliohusika kutoa risiti *fake* kutoka benki, wameshapatikana na kama wamepatikana wamechukuliwa hatua gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe atupatie muda zaidi ili tuweze kuja kumletea hiyo taarifa. Lakini hatutaweza kuwataja watu hao kutokana na kwamba lazima tuwafiche watu hao. Lakini watachukuliwa hatua kama tulivyoahidi. Ahsante.

Nam. 129

Matunzo ya Majengo Makongwe ya Chuo cha Kilimo Kizimbani

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:-

Chuo cha Kilimo Kizimbani kina majengo ambayo ni ya enzi ambayo yanatambulika kama ni ofisi za Chuo na bado baadhi yake yanaendelea kutoa huduma hizo za kiofisi mpaka leo, pamoja na majengo hayo kuwa na umuhimu mkubwa baadhi ya wananchi hawaelewi umuhimu wa ofisi hizo kutokana na hali yake.

(a) Je, Wizara ina mpango wa kuyakarabati majengo yale ili yaweze kuwa katika hali nzuri kama ilivyokuwa zamani kutokana na umuhimu wa majengo hayo kwa Chuo cha Kilimo ambayo yanatumika kama mlango mkuu na asili wa Chuo hicho cha Kilimo.

(b) Wizara kuyaacha majengo yale na kuwa mabovu zaidi na hatimae kuhamwa haioni kuwa inapoteza zaidi uhalisia wa chuo kile ukizingatia pale sehemu yalipo kuwa ni maonyesho zaidi na ni kivutio hata kwa watalii.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kulifufua jengo ambalo lilikuwepo pale kama ni kituo cha kuweka mafuta ya matrekta na kuendelea na kazi hiyo ya kuhifadhi mafuta ya matkrekta kwa ajili ya chuo lakini hata kwa faida ya wananchi wa maeneo yale (wakulima).

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 129 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ninakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Chuo cha Kilimo Kizimbani kinakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa majengo, hali hii inapelekea kuwepo kwa uchache wa madarasa, dahalia, ofisi na nyumba za walimu. Bahati mbaya Chuo hakina bajeti ya maendeleo. Hivyo, imekuwa ni vigumu kutekeleza adhma ya kukarabati majengo hayo. Hata hivyo, wizara inafahamu kadhia hiyo na tayari imeingiza katika malengo yake ya muda mrefu.

(b) Mhe. Spika, kutokana na wizara kutokuwa na uwezo wa kuyakarabati majengo hayo, imesababisha baadhi ya majengo kuwa mabovu zaidi, hatimae kuhamwa na kuanguka. Aidha, wizara inafanya mazungumzo na wahisani wa maendeleo kukisaidia chuo kujenga majengo ya kisasa katika maeneo hayo ambayo yatakidhi haja za Chuo.

(c) Mhe. Spika Kituo cha Kuweka na Kuhifadhi Mafuta cha Kizimbani kimejengwa na Mradi wa Mpunga wa Umwagiliaji Maji, ambao ulikuwa unafadhiliwa na *FAO* katika miaka ya 1980, kwa lengo la kuhifadhi mafuta ya mradi huo. Kwa bahati mbaya baada ya kumalizika mradi huo katika miaka ya mwishoni mwa 1980, mafuta hayakuwa yanahifadhiwi katika kituo hicho. Hali hii, ilisababisha tangi la mafuta kuoza na mashine ya kusukumia mafuta kuharibika.

Aidha, wizara haina lengo la kukarabati tangi la mafuta pamoja na *machine* yake, kwa sababu utaratibu uliokuwepo hivi sasa ni mzuri, mafuta yanahifadhiwa katika sheli za wafanyabiashara na yanapohitajika madereva hupatiwa kuponi ya kuchukulia mafuta. Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanikiwa kuweka sheli kila wilaya. Hivyo, upatikanaji wa mafuta umekuwa rahisi zaidi.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza tena. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake. Pia nimpongeze Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kwa hatua yake anayoichukua juu ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na hatimaye jana kutufungulia maonesho katika chuo hiki, nimpongeze sana Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Waziri ni sawa sawa Chuo cha Kilimo hakina bajeti. Lakini ninavyokifahamu Chuo cha Kilimo Kizimbani ni chuo ambacho kinajitegemea wenyewe, mfano wa kwamba kinajiendesha kutokana na maliasili ambazo zilizokuwepo pale.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna utaratibu gani wa kuhifadhi hizi maliasili ambazo zinapatikana pale chuoni na kuziendeleza zaidi ili chuo hiki kikaweza kujitegemea wenyewe na sio bajeti kutoka serikalini, kwa sababu tunaonekana kwamba serikali ina bajeti nyingi na mambo mengi. Kuna utaratibu gani wa kukifanya hiki chuo kikaweza kujitegemea wenyewe kutokana na mali na kila kitu ambacho kinapatikana pale ndani ya chuo.

(b) Mhe. Waziri ni sawa sawa kile kituo pale cha mafuta kiliharibika muda mwingi na hakifanyi kazi muda mwingi. Lakini inaonekana kwamba kuna majengo pia ambayo yanahifadhi yale yale matrekta pale. Majengo haya pia bado sasa hivi yako katika hali mbaya, lakini hata hayo matrekta ambayo unasema kwamba mafuta yanapatikana katika vituo vya mafuta ambavyo viko ndani ya wilaya. Huoni kwamba kuna usumbufu mkubwa unaopatikana katika kituo kile au Chuo kile cha Kilimo kwa kufuata mafuta hayo katika sheli zilizokuwepo Kitundu, Melisita au Kijichi. Kwa nini zisirahisishwe kazi hizi ili mafuta haya yakaendelea kupatikana pale pale hata kama chuo hakina bajeti, lakini kuna utaratibu gani ambao utafanyika ili mambo haya yaweze kukaa sawa pale ndani ya Chuo kile cha Kilimo Kizimbani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa sasa hivi kinajiandaa kujiunga katika Chuo cha *SUZA.* Vile vile hatuna mpango wa kukarabati majengo hayo, bali tuna mpango wa kukitanua chuo hiki, kwa hivyo nyumba zile zitaangushwa kwani ni nyumba za udongo tu.

Vile vile katika kujitegemea, tunajitahidi kuwasaidia ile ruzuku, Chuo ni lazima kipatiwe ruzuku mpaka kitakapojiweza ndipo kitaweza kujitegemea wenyewe. Katika masuala ya ile sehemu ya mafuta, kama nilivyomwambia Mhe. Mwakilishi kwamba hatuwezi tukarudisha mfumo ule, hatuwezi tukaweka mafuta pale wakati kuna vituo maalum vya mafuta ambavyo vina ulinzi kamili na kila kitu, pale hatuwezi kurejesha huo si usumbufu lakini ni kufuata ile tuliyowekewa na Mhe. Rais alivyotuwekea vituo kila Wilaya, kwa hivyo sio usumbufu kwao wao.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuweza kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali moja la nyongeza, kufuatilia majibu mazuri ya msingi ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri alisema kwamba wana mipango ya kuweza kuzungumza na wafadhili juu ya kuweza kukarabati au kushughulikia majengo ambayo yanahitajika katika suala zima la mafunzo katika Chuo hichi cha kilimo ambacho tunakitegemea, Suala langu ni moja lenye vifungu (a) na (b).

a) Ni maandiko mangapi ambayo wamewapeleka wafadhili kuweza kuwaomba juu ya kuyashughulikia majengo hayo.

b) Ukiacha kwategemea wafadhili ambao wana hiyari yao kukubali au kukataa ni mikakati gani ya dharura Wizara inachukua ili kuyanusuru majengo haya ambayo ni mhimili mkubwa katika mafunzo ya kilimo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kuhusiana na maandiko mangapi tumeomba ningeomba Mhe. Muwakilishi nimletee kwa maandishi kwa sababu sina taarifa kamili kuhusiana na maandiko mangapi tumeandika.

Kuhusu majengo Mhe. Spika, tunayafanyia ukarabati mdogo mdogo ambao hauna gharama kubwa zaidi lakini yale ambayo yameanguka kama nilivyosema hatuna mpango wa kuyajenga tena, kwa sababu tuna mpango wa kukitanua chuo hichi majengo yake.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa.

Mhe. Spika, Chuo cha Kilimo Kizimbani kimezungurukwa na wananchi wa Shehia za Mbuzini, Kizimbani, Dole na Bumbwisudi bahati mbaya zinapotokea ajira zisizo za kitaalamu huwa wananchi wa maeneo hayo hawapati.

a) Je. Mhe. Waziri anawaahidi vipi wananchi wa maeneo haya wakati wao ndio walinzi wa eneo lile.

b) Kwa muda mrefu kuna majengo tulianzisha pale kwa ajili ya kusindika matuda lakini mpaka leo hatusikii taarifa yoyote kutoka Serikalini, kuna mpango gani wa kiwanda kile cha kusindikia matunda ili wananchi wapate kufaidika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, zinapotoka nafasi hizi tunazitangaza kwa hiviyo ningependa labda Mhe. Muwakilishi awashajihishe watu wake au awashajihishe hizi shehia zilizotuzunguruka kuomba nafasi hizi ili waweze kuwa wao ni kipaumbele zaidi kwa kupata nafasi hizo za kazi.

Mhe. Spika, suala lake (b) sijamsikia vizuri.

Mhe. Spika: Mheshimiwa suali (b) lirudie kidogo alisikie Mheshimiwa.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Spika, pale Kizimbani kuna jengo ambalo lilianzishwa kwa ajili ya usindikaji wa matunda kwa muda mrefu sana, lakini kwa bahati mbaya mpaka leo hakuna maendeleo yoyote na hakuna taarifa zozote za Serikali ambazo zinatolewa. Je, Serikali ina mpango gani wa kiwanda kile cha kusindika matunda.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Maliasili: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza (b) kama ifuatavyo.

Kituo kile kinaendelea vizuri bdo hakijakamilika na kitakapo kamilika Waheshimiwa Wawakilishi mtapata taarifa kamili ili muweze kukiona.

Mhe. Spika: Ahsante kuna majibu ya nyongeza kutoka Serikalini Mhe. Waziri.

Mhe. Sira Ubwa Mamboya (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ningependa kuongezea jawabu la hili suala ambalo Mhe. Masouda ameulizia. Kituo hicho kimeanzihwa na wakora na Wakorea walileta vifaa ambavyo havijakamilika. Sasa hivi Wizara ya Kilimo imeshawasiliana na Wakorea hao na vifaa vitaletwa na karibu kitamaliza.

Nam. 83

Upungufu wa Madaktari wa Ngozi Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Hivi karibuni Gazeti la Zanzibar Leo limemnukuu Daktari wa Ngozi wa Hospitali ya Mnazimmoja Dkt. Nassor Rashid Juma akieleza uhaba wa madaktari wa ngozi katika Hospitali hiyo, huku idadi ya wagonjwa wa ngozi ikiongezeka katika Kliniki ya Ngozi inayoendeshwa kila siku ya Jumatano ambapo wagonjwa kati ya 50 mpaka 90 hupatiwa huduma kwa siku.

Je, Wizara imejipangaje kutatuwa tatizo hilo kwa kuongeza idadi ya wataalamu wa magonjwa ya ngozi katika Kliniki hiyo na Hospitali nyengine za Wilaya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 83 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika**,** ni kweli Hospitali ya Mnazi mmoja ina uhaba wa madaktari wa ngozi na kupelekea daktari mmoja kutibu idadi kubwa ya wagonjwa wa ngozi katika kliniki hizo zinazofanyika kila Jumatano. Wizara iko katika jitihada za kusomesha madaktari bingwa wa maradhi hayo ambapo daktari mmoja anatarajiwa kumaliza masomo yake mwakani na mara atakapomaliza atarudi kuendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wa maradhi hayo. Vile vile, kwa kipindi hiki cha mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara imepanga kusomesha madaktari watatu wa fani ya maradhi ya ngozi na watakapomaliza watasaidia kutatua changamoto ya uhaba wa madaktari wa ngozi katika hospitali zetu.

Mhe. Spika, naomba nimthbitishie Mhe. Muwakilishi wa Jimbo la Paje kwamba pamoja na upungufu huo wa madaktari wa ngozi tulionao, bado tunaendelea kutoa huduma hii vizuri katika hospitali yetu, kwani hospitali ya Mnazi Mmoja tunashirikiana na madaktari bingwa wa ngozi kutoka Uholanzi na kutoa huduma kwa wagonjwa kila siku ya kliniki yaani Jumatano.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze kwa dhati kabisa Naibu Waziri na atakaposema ukweli ndio huwa mpenzi wa Mwenyezi Mungu kwa kukiri kuwa hili suala lipo na ni daktari mmoja.

a) Katika suala la msingi umesema kila Jumatano ndio siku ya wagonjwa kukutana na daktari wa maradhi ya ngozi, hivi kweli Jumatano wagonjwa hao kumuona na daktari huyo mmoja atahudumia wagonjwa wangapi, na kama atawakosa wale wengine ndio wasubiri mpaka jumatano au mtu anakula jumatano hata jumatano.

b) La pili ulitaja daktari mmoja mnasomesha bingwa na wengine watatu kweli madaktari wanne hawa wakishamaliza watatosha Unguja na Pemba, na ukizingatia kuna jengo la Abdalla Mzee limefunguliwa juzi juzi nafikiri ndio kuna kilio hicho hicho cha Daktari wa ngozi, je ni sahihi hiyo Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, namuomba Mhe. Jaku arudie suala lake kwa kweli sikulipata vizuri Mheshimiwa naomba uongee kwa utaratibu kidogo.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku rudia suala la pili lakini rudia taratibu kidogo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze kwa dhati kabisa Naibu Waziri kwa kukiri kwa kusema ukweli katika Baraza kwa kuwa ana upungufu wa madaktari wa ngozi yuko mmoja tu.

Katika suala la msingi kila Jumatano ndio siku ya kutibu maradhi ya ngozi, Je, ni sawa maradhi hayo kutibiwa kila siku ya Jumatano na daktari huyo mmoja anashughulikia wagonjwa wangapi kwa siku ya Jumatano au maradhi hayo yanakuja Jumatano hata Jumatano hilo la kwanza.

La pili umesema kuna dakitari bingwa mmoja anasomeshwa na wengine watatu jumla watakuwa wanne, suala langu hawa madaktari wanne watatosha kweli Unguja na Pemba na ukizingatia nafikiria kuna harufu Hospitali ya Abdalla Mzee iliyofunguliwa juzi kuna upungufu wa daktari wa ngozi kwa mujibu wa harufu niliyoinusa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spka, naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub suala lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, siku ya Jumatano ndio siku maalum ya *clinic* ya wagonjwa wa ngozi iliyopangwa kwa mujibu wa huduma zinavyotolewa, kila *clinic* huwa ina siku yake maalum sasa hii siku ya Jumatano ni siku maalum ya *clinic* ya magonjwa ya ngozi kwa bahati nzuri *Specialist* aliyekuwepo pale ni mmoja wa maradhi ya ngozi lakini ana wasaidizi wake ambao wanamsaidia kutoa huduma. Na katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba kuna madaktari ambao ni Waholanzi wanasaidiana nae kutoa huduma kwa wagonjwa hao. Kwa hivyo kwa siku ile huwa wanato huduma kwa wagonjwa 50 mpaka 90.

Naomba nimjibu Suala la pili kwamba madaktari hawa watatu ambao tunawasomesha hawa tunategemea kuwasambaza Unguja na Pemba, kwa sababu Pemba tulikuwa nae daktari mmoja lakini kwa bahati ameshastaafu sasa pia tuna tatizo kule la madaktari wa magonjwa wa ngozi na

wanaotoa huduma hiyo kule sasa hivi ni vijana ambao wamepata mafunzo kutoka mradi wa *PHL*, hawa wanasaidiana na madaktari wengine kutoa huduma ya ugonjwa wa ngozi.

Mhe. Jaku naomba nikuthibitishie kwamba huduma hii inatolewa tena ipasavyo pamoja na kwamba *Specialist* tuliokuwa nao ni wachache lakini huduma za magonjwa haya zinatosha.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri Mwenyewe wa Afya kwa majibu ya ziada.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi hii na nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana.

La kwanza kabisa alilouliza katika suali lake la nyongeza Mhe. Jaku Hashim Ayoub hii *clinic* ipo siku ya jumatano siku zilizobakia daktari huyu anakwenda *around* katika wodi mbali mbali zilizolazwa wagonjwa wa ngozi, lakini wakati huo huo pia na *outreach program* anatembelea hospitali za Wilaya na Mkoa kama vile Kivunge na Makunduchi ndio siku nyengine n haina maana kwamba watu wanaumwa ugonjwa wa ngozi siku ya jumatano tu ndio huyu daktari akawaanafanya kazi, hapana.

Lakini la pili naomba nitoe kidogo taaluma katika maradhi mawili wanatwambia wataalam wenyewe yanakuwa hayana *Emergence* ni meno na ngozi, hili wametwambia wataalam wenyewe maana mtu hawezi kuumwa na jino mpaka akafa, au akaumwa na maradhi ya ngozi mpaka akafa. Kwa hivyo maradhi haya mawili yanakuwa hayana *emergence* ndio maana yana *clinic* yake maalum.

Lakini la tatu hapo hapo naomba nimjuulishe Mheshimiwa kwamba kila daktari aliyesoma *MD* yaani *Doctor of Medicine* anaweza kutibu maradhi ya ngozi kila daktari, isipokuwa huyu bingwa anashughulikia yale maradhi ya ngozi *complicated* ambayo yanakaa muda mrefu bila ya kupata ufumbuzi ama kupona, lakini maradhi ya ngozi mengine yoyote hata mimi nimeshawahi kupata maradhi ya ngozi nimekwenda kwa Dkt. Mambi ndio aliyenitibu ni daktari wa kawaida na anatibu.

Mhe. Spika, jengine alilouliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuna fani ya madaktari kila pahala duniani wanakuwa wachache, nimetoa juzi mfano wakati natoa maelezo hapa mfano wa *radiology* ni wachache sana madaktari wa ku-*operate MRI* hata Dar es Salaama tumekwenda kutafuta sisi wapo wawili tu wametwambia hawawezi kutusaidia kwa sababu wao wenyewe wana mahitaji hayo makubwa na wako wawili. Taaluma ya usingizi na ganzi wako wachache nilieleza juzi hapa Zanzibar tunae mmoja *And Chnology is Internal Blans* pia wako wachache na *Dermatology* pia ni wachache.Tunachofanya sasa hivi tunaongeza jitihada za kuwahamasisha na kuwashajihisha wale waliomaliza Degree ya kwanza ili waweze kwenda kufanya *Specialization* kwenye *field* ambazo zimekosa taaluma kwa miaka mingi na *field* hizi wengine wanakuwa wanalalamika kwa sababu ni ngumu sana.

Mfano *Neuroglia, Neurosurgery* ni *field* ngumu tunae mmoja tu Dkt. Said Idrissa kwa hapa Zanzibar ambae ni *qualified* kusomea *field* hizi, kwa hivyo tunaendelea na jitihada za kuwashajihisha madaktari wetu waliomaliza Degree ya kwanza nafasi za kwenda kusomesha

Specialization zipi na tutaendele, kwa fani hii sasa hivi wako wawili ambao wanasoma mmoja yuko nchini Egypt akimaliza tunatarajia atarudi.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: kidogo kuweka *Hansard* sawa tu Mheshimiwa katika maelezo yake tu wala hakuna jengine kubwa kama utaniruhusu.

Mhe. Spika: Hapana Mheshimiwa naomba ukae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante.

Machano Othman Said: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi hii na mimi kabla ya kuuliza swali langu kwanza naomba nimpongeze sana na kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuitizama sana sekta hii ya afya kwa kutoa fedha na huduma nyengine swali langu liko hapa.

Juzi Mhe. Waziri, katwambia kwamba tuna mtaalam binga au Daktari bingwa wa mambo ya gansi na usingizi mmoja, lakini pia kuna daktari mmoja wa mionzi na leo anatwambia kuna daktari bingwa mmoja wa magonjwa ya ngozi sasa swali langu liko hapa.

a) Hivi tukiacha madaktari bingwa wa kigeni Hospitali yetu kuu ya Mnazi Mmoja ina madaktari bingwa wangapi na kwa nini hawatoi motisha maalum kwa hizi kada ngumu za afya ili kuwatia hamu wale wasomaji waweze kuchukua kada hizi.

b) Miaka ya kati kati hapa kwa juhudi za viongozi wetu Serikali ya Zanzibar ilianzisha Chuo cha Afya chini ya ufadhili wa Cuba, sasa wale waliosoma wamefikia hatua gani na tunawatarajia vipi katika maendeleo yao naomba kufahamu hapo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Machano kwa maswali yake mazuri sana.

Kama atakumbuka katika kitabu cha bajeti nilitaja mabngwa tuliokuwa nao hapa Zanzibar maana inawezekana wote wakaweko Mnazi Mmoja lakini wengine wakasambazwa sehemu nyengine, mabingwa tuliokuwa nao hapa Zanzibar ni 33 wote na mabingwa hao ni katika *field* mbali mbali, kuna hawa wa sukari, kuna wa mifupa, kuna ngozi, kuna usingizi, kuna *ragiology* baadhi yao nawafahamu pia majina yao kwa hivyo wote jumla yao ni mabingwa 33.

Hawa madaktari wa Cuba wanaendelea kusoma tunawashajihisha sana wanapomaliza tu kwa sababu ndio madaktari wetu wazalendo wamesomea hapa hapa, tunawashijihisha sana wanapomaliza tu waende wakachukue *specialization* moja kwa moja ikiwezekana, lakini kuna utaratibu wa kwamba katika *field* ya *medicine* wanatakiwa kwanza wafanye kazi miaka miwili kupata *experience* ambayo ni pana zaidi itakayowasaidia kwenye *specialization*.

Na naomba niseme hivi Mhe. Spika, ili ieleweke daktari wa kawaida ni *MB* huyo anatibu kila maradhi, *Specialization* anakwenda kufanya kama *Masters* vile yaani *Degree ya Specialization*

anakwenda kufanya Masters yake ndio anakuwa bingwa katika fani ile, haina maana yule bingwa hawezi kutibu maradhi mengine na haina maana yule aliyesoma *MB* hawezi pia kusaidia au kutibu katika maradhi mengine ndio maana kwanza kunakuwa na daktari wa zamu katika wodi, halafu kuna daktari wa pili. Mwisho kabisa *on call* anaitwa yule *Specialist* kukiwa na tatizo linalohusiana na maradhi yale ambayo yanahitaji *specialization.*

Nam. 86

Hali ya Ugonjwa wa Kipindupindu Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Katika Hotuba ya Baraza la Eid el Fitr, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein ameeleza athari ya Ugonjwa wa Kipindupindu katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu.

Je, ni juhudi gani Wizara ya Afya inazichukuwa kukabiliana na maradhi hayo bila ya kutegemea msaada wa Shirika la Afya Ulimwenguni *(WHO).*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 86 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kulieleza Baraza lako tukufu kwamba Wizara ya Afya inachukuwa juhudi mbalimbali kukabiliana na maradhi ya Kipindupindu na bila ya kutegemea msaada wa Shirika la Afya Ulimwenguni *(WHO),* juhudi hizi za Wizara zinaelekezwa zaidi katika hatua za kudhibiti na kukinga ili maradhi ya Kipindupindu yasiweze kutawala mazingira ya wananchi wa Zanzibar, Wizara kwa kushirikiana na kitengo kinachohusika na ufuatiliaji wa maradhi ya Kipindupindu inaendelea kutoa elimu kwa kuwahamasisha wananchi juu ya kufuata Kanuni za Afya katika mazingira yao kwa kupitia *clinik* zetu masheha wa shehia pia inashirikiana na taasisi za Serikali kama *ZAWA* na Halmashauri katika udhibiti wa mazingira ili kuepuka mripuko wa maradhi hayo.

Mhe. Spika, Wizara pia katika jitihada na dhamira ya kukitokomeza maradhi ya Kipindupindu inaendelea na mkakati maalum kwa kuendelea kutoa elimu ya Afya kupitia Radio, *TV* na Vipeperushi kila baada ya muda, na lengo ni kuwataka wananchi kuendelea kuwa na tahadhari na maradhi hayo kwa kuweka mazingira safi, kuchemsha maji ya kunywa na kukosha mikono kabla ya kula na baada ya kutoka chooni kwani uwepo kwa kipindupindu inategemea na mazingira unayoishi.

Mhe. Spika, Maafisa wetu wa Afya Wilaya wanaendelea kufanya ukaguzi wa usimamizi wa biashara za vyakula na kufanya ukaguzi wa maji yanayotumika kwa watumiaji pamoja na kutoa ushauri bora kwa taasisi husika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala dogo tu la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Je, ni sababu gani inayopelekea katika mwaka huu sijui mara tatu au mara nne kupata maradhi haya ya kipindupindu mfululizo.

b) Ni maeneo gani yaliyopata maradhi hayo ya kipindupindu na je sasa yako salama na Wizara imechukua hatua gani Mwenyezi Mungu asije akajaalia kupata maradhi hayo, na vile vile ulipojibu ulisema maji yanayotumika kwa watumiaji pamoja na kutoa ushauri bora kwa taasisi husika kuna eneo wengine hata maji hawapati sijui kipindu pindu hakitozidi hasa ukizingatia eneo la Michamvi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, sababu zinazopelekea *(samahani sana)* maeneo ambayo yanapata sana matatizo haya kipindupindu ni maeneo yale yale ambayo yanapata siku zote maradhi ya kipindupindu.

Mheshimiwa samahani sana.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri mwenyewe anajibu, Mhe. Waziri mwenyewe naomba unyanyuke. Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Waziri kalisikia wache ajibu Mhe. Waziri naomba ujibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kutupa nafasi hii ya kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Paje swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Serikali imeshatoa agizo ifikapo mwaka 2020 kiwe kimeshamaliza kipindupindu Zanzibar na kina mkakati maalum na sisi wizara yetu ni muhusika moja wapo. Lakini hili suala hatushughuliki sisi tu wizara yetu afya, hili suala ni mtambuka na linaongozwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mwenyewe kwa sababu kwa sababu ni *national strategy* ya kutokomeza kipindupindu Zanzibar.

Tatizo kuu la kipindupindu Zanzibar kwanza eneo wameuliza, eneo linalotokea kipindupindu hasa tunaitwa *hotspot* kitaalamu wanaita *hotspot* ni ukichora kama unachora *triangle* unaanzia hapa eneo la Chumbuni unakuja zako mpaka Bububu, unakuja zako mpaka eneo la Fuoni unarudi tena hii barabara ya Amani unakuja kuunganisha tena huko Mtoni *triangle* ile ama *rectangle* ile ndio *hotspot* ya kipindupindu.

Sababu kubwa kabisa ni watu kuvamia kwenye eneo la kuishi bila ya vile viwanja ama eneo lile kupimwa, hiyo ndio sababu kuu tusimumunye maneno wala tusitafe maneno wale walovamia wakawa *sewerage*, hakuna michirizi hakuna maji machafu, hakuna mitaro ukitaka kuita ama karo na nyumba moja inajengwa na nyumba ya pili inaelekezana ukumbi choo, huyu kwake nyuma chooni huyu kwake mbele ukumbini na wakati huo huo unakuja kuchimba kisima katika eneo hilo ambao kinakuwa ni *shallow well* kisima cha kilichokuwa si cha kima kirefu.

Sasa eneo lile lote Mhe. Spika, liko *contaminated* kwa lugha ya kawaida ya Kiswahili kuna maambukizi, kipindupindu kinaanzia sisi ni wa mwisho kupokea mpira yaani kudaka yaani kama golikipa vile unadaka mpira, lakini kipindupindu kinaanzia na maji kuingia mdomoni ambayo tayari yameshakuwa *contaminated* na kinyesi ama uchavu ama kwa lugha ya fasaha mtanisamehe kwa lugha yangu, maana lugha ya afya yawe yameingia mavi mtanisemehe kwa lugha yangu lakini ndio uhalisia.

Yale maji yanapoingia mdomoni ndio kipindupindu kinapoanzia pale, kwa hiyo katika *elimination strategy* mpango mkuu wa kutokomeza kipindupindu Zanzibar jambo la mwanzo kabisa ni kuweka njia sawa ya maji machafu na maji yale huwa yanachukuliwa hasa wakati wa mvua kama tutachunguza kipindupindu baada ya mvua tu, kina *rapidly* kipindupindu kwa sababu yale maji machafu, huwa yanachukuliwa na watu wengine pia hutupa taka zao pamoja na maji machafu yanayotokea nyumbani kwenye mchirizi wa maji ya mvua. Na ndio maana tunapiga kelele sana tunapokuwa baada ya mvua kwamba zile njia ziwe safi.

Sasa Mhe. Spika, katika kujibu hapa hili si jukumu la Wizara ya Afya peke yake ama Ofisi ya Makamu wa Rais peke yake, ama Wizara ya Maji (ZAWA) peke yake, ama Wizara ya Tawala za Mikoa peke yake, hili ni jukumu letu sote hususan yule mwananchi anayetupa *pempas* ama uchafu moja kwa moja kwenye michirizi ile ya maji.

Jukumu hili ni la mwananchi ambaye anachimba kisima anajua eneo la kisima hichi sio mita 30 kutoka chooni maji yale *definite* yatakuwa *contaminated* na kipindupindu hakitaicha Zanzibar. Lazima tubadilishe tabia,na tabia hiyo inaanzia kule kwenye *rectangle* hiyo ya mwananchi mwenye kubadilisha ndio tutaweza. Sisi hatutegemei *WHO* au mtu mwengine yeyote tunafanya hii kazi kama sisi wenyewe kama wizara, wale wanatupa misaada yao lakini tunafanya sisi wenyewe kama wizara na Mheshimiwa mimi nitaomba iko siku kama itawezekana tuje na waraka hasa humu ndani, tuzungumzie suala la kipindupindu ili wawakilishi na wao wote wajue jukumu lao nini katika kuondosha kipindupindu. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Nam. 16

Kuimarishwa kwa Idara ya UUB

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Idara Maalum ya Ujenzi na Utengenezaji Barabara (UUB). Hata hivyo, mara nyingi tenda za ujenzi wa barabara mbali mbali kutolewa kwa kampuni mbalimbali badala ya kuitumia (UUB). Hali hii inasababishwa na Idara hiyo kuwa bado inategemea zana za kutendea kazi ambazo ni mbovu au zimechoka na kufanya wenye Kampuni nyengine kupata kazi za Ujenzi wa barabara. Idara hiyo inaonekana kama haina uwezo, viwango na utaalamu kumbe ni ukosefu wa zana tu.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuijengea uwezo Idara hiyo ambayo kwa sasa zana zake ni mbovu na zimechoka ili kuendana na ushindani wa kibiashara.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwajengea uwezo wa zana na fedha Idara hiyo ili kulipunguzia Taifa mzigo wa gharama za fedha nyingi zinazopotea kwa kuwapa kampuni nyengine kazi.

(c) Je, Serikali haioni kuwajengea uwezo Idara hiyo ikapiga hatua za maendeleo kwa haraka kwa kupanua wigo wa ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji naomba nichukue nafasi kabla ya kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Saidi, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chake Chake, swali lake Nam. 16 nitowe maelezo yafuatavyo:-

Mhe. Spika, Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara imepewa jukumu la kuzitunza kwa kuzifanyia matengenezo barabara kama zilizoainishwa kwenye marekebisho ya Sheria mama *(Road Decree Cap 114)* mwaka 2013. Jukumu jingine la Idara ni ujenzi wa barabara mpya kama Serikali itakavyoona inafaa. Kwa miradi ya utunzaji barabara, Serikali ilianzisha Sheria ya Mfuko wa Barabara ambao ndio wenye jukumu la kukusanya fedha za utunzaji, matengenezo mbalimbali ya barabara nchini. Kwa upande wa miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara Serikali kwa kushirikiana na wahisani wa maendeleo hugharimia miradi hiyo. Kazi za ujenzi wa barabara zinahitaji mitambo na zana nyingi ambazo hugharimu fedha nyingi, hivyo basi kutokana na uchakavu na uchache wa mitambo iliyonayo Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara, hukosa uwezo ya kuzifanyia matengenezo mbalimbali yanayojitokeza kwenye barabara na hivyo baadhi ya kazi hizo hufanywa na wakandarasi ili barabara hizo ziweze kupitika kwa urahisi kwa muda wote.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, sasa naomba kuchukua nafasi hii kujibu swali Mhe. Suleiman Sarahan Saidi swali lake lenye kifungu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali imekuwa ikichukua hatua za upatikanaji wa mitambo na zana kwa ajili ya kazi za barabara kwa awamu, hivi karibuni Wizara yangu ilitangaza zabuni ya kuwapata wazabuni wenye uwezo wa kuleta mitambo ya kupikia lami kwa upande wa Unguja, na kwa upande wa Pemba gari la lami na mtambo wa kutandaza lami *(paver)* ambapo tathmini ya kuwapata wazabuni wenye sifa kwa mujibu wa Sheria ya manunuzi Namba 11 ya mwaka 2016 inaendelea. Aidha, wigo kwa ajira kwa vijana pia unapatikana kwa wakandarasi wanaopewa miradi hiyo ujenzi wa barabara. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Saidi: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini wacha nimuongeze (a) na (b) kidogo ili tufaidike zaidi.

(a) Kwa kuwa karibu wakandarasi wengi ambao tunawapa miradi kwa kila aina baadae huleta matatizo lakini kwa sababu ya ukosefu wa Idara Maalum ambayo inaweza ikashughulika na suala lile inawezekana hatuna, lakini kwa sababu Serikali ina Idara yake Maalum ya UUB ambayo inashughulika na masuala ya barabara kwa hivyo haioni kwamba kutokana na kwamba wanao wataalamu, wafanyakazi pamoja na

kwamba wao ndio dhamana ya watu hawa katika kujenga barabara nyengine mpya pamoja na kuimarisha barabara katika *(Road Decree Cap. 114)* 2013 haioni umuhimu Serikali kwamba sasa umefika wakati wa kuiongezea nguvu Idara hii kwa wataalamu na kwa vifaa ili tenda zetu na wakandarasi ambao sio waaminifu wasipewe nafasi katika suala hili.

(b) Kwa sababu hili ni eneo ambalo lina umuhimu sana katika Serikali yetu na mara nyingi sana UUB inatusaidia katika mambo yetu bila ya kuwa na fedha ambazo zitakuwa maalum, haioni kwamba Serikali imefika wakati sasa kwamba iongeze nguvu ili kuingia katika ushindani wa kibiashara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kuchukua nafasi kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Saidi, maswala yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Kama nilivyosema hapo kabla kwamba Serikali inaona umuhimu wa Idara hii katika utunzaji na utengenezaji barabara ndio maana katika bajeti ya safari hii, tumetenga bilioni tano kwa ajili ya kununulia mitambo ya kufanyia kazi zana tofauti na vile vile hivi sasa tunaendelea kuiboresha Idara hii kwa kuwapatia wataalamu ambao wataendelea kufanya kazi hizi.

b) La pili vile vile, napenda kumjibu kwamba kazi zile ambazo zinaletwa na wafadhili wetu kuwa na vigezo maalum ambavyo vinatakiwa kwa hiyo ndio maana sisi hutangaza tenda zilizokuwa za wazi ili baadae yule anayekidhi na kufanikiwa kupata ile tenda ndio tunampa ile kazi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 105

Uwekaji wa Mkonga Katika Ujenzi wa Barabara

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Kwa kuwa mradi wa kuzika au uwekaji chini ya ardhi Mkonga wa Taifa uliofanyika miaka ya karibuni kwenye barabara eneo la Kongwe ya Wete/Chake Chake na hali ikijulikana na wataalamu wetu kwamba wakati wowote barabara hiyo itatengenezwa au itajengwa upya na kwa sababu mipango ya kulipa fidia inaonesha kwamba kutotengwa fedha ambazo zitatumika kwa ajili ya gharama za kuhamisha mkonga huo ili kupisha ujenzi wa barabara hiyo uendelee.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuweka fedha za gharama kwa ajili ya kuhamisha mkonga huo ni kujitia gharama ambazo zingeweza kuepukika toka hapo mwanzoni.

(b) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuiruhusu kampuni iliyopewa kazi ya kusambaza mkonga huo kuizika pembezoni mwa barabara jambo ambalo ni hasara kwa Serikali wakati wa ujenzi wa barabara hiyo.

(c) Je, gharama kiasi gani ambazo zingeweza kuepukika kama mkonga ungezikwa mbali na barabara kama ambavyo inaweza kujitokeza hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Konde, swali lake Nam. 105 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano uliozikwa miaka ya karibuni kwenye barabara kongwe ya Wete/Chake Chake umezikwa hivyo kutokana na sababu zifuatazo:-

1. Kwa ajili ya usalama wa Mkonga huo pindi ungezikwa mbali sana na barabara kungeweza kutokea uharibifu wa makusudi na hata usio wa makusudi unaosababishwa na shughuli za kibinaadamu.

2. Mradi huo haukujumuisha gharama za fidia na vipando na kitu chengine chochote katika *"phase"* ya kwanza.

3. Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano unahitaji maeneo yaliyonyooka ili kuweza kufanya kazi zake kama ilivyokusudiwa.

(b) Mhe. Spika, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kushirikiana na timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Ardhi inafanya tathmini kujua thamani ya vipando ambavyo Serikali itapaswa kulipia fidia pindi mzunguko wa pili wa mradi huo utakapoanza.

(c) Kutokana na mazingira ya barabara zetu kuwa nyembamba na watu wengi kujenga karibu na barabara hivyo kuwaondoa wote ni gharama kubwa sana kwa hiyo isipokuwa, Mkonga unaweza kwenye hifadhi ya barabara kuepuka gharama hizo ambazo ni kubwa kweli.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa majibu yenye muelekeo ya Mhe. Naibu Waziri lakini pamoja na majibu mazuri ambayo yanaridhisha yanatia moyo, hasa aliponielezea vile vipengele vitatu vilivyosababisha kwamba vizikwe karibu na barabara.

Lakini nilikuwa mimi lengo langu lilikuwa ni kutaka kujua kwa sababu tunao wataalamu, kwa nini wasifanye vipimo wakajua hapa wakati tukitenga hapa itamalizia barabara, na wao ndio wakazika, wakazika maeneo ambayo yatakuja kuisababishia hasara ya kuzikuwa na kuzika tena wakati wataalamu tunao ni kwa nini wataalamu wasifanye vipimo hivyo. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid, swali lake nyongeza kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema mwanzo mradi huu ulipokuwa *Phase* ya mwanzo wenyewe walikuja na viwango vyao na wakatushauri kwamba lazima ujengwe karibu na barabara sasa hili suala lake analolisema hivi sasa, tutalichukua na kulifanyia kazi katika ile *Phase II* unaotokana na mradi wa *E-health* ambao unategemea kujenga hospitali katika hospitali ishirini na nne za Zanzibar na vituo vyake basi tutahakikisha kwamba ushauri wake tunaufanyia kazi. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 106

Matumizi ya Gari za "*Convoy*" Kwa Usafiri wa Daladala

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, kwa sababu jibu nimeliona liko sawa mimi naondoa swali hilo. Ahsante sana Mheshimiwa *(Makofi)*

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu

Mhe. Spika: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, juzi ngoja niisome hii Kanuni niliyoisimamia 42(9) baada ya muda wa swali kwisha Mjumbe yeyote anaweza kutoa hoja kwamba Baraza liakhirishe shughuli zake zinazoonesha katika shughuli ya Baraza lijadili jambo la dharura muhimu kwa umma kwa idhini ya Spika.

Nasimamia namba (9) jambo lililotolewa kwa hoja chini ya Kanuni hii litahesabiwa kama jambo la dharura iwapo:

(a) Ni jambo makhsusi Mhe. Naibu Waziri juzi alipokuwa akijibu swali hapa Nam. 74 alijibu hivi:

> *"*Naibu Waziri wa Ardhi, Nishati Mhe. Naibu Spika, maji ya dharura tunakuwa tunapeleka na tunaendelea kupeleka na sasa nimwambie kwamba tukitoka hapa ili aonane kwa sababu tunaweza tukapeleka, akaja akasema hajapelekwa tuwasiliane nae kusudi akakikishe kwamba tunapeleka maji ilikuwa hoja ya dharura, niliuliza swali akanambia Naibu Waziri atapeleka maji kwa dharura lakini mpaka muda huu hakuna taarifa hiyo wala wananchi wa Michamvi huwa wananipigia siku kuniuliza hayo maji ya dharura mbona hatujayaona, sasa imekuwa kero kwa wananchi wangu wa Michamvi. Nilikuwa nataka kauli ya Serikali*."*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Jaku Hashim Ayoub bahati mbaya Waziri wa Maji hayupo lakini Serikali ipo imesikia na bahati nzuri nyengine ni kwamba leo kuna Hoja ya Ripoti ya ZAWA itakuwepo hamu Barazani, kwa hiyo nadhani itakuwa wakati mzuri sana wa kupitisha hilo jambo lako, halafu ukapata majibu yaliyo sahihi.

Waheshimiwa Wajumbe wakati wa maswali umekwisha na sasa tunatangazo la wageni.

Wageni wetu walioko ni wageni wa Mhe. Spika ambao wanatoka katika Manispaa ya *Sandsvall Sweden* ni wenyeji wa wadi ya Makunduchi jumla yao ni kumi wanaongozwa na Spika wa Baraza lao Ms. Arianne Sundman.

Wengine ambao wameongozana nao ni:

You will excuse my pronunciation of your names but wherever I mention your name should be standing up for the pray, member can appreciate your presence

1. Mr. Joan Pinheiro, *Chair of Board of Child Care and Education, Municipality of Sundsvall,*
2. Mr. Hans Zetterkvist, *Member of Board of Child Care and Education,*
3. Ms. Maria Astrom, *Board of Child Care and Education,*
4. Ms. Linda Strandfjall, *Board of Child Care and Education,*
5. Mr. Bjorn Sweden, *Project Group Leader,*
6. Ms. Asa Jerfsten, *Development and Quality, within Child Care and Education,*
7. Ms. Christin Strombery - *Coordinator*

You are almost welcome to the Zanzibar House of Representatives and I will glade meet very short after this.

Pamoja nao wamefuatana nao:

1. Bwana Mohamed Ameir Muombwa naye anyanyuke – Huyu Mratibu wa Mashirikiano baina *Sundsvall Municipality* na Wadi ya Makunduchi.
2. Bwana Hafidh Ameir - *Senior Citizen of* Makunduchi.
3. Bwana Moh'd Simba - Msemaji wa Tamasha la Vyakula vya Asili Makundichi.
4. Bwana Makame Ramadhan Makame – Ni Mjumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Karibu sana

You are almost welcome to the Zanzibar House of Representatives.(Makofi).

Baada ya tangazo hilo kabla sijamwita Katibu kwa shughuli inayoendelea naomba sasa nimwite Mwenyekiti ili achukue kiti mimi niweze kukutana na wageni. Karibu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti

HOJA ZA SERIKALI

Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji ya Maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika *PAC* Kwa Mwaka 2016/2017

Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha ili kulijuilisha Baraza la Wawakilishi hatua zilizofikiwa za utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yako ya Kudumu ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) kwa mwaka 2016. Naomba basi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza kwa kutuwezesha tena kukutana asubuhi hii kwa kutekeleza majukumu yetu muhimu katika kuwatumikia wananchi wenzetu. Namuomba Allah aniwezeshe kuwasilisha vyema taarifa hii.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyokuwa kwa taarifa nyengine zinazoendelea kuwasilishwa, uwasilishaji wa taarifa hii nalenga kutekeleza matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kama ilivyorekebishwa, sura ya tatu ifungu 43, kifungu kidogo cha 5, inayoelekeza uwajibikaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Baraza ko hili Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine, Kanuni ya 108(15) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la waka 2016 inaitaka kila Wizara kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo a Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi mara moja kwa mwaka katika mwezi wa Septemba au Oktoba. ata hivyo, kwa Ripoti ya PAC, Kanuni inamtaka Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuwasilisha utekelezaji wa Wizara zote za Serikali. Hivyo, katika kutekeleza matakwa hayo ya Kanuni za Baraza letu, taarifa hii awasilisha utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati ya PAC uliofanywa na Wizara na Taasisi mbalimbali za erikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena naomba nitumie fursa hii adhimu kumshukuru sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake makini na imani ake kwangu ya kunipa nafasi ya kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango. Namshukuru pia Mhe. Rais kwa uongozo yake anayotupatia kila siku ambayo kwa kweli kila mmoja wetu anaona imeleta manufaa na mafanikio akubwa katika nchi yetu. Namshukuru sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamo wa Pili wa Rais, kwa uniongoza na kunielekeza katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Mhe. Mwenyekiti, niruhusu pia nikushukuru Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid amshukuru pia Mhe. Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma, nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha wa Baraza hili kwa jinsi mnavyoliongoza Baraza letu kwa umakini na ufanisi kubwa. Shukurani hizi maalum nazitoa kwa dhati kabisa kutokana na mashirikiano makubwa ambayo natupatia taasisi yetu. Tunathamini sana mashirikiano haya ambayo tunaamini kuwa yataendelea siku hadi siku.

Kazi za Kamati, Ushauri na Maoni Yake:

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika PAC) inaundwa na Wajumbe 7 wenye weledi ambao nitawataja kama ifuatavyo:

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa – Mwenyekiti;
2. Mhe. Shaib Said Ali – Makamo Mwenyekiti;
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani – Mjumbe;
4. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi – Mjumnbe;
5. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf – Mjumbe;
6. Mhe. Rashid Makame Shamsi – Mjumbe; na
7. Mhe. Salma Mussa Bilal – Mjumbe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa wakati huo pia Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Zulfa Mmaka Omar walikuwa Wajumbe wa Kamati ya PAC.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii nimshukuru Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati yako ri kwa mashirikiano ya dhati, mashauriano na maoni na ushauri wa busara lakini wenye weledi mkubwa wanaoendelea kutupatia. Wizara yangu ina deni kubwa kwa Kamati hii kwa mashirikiano yake na miongozo ya na inayotupatia inayopelekea kuimarika kwa ufanisi wa utendaji Serikalini kwa Wizara na Taasisi zake.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka uliomalizika wa Fedha 2016/17, Kamati katika kutekeleza kazi zake, ilikutana a Watendaji wa Wizara, Taasisi za Serikali na baadhi ya Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo zilizohusika a kazi kwa kipindi husika, hatimae Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kushuhudia uhalisia wa aelezo ya Wizara, Taasisi na Kamati za Mfuko wa Jimbo. Kazi hii ilifanyika ndani ya wiki saba (7) katika wamu tatu (3) tofauti kama ifuatavyo:

i. Mzunguko wa Kwanza: tarehe 22/08/2016 – 09/09/2016;
ii. Mzunguko wa Pili: tarehe 31/10/2016 – 11/11/2016;
iii. Mzunguko wa Tatu: tarehe 16/01/2017 – 27/01/2017.

Mhe. Mwenyekiti, Kama nilivyotangulia kusema, katika ziara za kikazi zilizofanywa na Kamati ya Kuchunguza esabu za Serikali na Mashirika katika Wizara, Taasisi na Mashirika, Watendaji wote walifaidika sana na ajadiliano ya kina yaliyofanyika na hatimae maoni na ushauri mbalimbali wa Kamati. Naomba kwa mara yengine tena kuishukuru sana Kamati yote chini ya uongozi wa Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelekezo yaliyokuwa yakitolewa moja kwa moja wakati wa mizunguko ya kazi, pia Kamati iliwasilisha maagizo 228 kwa Wizara na Taasisi za Serikali baada ya kukamilisha ziara zake za waka wa fedha 2016/2017. Maagizo hayo yalilenga katika Wizara, Taasisi, Idara, Mashirika na Kamati za Mifuko ya Maendeleo ya Majimbo. Maagizo hayo yaligawika kama hivi ifuatavyo:

Maagizo 124 yaliyohitaji utekelezaji wa kudumu, ambapo utekelezaji wake utapaswa kuzingatiwa siku zote atika utendaji wa kazi za kila siku kupitia katika Wizara na Taasisi husika za Serikali na upo katika hatua tofauti a utekelezaji. Lakini pia maagizo 26 utekelezaji wake ulikamilika na maagizo 78 yanaendelea kutekelezwa.

idha, kati ya hayo, maoni 56 yalikuwa maalum kwa Wizara na Taasisi husika na yataendelea kutekelezwa.

Utekelezaji wa Maoni ya Kamati kwa
Wizara, Taasisi na Mashirika:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu ndio inayoratibu utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kuchunguza Hesabu za erikali na Mashirika Serikalini, imeyafanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa kwa kushirikiana na Wizara, Taasisi na Mashirika husika ambayo utekelezaji wake upo katika hatua kuu tatu (3) tofauti kama livyoeleza.Yapo yale Maagizo ambayo utekelezaji wake ni wakudumu (*Continuers*) utakuwa unaendelea. akini vile vile yapo ambayo utekelezaji wake umekamilika na yapo makundi ambayo utekelezaji wake naendelea hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa kutolea maelezo ya kina kwa utekelezaji wa kila ushauri wa Kamati lakini achelea kuwa haitoyumkinika kutokana na wingi wa maoni ya Kamati kama nilivyosema maoni 228. Lakini vile chache wa muda wetu hapa Barazani. Hata hivyo, utekelezaji huo umewasilishwa kwa kila Mjumbe katika adueli ambalo tayari Waheshimiwa Wajumbe mnayo. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kupitia utekelezaji huu amoja na Wizara yangu na kila Wizara au Taasisi iliyotajwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara na Taasisi zifuatazo ndizo zilizohusika kupata ushauri na maoni kutoka kwa Kamati:

1) Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi: Wizara hii ina maoni manane (8), sita (6) utekelezaji wake ni wa kudumu na mawili (2) utekelezaji wake unaendelea.

2) Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: ina maoni sita (6), ya utekelezaji wa kudumu ni matatu (3), agizo moja limekamilika kutekelezwa na mawili (2) yanaendelea kutekelezwa.

3) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali: Kamati ilitoa maoni manane (8) kwa Wizara hii, matano (5) utekelezaji wake ni wa kudumu, mmoja utekelezaji wake umekamilika na mawili (2) utekelezaji wake ni wa kuendelea.

4) Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira (Unguja): ina maoni matano (5), kati ya hayo matatu (3) ya kudumu, mawili (2) yanaendelea kutekelezwa.

5) Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira (Pemba): yenye maoni manne (4) ambayo yote ni ya utekelezaji wa kudumu.

6) Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Ofisi hii na Idara zake ina jumla ya maoni 44, kati ya haya maagizo 27 ni ya utekelezaji wa kudumu, utekelezaji uliokamilika ni maoni manne (4) na utekelezaji wa kuendelea ni wa maoni 13.

7) Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Tume ya Ukimwi): Kamati ilitoa maoni manane (8), sita (6) kati ya hayo ni ya kudumu kwa maana utekelezaji wake utakuwa ukiendelea na mawili (2) utekelezaji wake unaendelea hivi sasa.

8) Wizara ya Afya: ina maoni kumi nan ne (14), yenye utekelezaji wa kudumu ni manane (8), yaliyokamilika ni mawili (2) na yanayoendelea kutekelezwa ni manne (4).
9) Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake, Wazee na Watoto: maoni kwa Wizara hii ni manne (4), moja ni utekelezaji wake umekamilika, mawili (2) ya kudumu na moja linahitaji utekelezaji wa kuendelea.

10) Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Ofisi ilipokea maoni kumi na moja (11) ambayo manane (8) kati ya hayo utekelezaji wake ni wa kudumu, moja utekelezaji wake umekamilika na mawili (2) yanaendelea kutekelezwa.

11) Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA): maoni yaliyotolewa kwa Chuo ni sita (6), ambapo manne (4) ni ya kudumu na mawili (2) utekelezaji wake ni wa kuendelea.

12) Shirika la Umeme (ZECO): maoni yaliyotolewa kwa ZECO ni matano (5), manne (4) yamekamilika na moja linahitaji utekelezaji wa kuendelea.

13) Shirika la Magazeti: Shirika limepokea maoni manne (4), yenye utekelezaji wa kudumu ni mawili (2), moja utekelezaji wake umekamilika na moja linaendelea kutekelezwa.

14) Shirika la Meli na Uwakala: maoni matatu (3), kati ya haya moja utekelezaji wake ni wa kudumu na maagizo mawili (2) utekelezaji wake ni wa kuendelea.

15) Shirika la Utangazaji (ZBC): Shirika limepokea maoni manne (4) kutoka kwa Kamati, kati hayo moja limekamilika na matatu (3) yanaendelea kutekelezwa.

16) Chuo cha Kilimo (Kizimbani): Chuo kimepokea maoni matatu (3), mawili (2) ya kudumu na moja ni agizo linaloendelea kutekelezwa.

17) Chuo cha Uongozi wa Fedha, Chwaka (ZIFA): maoni yaliyotolewa na Kamati kwa Chuo ni manne (4), maoni yote yaliyotolewa ni ya kudumu.

18) Mamlaka ya Maji (ZAWA): Mamlaka ilipokea maoni sita (6), kati ya hayo manne (4) utekelezaji wake ni wa kudumu na mawili (2) ni ya utekelezaji wa kuendelea.

19) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (ZAA): maoni ni sita (6), kati ya hayo matano (5) ni ya kudumu na moja ni lenye utekelezaji wa kuendelea.

20) Mamlaka ya Uwekezaji (ZIPA): Mamlaka imepokea maoni sita (6), matano ya kudumu na moja la kuendelea.

21) Bodi ya Mapato (ZRB): maoni yaliyopokelewa ni sita (6), mawili ya kudumu, moja limekamilika na matatu (3) utekelezaji wake ni wa kuendelea.

22) Chuo cha Utumishi wa Umma (IPA): Chuo kimepokea maaoni sita (6), mawili (2) ya utekelezaji wa kudumu na manne (4) ni ya utekelezaji wa kuendelea.

23) Mfuko wa Barabara: Kamati ilitoa maoni 23 kwa Mfuko, kati ya hayo, manane (8) ya kudumu, matatu (3) yamekamilika na 12 utekelezaji wake ni wa kuendelea.

24) Mfuko wa Majimbo (CDF): maoni ya Kamati kwa Mfuko wa Jimbo ni 34, kati ya hayo 14 ya kudumu, 7 utekelezaji wake umekamilika na 13 utekelezaji wake ni wa kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, maoni yote yaliyotolewa na Kamati kwa Taasisi hizi ni 228, ambapo 194 yamehusisha Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali na maoni 34 yalihusisha Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Maagizo ya Jumla kwa Serikali:

Mhe. Mwenyekiti, kati ya maagizo yote yaliyotolewa (228), kumi na mbili (12) yaligusa kila Wizara na Taasisi Serikalini zinazopata fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ambapo Wizara yangu ndio inayowajibika kutekeleza Maagizo hayo, naomba niyataje maagizo hayo:

gizo la Kwanza

Ihe. Mwenyekiti, ilikuwa ni Serikali kuingiza fedha kwa Wizara/Taasisi za Serikali kama zinavyoomba, ili uepusha usumbufu kwa watendaji na jamii kwa ujumla, na kuwepo kwa mrundikano wa madeni katika Vizara/Taasisi hizo.

Ihe. Mwenyekiti, mgao wa fedha huzingatia Bajeti za Wizara/Taasisi, uwezo wa Kifedha kwa mwezi husika na upaumbele cha matumizi katika mwezi huo. Utaratibu huu unatokana na utaratibu uliopo wa Bajeti inayotegemea edh Taslim *(Cash Budget)* ambayo hutegemea utendaji wa makusanyo ya mapato kwa kipindi husika. Kadiri avyowezekana, Serikali imekuwa ikitoa fedha kulingana na Bajeti na mapendekezo ya Mtiririko wa Fedha *Cash Flow).* Kwa mwaka wa fedha 2016/17 ambapo hali ya mapato ilikuwa nzuri, takriban Wizara zote zilipata edha za kuendeshea Ofisi kwa mujibu wa Bajeti zao. Hata hivyo, serikali imepokea ushauri huo itautekeleza adiri hali ya mapato itakavyoruhusu na kulingana na mahitaji ya Taasisi.

Agizo la Pili

Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ni serikali kuzingatia utoaji wa fedha kwa kuchangia miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo ili kutoa sura nzuri yenye kuwashajihisha washirika wa maendeleo katika kujali utoaji wao wa fedha katika kuendeleza miradi ya nchi.

Ihe. Mwenyekiti, serikali kimsingi inakubaliana na ushauri wa Kamati na kwa kiasi kikubwa inaendelea uutekeleza. Kwa mwaka 2016/17 Serikali ilitumia TZS 51 bilioni kati ya TZS 71 bilioni zilizopangwa kutumika ama mchango wa serikali kwa kazi za maendeleo. Kiasi kilichobakia hakikuweza kutumika kwani kilipangwa wa ajili ya mchango wa serikali katika mradi wa ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Uwanja wa Ndege wa beid Amani Karume ambao kwa bahati mbaya ujenzi haukuendelea katika mwaka huo. Kwa mwaka 2017/18 erikali imepanga kutumia bilioni TZS 116.1 kama mchango wake kwa kazi za maendeleo ikiwa ni ukuaji wa silimia 127.6 kutoka kima halisi kilicholipwa mwaka jana.

Agizo la Tatu

Ihe. Mwenyekiti, ni malipo ya fedha za kigeni yanayofanywa na Mfuko Mkuu wa Hazina na kuingizwa miamala atika wizara/taasisi husika kupitia katika mfumo uliopo wa *IFMS (dummy transactions)* kuweka sawa umbukumbu za kihesabu katika bajeti zao.

Ihe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa serikali imekuwa ikilipa Ankara zozote zinazohitaji malipo ya fedha za kigeni e ya mfumo wa IFMS na baadaye kurikodi katika IFMS kiasi hicho kwa fedha za Kitanzania bila ya kutoa tena dha *(Dummy Transaction)* ili kuwezesha malipo hayo kuwemo katika matumizi ya serikali. Ili kurekebisha hali i, tokea Novemba 2016 serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kutumia wataalamu waliounganisha tandao huu *(Soft-Tech Consultant Ltd)* kwa kushirikiana na wataalamu wetu wa ndani wameanza kufanya kazi ubadilisha mtandao huwo na wanatarajia kujaribu tena marekebisho hayo katika mwezi huu wa Oktoba.

Agizo la Nne.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Wizara/Taasisi zote za serikali kuwa makini wakati zinapofanya malipo ili kuepusha kasoro zisizo za lazima pamoja na kuhakikisha kwamba matakwa ya sheria na kanuni za nchi inafuatwa na kutumia busara wakati wa kutoa masurufu ili kuepusha lawama zisizo za msingi, pamoja na kulinda usalama wa watendaji serikalini.

Ihe. Mwenyekiti, kimsingi, hili ni mojawapo ya mambo ambayo yanapaswa kutekelezwa muda wote. Serikali akubaliana na maoni haya ya Kamati yanayolenga kuimarisha usimamizi wa fedha za Umma na utawala bora

chini. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara/Taasisi nyengine zote za Serikali iko tayari kutekeleza ushauri uo kwa kufuata misingi ya Sheria na Kanuni za usimamizi wa Sheria za Fedha na Sheria nyenginezo za nchi na aasisi zote, hii ni wajibu wa msingi kufuata sheria na taratibu zinazoelekeza katika matumizi ya usimamizi wa dha za umma.

gizo la Tano

Mhe. Mwenyekiti, serikali kuzingatia kuwepo kwa mipango yake kwa mujibu wa uwezo ilionao na sio kupanga mipango mingi wakati mmoja na hatimae kuwaweka katika kipindi kigumu watendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme serikali imepokea ushauri huu wa Kamati. Lakini pia niseme jitihada zimekuwa zikichukuliwa kuweka vipaumbele vya Miradi ya kutekelezwa kwa kuzingatia uwezo wa serikali. Serikali pia ilianzisha na inasimamia Mfuko wa Miundombinu kwa lengo la kuharakisha maendeleo ya Miundombinu ya msingi kwa kutumia fedha zetu za ndani. Jitihada za kutekeleza miradi ya vipaumbele, ikiwemo kupitia Mfuko huo wa Miundombinu zitaendelezwa.

Agizo la Sita

Serikali ihakikishe inakamilisha miradi yote iliyoanza ndipo ianze na miradi mipya ili kuepusha kitendo cha kuzitaka taasisi zake kukamilisha wenyewe miradi yao kwa kutumia fedha za matumizi mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake hukamilisha Miradi ya Maendeleo na zaihamishiwi katika matumizi ya Kazi za Kawaida. Hata hivyo, ni vyema ikaeleweka kuwa Miradi ya Maendeleo ina utaratibu wake wa kuidhinishwa sambamba na Bajeti yake. Miradi hiyo huibuliwa na Sekta na kukubaliwa na Kamati ya Mipango kabla ya kuwasilishwa Baraza la Mapinduzi kama sehemu ya mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na hatimae kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi kwa kuidhinishwa. Taasisi zinazotekeleza Miradi nje ya utaratibu huu hazihesabiwi kuwa zinatekeleza Miradi ya Maendeleo kwa madhumuni ya Bajeti iliyoidhinishwa na Baraza hili tukufu.

gizo la Saba

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Wizara/taasisi za serikali kuhakikisha zinatekeleza maoni ya kamati za Baraza la Wawakilishi, kwani baraza la Wawakilishi ndilo lenye mamlaka ya kuisimamia serikali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imepokea maoni haya ya Kamati na kimsingi inakubaliana nayo. Kama alivyotangulia kutamka, Uwasilishaji huu wa Taarifa za Wizara mbalimbali za utekelezaji wa maoni ya Kamati ya Kudumu za Baraza ni kieleelzo cha utekelezaji huo wa matakwa ya Katiba na Kanuni zetu. Hapana shaka kuwa serikali itaendelea kutimiza wajibu wake huu muhimu.

Agizo la 8

Mhe. Mwenyekiti lilikuwa Serikali kuwa makini inapofanya mabadiliko ya mishahara kwa watendaji wake ili kuepuka malalamiko yasio ya lazima na vile vile kuzingatia uwepo wa fedha za marekebisho ya mishahara hiyo na siyo ziada ya fedha inayohitajika kufanyika marekebisho kutoka bajeti za Wizara au Taasisi za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa utaratibu wa sasa na naomba hapa nisisitize kwa utaratibu wa sasa Serikali hutenga fedha katika bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Idara ya Bajeti kwa

ajili ya kukidhi haja ya marekebisho yoyote makubwa na jumla yanayohusiana na mishahara kwa maana *Salary Adjustment* hivyo tayari ushauri huu wa kamati umeshakwisha zingatiwa na utakelezwa na Serikali.

Agizo la 9
Ni Serikali ihakikishe kwamba Kamati za Mfuko wa Majimbo zitafuatwa taratibu zilizoelekezwa katika sheria na zinafuatwa miongozo husika.

Mhe. Mwenyekiti, huu ndio ushauri mwengine muhimu kutoka katika Kamati yako ya Kuchunguza Hesabu za Serikali ushauri unatutaka Waheshimiwa Wajumbe na Kamati zetu za Maendeleo ya Jimbo kuwa makini na kuonesha mfano mzuri wa Usimamizi wa Fedha za Umma ili hatimaje nasi tuweze kuisimamia vyema Serikali.

Kimfumo kwa sasa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imechukuwa hatua mbali mbali ikiwemo mapitio ya sheria namba 4 ya mwaka 2012 ya Mfuko wa Jimbo miongoni mwa marekebisho Murugenzi wa Serikali za Mitaa ndiye atakayekuwa Katibu wa Kamati ili kujenga uwezo wa Kamati za Jimbo pamoja na kuimarisha uthibiti wa mapato na usimamizi bora wa matumizi ya fedha na kuhakikisha taratibu nyengine za kiutendaji vinafuatwa kikamilifu.

Agizo la 10
Mhe. Mwenyekiti, ni Serikali kuzipatia fedha kwa wakati Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ili ziweze kutekelezwa vyema majukumu yao Mhe. Mwenyekiti, Serikali imepokea ushauri huu na itaendelea na utekelezaji wake hata hivyo kama ilivyoelezwa matumizi bora ya mfuko huu yanahitaji uwazi na uwajibikaji kutoka kwa Kamati za Jimbo ni vyema kamati hizo zitekeleza majukumu yake kwa kufuta sheria ili fedha nazo ziweze kuingizwa na kufanikisha adhma ya kuanzishwa mfuko huo ya kuwaondolea wananchi adha ndogo ndogo zinazowakabili. Kamati za Jimbo zihakikishe marejesho kwa wakati na ukamilifu ili fedha nyengine ziweze kutolewa.

Agizo la 11
Serikali kuhakikisha kuwa taasisi zake zote zinatunza viambatanaisho muhimu vya nyaraka za matumizi yanayofanywa na Serikali, uwekaji ulio bora wa nyaraka za malipo na uhifadhi wa nyaraka asili kwa maana *original document* ambazo ndizo zenye nguvu kisheria. Aidha kamati imewataka watendaji kufanya kazi kwa uadilifu katika matumizi ya fedha za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imepokea ushauri huu ambao pia unabeba matakwa ya sheria, mafunzo ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha na kanuni zake yatatolewa kila baada ya muda kuwakumbusha watendaji kurekebisha kasoro zinazojitokeza katika utekelezaji wa kazi za kila siku za kiuhasibu. Aidha inatarajiwa kuwa Idara huru ya ukaguzi wa ndani iliyoanzishwa hivi karibuni na Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein itasaidia katika kuimarisha kufuatwa kwa matakwa ya sheria na misingi ya kazi za kiasili Serikalini katika Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kabla maelezo niliyoyatoa ni muhtasari tuu wa Taarifa ya Utekelezaji wa maoni ya Kamati ya PAC Taarifa ya Utekelezaji kwa kila ushauri wa Kamati imeambatanishwa kwa urahisi Waheshimiwa Wajumbe kuusoma na kuuwelewa.

Kamati ya PAC imepata muda wa kupitia kwa kina na kupata maelezo ya ziada ya utekelezaji huo kutoka kwa Wizara na Taasisi husika. Kwa mara nyengine tena naipongeza sana Kamati ya PAC kwa kazi kubwa iliyofanya ya kutowa maoni na hatimae kufuatilia utekelezaji wake.

Naomba pia niendeleza tuu ahadi yangu kwa niaba ya Serikali kuwa Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake zote itaendelea kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na kazi za Kamati za Kudumu za Baraza hili Tukufu, itatekeleza kwa makini ushauri na maoni ya kamati hizo na hatimae kutimiza wajibu wake wa kutoa maelezo ya utekelezaji kama Katiba ya Nchi na Kanuni za Baraza zinavyoelekezwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya Muhtasari wa Utekelezaji naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni ya Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali PAC kwa mwaka 2016/2017 kama ilivyoaambatanishwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri nakushukuru sana kwa uwasilishaji wako mzuri sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kuthibiti Hesabu za Serikali na Mashirika.

Mhe. Rashid Makame Shamsi (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika):

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti**,** kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya PAC naomba sasa nami niwasilishe Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kuthibiti Hesabu za Serikali na Mashirika PAC juu ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati hiyo kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, kwa kutujaalia uhai, uzima na uwezo wa kukutana hapa leo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu muhimu ya kikatiba ya kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, naomba nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili kusema machache na ya muhimu, yanayohusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya PAC ya mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mhe.Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dr Khalid Salum Mohamed kwa kuweza kuwasilisha hapa Barazani Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya PAC kama ambavyo kanuni ya 108 fasili ya 15 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016, inavyosomeka.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa maagizo hayo yalikuwa ni mengi na tumeyasikia yaligusa Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali pamoja na Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani maalum kwa watendaji wa Afisi ya Baraza wakiongozwa na Katibu wa Baraza Ndugu Raya Issa Msellem kwa maelekezo na ushauri wao kwa Kamati wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa namna ya pekee kabisa napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wenzangu wa Kamati ya PAC kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ushirikiano mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe hawa wamekuwa wakishiriki mijadala ya vikao vya Kamati kwa umakini na umahiri mkubwa na kutumia vyema Elimu, Taaluma, Uzoefu na Vipaji vyao katika kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa za Hesabu pamoja na taarifa nyengine zinazoletwa katika Kamati, na kutoa ushauri ambao umeiwezesha Kamati yetu kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Nawashukuru pia Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wao, naomba kuwatambua Wajumbe na Makatibu hao wa Kamati kama ifuatavyo :-

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Mwenyekiti.
2. Mhe. Shaib Said Ali - Makamo Mwenyekiti.
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi - Mjumbe
5. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mjumbe
6. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Mjumbe
7. Mhe. Salma Mussa Bilali - Mjumbe
8. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
9. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 108 fasili ya 15 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016, Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya PAC iliwasilishwa na kujadiliwa katika Kamati, katikati ya mwezi wa Septemba, 2017.

Mhe. Mwenyekiti, Maagizo ya Kamati ya PAC yaliyomo katika Ripoti ya Kamati kwa mwaka 2016/2017 iliyowasilishwa katika Baraza lako Tukufu tarehe 28/2/2017, yanatokana na kazi iliyofanywa na Kamati hii ya kuzichunguza na kuzifuatilia Ripoti nne za Ukaguzi uliofanywa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ripoti zenyewe ni hizi zifuatazo:-

1. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Wizara ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2013/2014,

2. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2013/2014,

3. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF) kwa kipindi cha mwaka 2011 hadi 2015 na

4. Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika sana na Ripoti hiyo pamoja na ufafanuzi uliokuwa ukitolewa na watendaji wa Wizara na Taasisi husika, ijapokuwa katika Ripoti hiyo kulikuwa na baadhi ya kasoro ndogo ndogo ambazo Kamati ilizibaini na iliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zinazohusika kuzirekebisha kasoro hizo. Pamoja na hayo, Mhe. Mwenyekiti Kamati imeona ni vyema kusema machache yaliyo muhimu kwa maslahi ya nchi hii na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti**,** katika utekelezaji wa Maagizo yanayohusiana na Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya SMZ, Kamati imefarajika kuona kuwa Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa za kuufanyia marekebisho na majaribio Mfumo wa Matumizi ya Fedha za Pamoja (*IFMS*) ili mfumo huo uweze kuchukua pia fedha za kigeni kama vile Dola za Marekani badala ya kuchukua aina moja tu ya fedha ambazo ni fedha za Tanzania kama ilivyo hivi sasa. Ni imani yetu kuwa marekebisho na majaribio ya mfumo huo wa (*IFMS*) yatakamilika katika muda uliopangwa ili kuepusha kutumika kwa mfumo mwengine unaotiliwa mashaka, maarufu ni *DUMMY*.

Mhe. Mwenyekiti**,**katika utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yanayohusiana na Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Taasisi za SMZ, Kamati inalipongeza Shirika la Umeme, Zanzibar (*ZECO*) chini ya usimamizi wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kuweza kufanya kikao na Shirika la Umeme, Tanzania (*TANESCO*) tarehe 4, Mei, 2017 na tarehe 7, Mei 2017 ili kujua deni halisi ambalo *ZECO* inadaiwa na *TANESCO* ambapo kutokana na hatua hiyo iliafikiwa kuwa deni halisi ni Tsh. 57.8 billioni hadi mwezi wa Aprili, 2017.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati pia imeridhishwa na jitihada za Serikali za kulipa deni la matumizi ya umeme kwa Taasisi zake ambayo ni malimbikizo ya madeni hadi mwezi wa April, 2017, fedha ambazo hulipwa moja kwa moja kwa *TANESCO* ili kupunguza deni inalodaiwa *ZECO* na *TANESCO* ambapo hadi mwezi wa Juni, 2017 jumla ya Tsh 13 bilioni zilikuwa zimeshalipwa. Hii ni hatua muhimu ya kujivunia kwani Wahenga walisema "Dawa ya deni ni kulipa"

Mhe. Mwenyekiti**,** katika utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yanayohusiana na Ripoti ya Hesabu za Serikali kwa Mfuko wa Jimbo (CDF), Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutilia mkazo katika kuisimamia na kuifuatilia kwa karibu zaidi miradi ya maendeleo inayotekelezwa kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo na kuhakikisha kuwa taratibu za kisheria zinazoongoza miradi hiyo pamoja na Sheria nyengine za nchi zinafuatwa kikamilifu ili lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huo liweze kufikiwa,

Mhe. Mwenyekiti**,**aidha, kuna haja kubwa kwa Serikali kutoa elimu ya kutosha na ufafanuzi wa kina juu ya suala la posho la vikao kwa Kamati za Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo kwa kuwa imebainika kuwa baadhi ya Kamati hutumia fedha nyingi za Mfuko kwa ajili ya kulipa posho la

vikao na viwango vya posho hilo hutofautiana baadhi ya Kamati Mwenyekiti hutoa fedha zake binafsi kulipia posho la vikao.

Mhe. Mwenyekiti**,**tunashauri hili kwa kuwa kifungu cha 27 cha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Namba 4 ya 2012 kinaeleza kuwa gharama za uendeshaji wa shughuli za Mfuko zitoke nje ya bajeti ya Mfuko na kwa kuwa fedha za Mfuko ni chache na zinatolewa kwa ajili ya kuleta maendeleo ndani ya Jimbo. Hivyo, fedha hizo kutumika kinyume na lengo hilo ni kwenda kinyume na Sheria ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa msingi huo tunaiomba Serikali katika mwaka wa fedha ujao itenge bajeti maalum kwa ajili ya uendeshaji wa Kamati za Mfuko na kwa kuwa hivi sasa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 imeshapita, tunashauri gharama za uendeshaji zitoke katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mhe. Mwenyekiti**,** sambamba na hilo, Kamati inaiomba Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuzihimiza Kamati za Mfuko wa Jimbo zilizopo hivi sasa kuikamilisha kwanza miradi iliyokuwa haijakamilika, kabla ya kuibuliwa kwa miradi mipya ili kuepusha kuwepo kwa milolongo au mlolongo wa miradi isiyokamilika ambayo haitakuwa na tija kwa wananchi wetu. Aidha, ni wajibu wa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu ambao ni Wenyeviti wa Kamati za Mfuko wa Jimbo kusimamia vyema miradi hiyo na kuhakikisha kuwa kasoro mbali mbali zilizojitokeza katika usimamizi na utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Jimbo katika kipindi kilichopita hazitokei tena katika kipindi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yanayohusiana na Ripoti ya Mfuko wa Barabara, Kamati imefarajika kuona kuwa Serikali ina mpango wa kununua mitambo mitatu mipya ya lami inayojumuisha mtambo wa kupikia lami, mtambo wa kutandazia lami na mtambo wa kusambaza lami ya maji pamoja na ununuzi wa lami ya tani 1,700 ambapo jumla ya Tsh bilioni 5 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati ya PAC ililibaini tatizo hilo la uchakavu na uhaba wa vifaa vya matengenezo ya barabara na kuishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya vifaa hivyo. Ni wazi kuwa hatua hii ya Serikali itasaidia sana kutatua tatizo sugu la uchakavu na uhaba wa vifaa linaloikabili Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (UUB) ambalo huzorotesha sana katika suala zima kazi za ukarabati wa barabara hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati pia inaendelea kuisisitiza Serikali kufanya jitihada za makusudi za kuhakikisha kuwa barabara mbali mbali zinazojengwa, zinakuwa na mitaro yaani *drainage system* ili kuepusha uharibifu unaofanywa na maji yanayoingia katika maeneo ya makaazi ya wananchi wetu lakini vile vile karibu na barabara hizo kama ilivyoonekana katika baadhi ya maeneo ya barabara ya Fuoni na barabara ya Daraja Bovu (Mkapa Road).

Mhe. Mwenyekiti**,** aidha Kamati inaendelea kuihimiza Mamlaka ya Maji (ZAWA) kwa kushirikiana na Idara ya UUB pamoja na mamlaka nyengine zinazohusika, kukaa pamoja na kuwa kuhakiki bomba zote za maji safi zilizopita katika mitaro ya maji machafu hususan kwenye *culvert* zikiwemo za maeneo ya Tibirinzi (Pemba) na Kijichi (Unguja) na kuhakikisha kuwa

bomba au *culvert* hizo bomba hizo za maji safi zinahamishwa mara moja ili kuwanusuru wananchi wetu na janga la maradhi ya mripuko ikiwepo kipindupindu.

Mhe. Mwenyekiti**,** katika hotuba ya Kamati iliyowasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu tarehe 18 Mei, 2017 tuliipongeza Serikali kwa kuiruhusu Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kuendelea na zoezi la uajiri wa wafanyakazi wapya, zoezi ambalo lilikwama kwa kipindi kirefu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa tunapenda kuliarifu Baraza lako kwamba hadi tunawasilisha maoni haya ya Kamati suala hili bado halijakamilika na tatizo linaloelezewa ni kuwa Bodi ya Ofisi ya Mdhibiti imemaliza muda wake tangu mwezi wa Oktoba, 2015. Bodi ambayo kwa mujibu wa kifungu cha 9, fasili ya (1a) cha Sheria ya Kuanzishwa kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi, Nam.8 ya 2003 ndio yenye mamlaka ya kupitisha ajira za taasisi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa suala hilo limeshakua muda mrefu wa takriban miaka miwili sasa. Hivyo, Kamati inaiomba serikali kuliangalia suala hili kwa uzito unaostahili ili zoezi la uajiri likamilishwe na hasa ikizingatiwa kuwa ofisi hii haijaajiri watendaji tangu mwaka 2010 na hivi sasa inahitaji takriban watendaji 50 kwa ajili hiyo. Bila shaka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu ina changamoto ya rasilimali watu na ndio maana inashindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake ya ukaguzi kwa wakati, kwani hadi hivi sasa imeshafanya ukaguzi na kutoa ripoti zake za mwaka 2014/2015. Kitendo ambacho kinaifanya Ofisi ya Mkaguzi kuwa nyuma kiukaguzi kwa miaka miwili.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa Kamati ya *PAC* inaendelea kuzipitia Ripoti za Ukaguzi za miaka ya nyuma 2014/2015. Hata hivyo, Kamati yako hairidhishwi na hatua hiyo hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya wakati hutoa ushauri ambao tayari serikali imeshaufanyia kazi, au kushindwa kutekeleza jukumu lake kutokana na kuwa baadhi ya wahusika wa jambo fulani wameshafariki au wameshaondoshwa madarakani au wameshastaafu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kulihakikishia Baraza lako Tukufu kuwa, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) itaendelea kusimamia na kuchunguza matumizi ya serikali kwa kuhakikisha matumizi hayo yanafanyika kwa mujibu wa sheria na kwa kuzingatia ufanisi na uadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia napenda kutoa shukrani za dhati kwako na kwa viongozi na watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali kwa ushirikiano wao mkubwa na Kamati hii ikiwa ni pamoja na kutoa maelezo na ufafanuzi unaohitajika wakati wa Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ilipokuwa ikijadiliwa katika Kamati, na hasa ikizingatiwa kuwa maagizo ya Kamati hii yalikuwa yanazigusa Wizara na Taasisi nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii, Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya uwasilishaji huo sasa nichukue fursa hii nikuombe ili na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji wa hotuba hii ya taarifa hii ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati. Mhe. Mwenyekiti, nakuomba.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, katika michango yangu nikiwa Mjumbe wa Kamati hii niende katika agizo la Kamati Nam.10 katika ukurasa wa 16.
Mhe. Mwenyekiti, kamati iliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kwamba juu ya suala zima la maendeleo ya Mfuko wa Jimbo (*CDF*) kuweza kutekeleza vyema majukumu yake. Katika majibu yake wizara ilieleza kama ifuatavyo.

Serikali imepokea ushauri huo na itaendelea na utekelezaji wake, hata hivyo imeelezwa matumizi bora ya mfuko huo yanahitaji uwazi, na uwajibikaji kutoka kwa Kamati za Jimbo. Ni vyema kamati hizo zitekeleze majukumu yake kwa kufuata sheria ili fedha nazo ziweze kuingizwa na kufanikisha azma ya kuanzishwa mfuko huo na kuwaondolea wananchi matatizo na adha ndogo ndogo. Aidha, Kamati za Jimbo zihakikishe zinafanya marejesho kwa wakati na ukamilifu ili fedha nyengine ziweze kutolewa.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama kamati katika suala zima la Mfuko wa Jimbo, kamati imeweza kutembelea karibu majimbo yote ya Unguja na Pemba, ingawa katika ripoti hii ambayo tunaiwasilisha ni majimbo tisa ambayo yameingia katika ripoti hii. Aidha, kamati imegundua changamoto mbali mbali, lakini changamoto kubwa sana ilikuwa ni suala zima la marejesho. Aidha, kuna baadhi ya majimbo unakuta kwamba wana upungufu wa vielelezo, aidha kucheleweshe kupeleka marejesho. Na baadhi ya majimbo Mhe. Mwenyekiti, unakuta hata vile vielelezo juu ya utekelezaji wa miradi unakuta havipo. Sasa hili ni tatizo.

Lakini vile vile niwapongeze wale Wenyeviti ambao walikuwa wanasimamia mifuko hii ya maendeleo katika majimbo ambayo tumeyatembelea kwa mashirikiano makubwa pamoja na Makatibu wao pamoja na Wajumbe wa Kamati hizi. Jambo la kusikitisha ni kwamba tulikosa baadhi ya mashirikiano katika baadhi ya majimbo na kwa Pemba yalikuwa ni majimbo mawili, lakini kwa Unguja tulikosa mashirikiano ya kuweza kukagua mifuko hii kwa majimbo matatu.
Mhe. Mwenyekiti, kutokana na tatizo la urejeshaji wa marejesho, kamati inaziomba sana Kamati za Maendeleo za Mifuko ya Jimbo na hususan hivi sasa ambapo waheshimiwa sisi ndio ambao tunazisimamia, basi tunaomba sana ndugu Wajumbe na ndugu Wenyeviti wa Kamati hizi tufanye marejesho haraka kwa zile fedha ambazo tumetiliwa za 2016/2017. Kwa sababu kufanya hivyo ndivyo Wizara ya Fedha na Mipango itakavyoweza kuziingiza fedha ambazo kwa maelezo ya Mhe. Waziri kwamba fedha hizo ziko tayari tunasubiriwa sisi tuweze kufanya marejesho. Kwa hivyo, niwaombe sana Wenyekiti wenzangu wa kamati hizo tufanye marejesho hayo haraka ili kuweza kuingiziwa fedha hizo kwa sababu wananchi wana matarajio makubwa sana na Mifuko hii ya Maendeleo kutokana na changamoto nyingi ambazo ziko katika majimbo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nitumie fursa hii kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* kwa wale Waheshimiwa Wawakilishi ambao mpaka sasa hawajafanya marejesho, na wana matatizo ya kuweza kuratibu hayo marejesho basi niwaombe sana Wawakilishi wenzangu waione kamati na hususan mimi ili kuweza kuwapa maelekezo mazuri ya kuweza kurejesha marejesho yao kwa wakati ili kuepuka kwa sababu Mfuko huu wa Maendeleo unakaguliwa na taasisi tatu. Unakaguliwa na Taasisi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuweza kujiridhisha kama utekelezaji umekwenda vizuri, lakini vile vile unakaguliwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali. Lakini *PAC* ni chombo cha tatu ambacho kinapita, sasa sisi tutaona tabu sana kwa Waheshimiwa Wawakilishi kuweza kuja kupata matatizo katika ukaguzi, kwenye miradi yao. Na hususan tunapotembelea sisi kama kamati kwa kweli mivutano na wawakilishi wenzetu itakuwa sio jambo la busara. Kwa hiyo, niombe sana Waheshimiwa Wawakilishi kufanya marejesho kwa wakati na yaliyotimia na msaada wa kisheria na wa taratibu Kamati ya *PAC* iko tayari kutoa kwa Waheshimiwa Wawakilishi.

Baada ya kusema hayo nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii kuwa Mjumbe wa mwanzo wa kuchangia. Na niwaombe sana Waheshimiwa Wawakilishi kuweza kuijadili na kuichangia hotuba hii na hatimae kuweza kuiunga mkono. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa niaba ya Mwenyekiti, kwa mchangio wako na mimi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wajitokeze kwa wingi kuchangia hoja hii.

Kwanza waheshimiwa nimepata barka ya wageni wengine hapa mbele yetu, tunao wageni wa Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma, wageni hawa wanatoka *Dodoma Youth Development Organization* (Doyodo) na jumla yao ni watano. Naomba niwatambue kwa majina wengine wenyewe ni:

1. Ndg. Rajab Juma Muhunga - Mwenyekiti
2. Ndg. Rashid Msonga Rashid - Makamo Mwenyekiti
3. Ndg. Betrice Ngerara - Afisa Nidhamu
4. Ndg. Amir Mohammed - Afisa Habari
5. Ndg. Abdul-latif Sappi - Afisa Habari Msaidizi.

Niwambie nyote karibuni katika ukumbi wetu huu wa Baraza la Wawakilishi, karibuni sana.(*Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na michangio, mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, akifuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said. Waheshimiwa hao, wote hawapo ndani Mhe. Ali Suleiman Ali endelea kuchangia.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kupata fursa hii fupi kabisa kuichangia taarifa hii ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze kwa dhati Mhe. Waziri na taasisi zake zote kwa kuhakikisha kwamba fedha zetu zinasimamiwa vyema na zinatumika ipasavyo. Lakini pia niipongeze Kamati yetu ya *PAC* kwa kazi yao nzuri na muhimu hasa tukizingatia Mhe. Mwenyekiti bila ya ufatiliaji wa taarifa hizi za Kamati basi mapungufu yanaweza kujitokeza na mambo ya hapa na pale yakatokea ya kurudisha nyuma maendeleo yetu hasa katika makusanyo wakati wa kutumia au utumiaji wa fedha zetu.

Mhe. Mwenyekiti, *PAC* ni sehemu moja wapo wa Kamati zetu za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zinazoshughulika na wizara zote za serikali na maidara na mashirika mbali mbali.

Lakini kwa ujumla naipongeza kwa kugundua mengi ambayo tukikaa vizuri na wenzetu wakatoa taaluma zaidi kama alivyotoa Makamu Mwenyekiti nampongeza sana basi tutafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesimama hapa nitakuwa na machache sana. Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa bahati nzuri imetuwekea Mfuko wa Maendeleo kupitia Baraza la Wawakilishi wa milioni 20 kwa kila mwakilishi mwenye jimbo. Lakini fedha hizi Mhe. Mwenyekiti, zina taratibu zake ama zilielezwa vizuri na kamati pamoja na Mhe. Waziri. Kwa hivyo, mimi nitoe ombi maalum, nimemfatilia sana msoma taarifa hii kupitia Mwenyekiti wa Kamati kwamba ametoa darasa zuri na kila siku mimi husema mheshimiwa kuiga zuri sio vibaya, kuiga baya ndio vibaya zaidi. Kwa hivyo, mimi nampongeza kwa dhati kwa ualimu wake aliokuwa nao na taaluma yake aliyokuwa nayo. Fedha zina utaratibu wa matumizi na fedha zilikoanzia ndio zinakorudishwa yaani marejesho, kwa hivyo mimi kwa upande wangu nimelipokea mikono miwili hili na nitakuwa wa mwanzo kumwendea yeye, ingawa nimeshazimaliza zamani fedha hizo. Mhe. Mwenyekiti, nitahakikisha kutoka leo mpaka Jumatatu *return* yangu nitafanya kwa afisi ambayo inayohusika kurejesha matumizi ya fedha hizi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ukishazipata fedha zina taratibu zake kama nilivyosema, lakini mara nyingi huwa tunababaika wengine, utaona fedha umeshaipata jambo la kufanya hulijui. Kwa hivyo, mimi nishauri na namshauri sana Mhe. Rashid Makame Shamsi, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni akubali utumishi mwema kuwasaidia wote waliokuwemo humu kwa wale ambao tuna kizungu zungu cha hapa na pale. Naamini mheshimiwa hilo litatusaidia sana na yale madai ya kusema kwamba mfuko wa mara ya pili tunautaka tena na tunautaka kweli kwa sababu tumeshamaliza mheshimiwa mara ya kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, pia niishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kupitia shughuli zake hizi kwa adhma hii njema ya mfuko huu. Nimshukuru Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwamba wao hawangojei kuitwa, wao wanatusubiri sisi tuwe tayari. Kwa hivyo, naamini Mhe. Mwenyekiti, hili ni suala zuri ambalo litatupa manufaa katika shughuli zetu mbali mbali za kuendeleza mazuri katika majimbo yetu mbali mbali kwenye nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kuna Mfuko wa Barabara, uwekezaji katika ukingo barabara ya Amani/Mtoni. Hili Mhe. Mwenyekiti, nimeona uendeshaji wa mkataba ulivyokwenda na matumizi yake na maendeleo yake yameonekana yamekwenda vizuri. Kwa hivyo, na hili nimpongeze Mhe. Waziri lakini takriban katika masuala yote yaliyokuwepo hapa hakuna suala baya kuliko yote ambayo yametajwa, na naamini kwamba waheshimiwa sote tumuunge mkono Mhe. Waziri wa Fedha, tuwaunge mkono wakusanyaji wa mapato, mapato haya yapatikane kwa wingi ili maendeleo yakuwe kwa haraka kama yanavyoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, leo tuna mashirika yetu kama vile Shirika la Umeme, Mamlaka ya Maji, kuna Bandari, kuna Uwanja wa Ndege na mashirika mengine yote ambayo tunayategemea, lakini bila ya kuwekewa utaratibu huu basi fedha huwa zinaweza kupotea bila ya mpango. Kwa hivyo, kamati inafanya kazi zake ipasavyo na ndio wajibu wake, kwa sababu moja katika Kanuni zetu za Baraza hilo linatuhusu.

Mhe. Mwenyekiti, leo katika kupongeza hilo na katika Shirika la Umeme (*ZECO*) pamoja na jitihada zao wanazozifanya. Kwanza nilipongeze Shirika la Umeme kwa kuendelea kulipa deni la *three billion* kama sikosei kwa mwezi, hilo ni suala kubwa. *Two billion* wanatoa wao na *one billion* inatola Mfuko wa Serikali. Kwa hivyo, nilipongeze kwa dhati kwa hili na naamini hiyo ni sehemu moja tosha ya kuhakikisha kwamba maendeleo yanapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pamoja na huo ugumu waliokuwa nao, si ugumu maama ukilipa ndio inavyotakiwa. Na mimi leo naipongeza serikali kupitia Shirika la Umeme, leo mbio za Mwenge zimezindua mradi wangu mkubwa niliokuwa napiga kelele wa Kwarara Madina kwa takriban hesabu ya mara moja wametumia *one seventy five million* (175,000,000). Mhe. Mwenyekiti, si jambo dogo tuipongeze serikali na tusaidie kila penye kasoro tuielekeze ili mahitaji haya yapatikane kwa manufaa ya nchi yetu. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho niwaombe watendaji wote wa mawizara yote zinapokwenda kamati zetu wajue wajibu wao na wajue wanapokwenda kamati hizi huwa sio Mahakimu, lakini utaratibu uwepo. Kwa hivyo, niseme tu kwamba kazi zao kubwa kutoa mashirikiano mazuri na mashirikiano mazuri ndio kutatua matatizo yanayojitokeza katika sehemu zao na maendeleo yanakuwa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa kwa leo baada ya kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote nampongea ndugu yangu Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa jitihada zake kubwa na Mwenyezi Mungu atakuwa hayuko radhi kama sitompongeza meneja na watendaji wake wote ma-*engineers* wake na wafanyakazi wote wa Shirika la Umeme kwa kazi nzuri iliyofanywa Jimbo la Kijito Upele sehemu ya Kwarara Madina.(*Makofi*).

Mheshimiwa haki yake tumpe naweza kusema Mhe. John Pombe Joseph Magufuli juzi amemteuwa Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki na mimi labda nitampa jina hilo kwa uhodari wake na umahiri wake katika jitihada za kufuatilia mambo mbali mbali.

La mwisho baada ya hayo niseme tu kwamba kuna mengine tutakuja kutoa taarifa katika Mamlaka ya Maji nini tunataka ili tufanikiwe na tuiombe serikali itusimamie ili tufanikiwe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache kwa heshima kabisa naikubali au naipokea taarifa hii na nimeunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa namwita Mhe. Suleiman Sarahan Said aendelee na mchango wake.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa ya kuchangia ili niweze kufanikisha katika masuala yetu haya ya maagizo ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nimpongeze sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein katika jitihada zake za kuhakikisha kwamba Zanzibar inapiga hatua za kimaendeleo na wananchi wake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini bado kuna baadhi ya mambo yanahitajika kuongezwa nguvu. Mimi ningetoa mawazo yangu kwanza nianzie na Mfuko wa Jimbo. Mfuko wa Jimbo kwa sasa hivi naweza kuzungumza kwamba ni Mfuko wa pekee ambao unabeba Mfuko wa Mbunge na Mwakilishi katika maeneo mengine. Kwa sababu wengine wabunge wetu hawafanyi vile inavyotakiwa katika Mfuko huu. Sasa kwa kweli Wawakilishi wamepata mzigo mkubwa sana katika majimbo yao baadhi ya Wawakilishi wale ambao wako peke yao.

Lakini ukiachia hivyo, kutokana na muundo unaojijengea sasa hivi hapa ni kwamba Mwakilishi ana jukumu kubwa sana la kutetea jimbo kuliko Mbunge. Sasa mimi ningeomba wanaohusika na Mfuko wa Jimbo kwamba muda umefika wa kuuongezea Mfuko wa jimbo ili nao uweze kujivuta. Kwa sababu Mfuko uliopo sasa hivi ni wa bajeti ya mwaka 2015, lakini sasa tumeshafika mwaka 2017 na mambo yameongezeka sana. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri akautizama Mfuko huu ukaongezeka kwa sababu kwanza ni Mfuko ambao kwa muda huu unakwenda kimahesabu na unakwenda kwenye jamii moja kwa moja. Kwa hivyo, ningemuomba waziri kama itawezekena basi afanye hilo ili tuweze kuwasaidia wananchi moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niweze kusema kwamba katika mazingira yetu pamoja na jitihada za serikali katika kuweka vitu vyake sawa katika mambo tofauti, lakini bado *register book* katika kila wizara hakuna *register* maalumu ya vitu vinavyoingia na vinavyotoka kwa ufasaha. Kwa hivyo, ningeomba sana Waziri wa Fedha au wanaohusika baada ya *register book* katika mambo mengi au katika kompyuta ambazo zinaweka *ledger book* ya vitu ambavyo vinaingia, vilivyokufa, vilivyouzwa, lakini pia kukawa na buku la kitaifa au la serikali kuu ambapo kama kutakuwa na utatanishi basi iweze kwenda moja kwa moja kwenye lile buku kubwa kwenda kuangalia yale matukio ambayo wizara imefanya.

Sasa hivi unaweza ukenda katika mawizara tunapata baadhi ya malalamiko kwamba kuna baadhi ya viongozi wanauza vitu bila hata ya kuwa na ushirikiano na serikali, lakini pia kuna vitu ambavyo vinakuwa havieleewki. Kwa hivyo, ningeomba pamoja na wizara, baadhi ya wizara nyengine bado hazijajiweka sawa katika mazingira haya. Hivyo, ningeomba kuwe na buku kubwa ambalo litaweza kumiliki wizara zote katika vitu vyote vinavyokwenda katika mawizara ili ikajulikana takwimu sahihi ya vitu vya serikali ili visiende ovyo. Naomba katika suala hilo likaweza kutizamwa vizuri sana. Kwa sababu hapa tunapoteza pesa nyingi za serikali kutokana na mambo yanavyokwenda na hata kama mtu atakamatwa kuuza vitu vile havina ushahidi na mtu yule tunapoteza ushahidi inakuwa hakuna kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mheshimiwa sehemu nyingi tumekwenda katika kuangalia matukio unapokwenda tayari kama ni mhusika ambaye anakwenda kukaguliwa pengine yuko nyuma kwa muda wa miaka miwili, tofauti yao ya kwenda kukaguliwa. Miaka miwili inawezekana mtu anayekwenda kukaguliwa keshakufa na hasara aliyoitia serikali ni kubwa sana, lakini wengine wameshasafiri kwa sababu yeye anayefanya kitendo kile anajua kwamba amefanya kitendo fulani. Kwa hivyo, anaweza akaichupa serikali akaiwahi kuikimbia bila ya watu kushitukia.

Sasa ningeomba hawa watu wa udhibiti na ukaguzi wa hesabu za serikali waende sambamba pamoja na mahesabu ya mwaka ili kuweza kujua serikali iko wapi. Kwa hivyo, cha msingi hiki tungekiangalia maana yake inaonekana imekuwa ni ukaguzi labda wa kupiga ripoti, lakini hatua nyengine haziendelei kwa sababu tayari tumeshachelewa muda mrefu sana. Kwa hivyo, inakuwa ni suala ambalo kidogo linakuwa na matatizo. Sasa ningemuomba hilo Mhe. Waziri kama kuna upungufu wa wafanyakazi basi ningeomba alifuatilie kwa sababu tunakosa mapato na mambo mengine mengi.

Vile vile niende na suala la manunuzi. Mhe. Waziri matatizo mengi yanatukumba sana sasa kwenye masuala ya manunuzi. Biashara ya manunuzi imekuwa kubwa mtu ananunua anavyojitakia mwenyewe bila ya kupata utaratibu, lakini pia ananunua vitu vilivyokuwa havina ubora matokeo yake tunapata matatizo sana tunanunua kitu cha siku tatu na pia manunuzi yenyewe yanakuwa hayana *guarantee*. Kwa hivyo, hatujui wa kumkamata nani tunakwenda tu na badala yake tunakuwa tumepoteza pesa za serikali zisizokuwa hazikutenda haki. Hivyo, ningeomba hili suala la manunuzi na sheria naona kama tumeshazipitisha basi likafanyiwa utaratibu wa haraka, ili tukaweza kwenda na maelekezo ambayo yanaweza yakatusaidia sana ili kuepuka baadhi ya watu ambao wananunua vitu ambavyo havina viwango.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwenye Mfuko wa Barabara. Mheshimiwa kwa kweli hapa serikali inapoteza pesa nyingi sana, hapa kuna mambo ambayo serikali inapoteza maana yake tuangalie ukweli barabara ninavyojua katika kufahamu ni pesa nyingi sana, lakini kuna vitu ambavyo vinatokezea ikiwemo pamoja na barabara kukosa mitaro. Barabara inajengwa inakunywa maji baada ya kipindi kidogo inaanza kufumuka, hata miaka mitano haifiki tunairudia barabara ile kwamba si barabara tena, angalia pesa ambayo imeshatumika kwa barabara ile.

Pia kuna barabara ambazo hazina viwango zinakuja kukaguliwa baada ya mwaka mmoja mkandarasi keshaondoka. Mheshimiwa hapa tunapoteza pesa nyingi sana lakini pia kuna mvutano wa barabara baina ya watu ambao sijui *interest* zao zinakuwaje, barabara inaweza kutaka kujengwa mwaka huu ikawa imekosana labda kwa pesa ndogo sana, lakini mkandarasi akaweza kugeuzwa baada ya miaka miwili ikaletwa tena *tender* nyengine ambayo imeshapita mara mbili ile pesa ambayo ilitaka kujengwa kwa mara ya kwanza. Sasa Mheshimiwa ningemuomba Mhe. Waziri akaziangalia hizi pesa ambazo zinapotea zisizokuwa na udhibiti mzuri, akaweza kuzidhibiti ili kuweza kuangalia hali halisi ambazo zinakwenda.

Vile vile nizungumzie na kitu kimoja ambacho tunakuwa tunachomekeana, utakuta baadhi ya mitaro ya maji machafu Wizara ya Maji inajiingiza humo humo kwenda kuweka *pump* za maji safi, matokeo yake *pump* ile kama itakuwa na *leakage* inakunywa maji machafu inashindwa kujulikana kama maji machafu yale yanatokea wapi, lakini na hasara nyengine kama ya kipindupindu inaweza ikatokea. Sasa ningemuomba waziri masuala kama haya ambayo baadae yanamfika yeye maana yake anahitajika kutoa pesa ya serikali akaweza kuangalia kwamba watu hawa wasijiingize katika nafasi kama hizo. Kwa sababu kama tulivyosema maji safi na salama lakini kuna maeneo ambayo kuna mabomba ya maji machafu wanapitisha mule mule mipira ile ambayo naweza kuzungumza pale Chake Chake kwenye Soko la Tibirinzi ndio yamepita humo humo na *pump* zenyewe wakati wa kutoka maji zinavuja, hivyo inaonesha na wakati wa mvua yanapita. Kwa hivyo, ningeonesha kwamba waweze kubagua maji ni hatari sana yanaweza

yakatuletea matatizo kama ya Mhe. Waziri wa Afya hapa habari ya kipindupindu ambapo maji ni machafu. Kwa hivyo, ningeomba litoke hilo.

Mhe. Mwenyekiti, pia ningesema kabisa kwenye miradi ya maendeleo. Miradi ya maendeleo mara nyingi tunataka tuchangie na serikali, tukichangia na serikali unaweza ukakuta kwamba tayari mradi umeshaletewa pesa lakini bado serikali haijatenga pesa. Kwa hivyo, inakuwa kidogo miradi inachelewa na kuweza kuwapa nafasi watu ambao wanakuwa hawana ukweli na zile *tender* na wakaweza kuchelewa halafu wakatupa hasara. Kwa hivyo, ningeomba katika jumla ya mambo kama haya serikali ikajipanga vizuri katika kuweka hizi sekta za maendeleo ili kosa lisitokee kwa upande wa serikali na sisi tukapiga maendeleo haraka iwezekanavyo.

Pia katika mawizara ningeomba sana Wizara ya Fedha katika bajeti tunazozipitisha tunakuwa na malalamiko mengi ya wizara, sijui sasa wengine wanatumia mwanya huo wakisema serikali bado haijatimiza viwango vya fedha, inakuwa ni malalamiko ambayo kwa kweli wengine watendaji waliokuwa si waaminifu wanatumia *loophole* hiyo ya kuongeza maelekezo ya kusema bwana pesa haijatimia, pesa haikufikia, sasa anapata sababu ya kusema na baadhi ya mambo mengine miradi inadidimia inakuwa haifikii kiwango. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningemuomba katika hatua ambazo tunamsaidia kwa kila hali ili tuweze kuendelea kupiga hatua.

Pamoja na hayo, mimi nataka nichangie kidogo kuhusu habari ya mishahara hewa, pamoja na waziri kuzungumzia bado kwamba hakuna mishahara hewa lakini bado kuna pesa ambazo zinapotea na ambazo ziko katika risiti, bado waziri ajitahidi sana kufanya kila mbinu za kuzuwia kwa sababu mianya ya kupotea pesa bado ipo na watu wanaifanyia kazi. Sasa ningemuomba waziri ajitahidi pamoja na kwamba kunahitajika mitambo na mambo mengine, lakini afanye jitihada zake ili pesa zisipotee kwa muda huo.

Mimi ningeomba na kitu kimoja, katika sehemu hizi za kukusanyia pesa kama tuseme *People's Bank* ningeomba waziri pamoja na kwamba benki hii inajikamata mwenyewe kama benki, lakini pesa zinazokwenda kulipwa pale kwa mfumo wa kisasa ni pesa za serikali. Mara nyingi tumeweza kuji-*commit* kwamba pesa ya serikali yote tunaipeleka benki na benki tuliyoidhinisha ni benki ya *PBZ.* Tunataka kwa kila siku ambayo tuko pale waziri anaijua kama pesa iliyoingia leo ni shilingi ngapi, lakini unakuta misongo ya pesa ambapo pesa zile serikali inazihitaji na pesa zile zinarudi majumbani kwa sababu tu ya *queue* au ya mambo mengine ambayo yanasababisha kutokukamilika kwa pesa zile. Pia tuangalie kwamba wale watu wenyewe ambao wanahitajika kupeleka pesa, nao wanataka wafanye kazi kwa siku ile siku nzima inapotea kwenye kulipa pesa. Ningemuomba sana Mhe. Waziri akakaa na *People's Bank* akahakikisha pesa inalipwa kirahisi ili tuweze kuikusanya vile inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba tena Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na serikali nyengine hazina maduka ni serikali ambazo zinategemea mapato yake kutokana na kodi, bado tunahitaji kwa kila mwananchi kulipa kodi. Ni wajibu wetu kuisaidia serikali, kumsaidia waziri katika kuhakikisha kwamba kodi inalipwa ili kila mmoja aweze kufaidika na pesa ile tuache malalamiko zaidi katika masuala ya kuisemea serikali kipesa, lakini na sisi tunashindwa kuhamasisha katika utekelezaji wa kodi zetu. Ningeomba sana, miradi ambayo inahakikishwa ina maendeleo katika jamii yetu basi ifanyiwe kazi na kulipa na wale wafanyabiashara basi wawe waaminifu katika biashara zao ili tuendane na kodi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo, lakini kitu ambacho kwa kweli kinasababisha mambo mengi ambayo yanapata upotevu wa malipo ni udhibiti wa vifaa maalum hivyo nilivyovizungumza lakini katika mashirika mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, biashara zetu tunaziona za serikali zinazotumika na makampuni yetu pamoja na viwanda. Kiwanda kila siku kinapokuwa cha serikali kinakuwa ni kiwanda cha hasara na kiwanda kinachokufa, lakini matokeo yake Mkurugenzi anaondoka pale anapewa kiwanda chengine kwenda kukimaliza. Ningeomba sana Mhe. Waziri akawa mkali katika kuliangalia katika watendaji wake, kama mtendaji amekuwa ni mtu ambaye amepelekwa katika maeneo hakuweza kulichangia taifa ameweza kudidimiza basi aweze na yeye kwenda kutafuta jembe akalime, sio abadilishiwe eneo kwa ajili ya kwamba ana *degree* au kitu gani. Wenye *degree* ni wengi sana lakini tunahitaji maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nimeshakuona na mimi nakushukuru sana na namshukuru sana waziri, namshukuru Rais wa Zanzibar ahsanteni sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na baadae Mhe. Said Soud Said.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Bismilahi Rahmani Rahiim. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana mimi kwa leo mchango wangu nimeuondosha kwa sababu siko sawa, lakini nitaomba Mhe. Said Soud Said aendelee.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza natanguliza kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) kwa kutujaalia kufika leo hii salama usalimini. Vile vile nachukua nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Kwa sababu ripoti hii ambayo imewasilishwa hapa ina maagizo yaliyomo ndani ya Ilani na kwa sababu utekelezaji wake ulikuwa unaangaliwa sana na kamati za Baraza la Wawakilishi basi pia nachukua nafasi hii kuzipongeza kamati hizo kutokana na kazi kubwa wanayoifanya ya kusaidia serikali ifikie malengo yake ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu Wawakilishi wote na watendani wa serikali tuna ulazima wa kuhakikisha tunaisimamia na kuitekeleza Ilani ya Uchaguzi. Kwa nini tufanye hivyo, kwa sababu ndio chama kilichoshinda uchaguzi na kumuweka Rais madarakani na Rais naye akachukua nafasi ya kuunda serikali kwa misingi ya kuiendeleza demokrasia ya Zanzibar na Tanzania. Kwa mantiki hiyo, kamati hii ambayo imepita na kuona mambo yote yaliyokuwa yamesita na yale yanayoendelea naipongeza sana. Nasema hivi kwa sababu tutapata nafasi kama serikali kuhakikisha kwamba yale yaliyosita lazima yatekelezwe ili Ilani ya Uchaguzi ipate nafasi yake ya kujitangaza tena mwaka 2020. Kwa vile zile kasoro ambazo zilionekana mimi

nahakikisha kwamba kasoro hizo tutazichukua na tutazizungumza ili kwa maana ya kuzikwamua ili serikali ionekane inatenda vile ilivyoagizwa na Ilani ya Uchaguzi.

Waheshimiwa Wawakilishi bado tuna nafasi ya kuona watendaji wa serikali wanaokwamisha kwa makusudi hatua za utendaji wa kazi za serikali maofisini kuonana na mawaziri husika kwa ajili ya kutoa ripoti zao, msisubiri mpaka mtu akaharibu mia kwa mia ndio baadae mkaanza kuzungumza.

Nazungumza hivi kwa maana hatuwezi tukajengewa Zanzibar na mtu mwengine yeyote, Zanzibar tutajenga wenyewe Wazanzibari na kuijenga Zanzibar ni kuhakikisha kwamba tunaondosha rushwa ya muhali kwamba labda mimi nikizungumza fulani hafai nitaonekana mbaya hamna, zungumza wazi wazi kwamba fulani amefanya kitu fulani na kwa maana gani amefanyaka kwa sababu amevunja sheria na katiba ya nchi. (*Makofi*).

Kwa misingi hiyo tutaisaidia serikali yetu kupiga hatua na tutaweza kufika tena 2020 na kukifanya Chama cha Mapinduzi kishinde tena uchaguzi ni sisi ndio tunatakiwa kusimamia maendeleo kwenye majimbo. Ule mfuko wa majimbo unaotolea usiishie kwenye mifuko ya nyuma. Mfuko wa majimbo unaotolewa ukafanya kazi kwenye Majimbo, usiishie hapa kwenye mifuko ya nyuma halafu mkaja hapa mkasema hili halijafanywa. Mfuko wa Jimbo ukafanyakazi ya Jimbo. Halafu sasa na nyinyi *PAC* ikifika mtoe ripoti *PAC* inakwama kupata ripoti ya mifuko ya jimbo. Kwa nini inashindwa kupata ripoti ya mifuko ya Jimbo *PAC* hii hii ya humu humu ndani. Naseme *PAC* mchukuwe hatu Mwakilishi kama hana ripoti ya Jimbo mtupe taarifa sisi Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais ipo, Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ipo sio mchukuwe pesa na kutia mifuko ya nyuma. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Wawakilishi ni watendaji wazuri na nataka nirudie tena kwa kusema kwamba Rais wa Zanzibar alipomchagua Waziri wa Fedha basi hakukosea. Kwa sababu fedha imepatikana na fedha ndio inayotengeneza nchi yetu. Mhe. Rais wa Zanzibar anatembea kifua mbele kwa sababu ya uchumi ulionyanyuka hapa Zanzibar. Rais wa Zanzibar anawajali wazee anawajali mpaka watu waliokwisha kufa. Karibuni hivi Rais wa Zanzibar alifanya harambee zaidi ya milioni ya mia nane kujenga nyumba ya Siti bint Sadi pamoja na wenziwe maana yake ni kuwajali wale wameshakufa. Lakini Rais anawajali kwa nini waliitangaza Zanzibar katika hatua za maisha yao. (*Makofi*)

Rais huyo huyo anawajali mpaka watu wanaofikia umri wa miaka 70. Sisi karibuni wengine tutaorodheshwa katika miaka 70 tuchukuwe elfu ishirini ishirini. Kwa maana gani tayari Rais anawajali watu wazima, Rais anawajali wafanyakazi anawaongezea mishahara kila siku, Rais anawajali Wazanzibari anawateua sehemu mbali mbali kwa ajili ya kufanya kazi za kujenga nchi hii. Sasa hivyo tunataka nini? na uchumi umenyanyuka kiasi cha kwamba sasa mpaka Serikali ya Oman inakuja kutembelea hapa, Serikali ya Oman inakuja kutembelea hapa kwa sababu ya uchumi tu. Hapo tulipokuwa masikini walikuwa hawaji hawa lakini sasa wanakuja wenzetu *Alhamdulillah* na tunawaambia karibuni Zanzibar na Zanzibar itaendelezwa na Wazanzibari wenyewe. (*Makofi*).

Waheshimiwa Wawakilishi ni nafasi yetu kujivuna katika mazingira ya kujenga Zanzibar yetu katka mazingira ya kusimamia Ilani ya Uchaguzi katika mazingira ya kulinda Mapinduzi. Bila ya

Mapinduzi ya mwaka 1964 fursa hii wengine tusingepata. Kwa vile, ukikichukia Chama cha Mapinduzi maana yake unachukia Mapinduzi. Kwa hiyo, "Mapinduzi Daima" huo ndio msimamo wetu sisi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Ahsante sana naunga mkono ripoti hii. (*Makofi*)
Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Said Soud Said. Sasa namwita Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kufafanua machache sana kwa muda usiozidi hata dakika 3 au 4 juu ya hoja iliyopo katika ukurasa hoja ya mengine ambayo Kamati inashauri Wizara ya Elimu kulipa madeni ya malimbikizo ya walimu. Nimeona nichukuwe fursa hii kueleza zile hatua ambazo mpaka sasa wizara imeshachukuwa juu ya suala hili ili Waheshimiwa Wawakilishi waelewe lakini pia na wananchi waelewe kwamba serikali kupitia Wizara ya Elimu kwa kweli haifurahishwi na madeni ya namna hii na ndio maana tumechukuwa hatua kadhaa.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kwa upande wa malipikizo ya likizo nataka kutoa ufafanuzi zaidi. tumelipa jumla ya walimu elfu mbili na mia mbili waliokuwa wakidai mwaka 2013/2014 sawa na jumla ya shilingi milioni mia mbili na ishirini. Lakini pia tumewalipa walimu wengine katika mwaka huo huo na kwa upande wa walimu Pemba katika mwaka 2014 tumewalipa walimu wote mia tisa na tisini na tatu sawa na jumla ya shilingi milioni tisini na tisa na laki tatu.

Aidha kuna wafanyakazi mia moja na ishirini na moja kwa mwaka 2015 tayari wameshalipwa malimbikizo yao sawa na milioni kumi na mbili na laki moja. Wamebakia wafanyakazi mia saba na tatu wa mwaka 2015 na jumla ya sabini milioni wanadai watu hao. Kwa mwaka 2016 wafanyakazi wanaodai huduma hiyo ya kilizo ni mia nane na arubaini kwa jumla tukichanyanyisha mwaka 2015 na 2016 tunadaiwa milioni mia moja hamsini na nane laki tatu. Hili lilikuwa ni deni kubwa kama mtakumbuka ilikuwa kwenye bilioni huko tumeweza kulipunguza limeweza kubakia kama hivi.

Kuhusu malimbikizo mengine Mhe. Mwenyekiti ya mishahara kwa upande wa Unguja kwa mfano mshahara kundi maalum cheti wenye uzoefu wa miaka 30 kazini tumelipa karibu walimu mia nne na ishirini na tatu sawa na milioni mia tano sabini na sita lakini tatu thamanini na tatu mia nne na thalathini. Kwa hivyo, wamebakia walimu mia tatu na arubaini na nne. Kundi la waliorudi masomoni hili bado hatuajalipa tunadaiwa jumla ya fedha mia nne na hamsini na tatu milioni mia tano sitini na nne mia nane sitini na nane.

Kwa Pemba kundi maalum cheti wenye uzoefu wa miaka 30 kazini tumelipa jumla ya walimu mia moja na thalathini. Ninachosema kwamba juhudi zinaendelea kuchukuliwa na kwa kweli deni hili halitufurahishi na hakuna mwalimu ambaye atakoseshwa haki yake niwaeleze tu kwamba tupo makini kulishughulikia suala hili. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aweze kujibu hoja zilizo mbele yetu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima, afya njema. Lakini vile vile kutuwezesha kufanya shughuli zetu za Baraza kwa umakini na ufanisi chini ya uongozi wake.

La pili nichukuwe fursa hii kumshukuru sana sana Mhe. Rais wetu Dr. Ali Mohd Shein nirudie kumshukuru kwa miongozo anayotupa maelekezo anayotupa na kama ilivyoelezwa hapa na Wajumbe kwamba hali tuliyonayo ya kuimarika kwa uchumi wetu inatokana na miongozo yake. Kwa hiyo, sote tumshukuru sana na kumpongeza kwa sababu kweli uchumi wetu umeimarika na jana hapa nilisema kwamba kasi ya ukuaji wa uchumi imekuwa ikiongezeka kwa asilimi 6.8. Lakini tunatarajia katika mwaka huu wa fedha tutafikia wastani wa asilimia 7.1 mpaka asilimia 7.2. Hiyo yote inatokana na juhudi na maelekezo ya Mhe. Rais Dr Ali Mohd Shein. (*Makofi*)

Lakini pia jana nililisema mapato yetu pia yanaongezeka na yameongezeka kwa ziadi ya 100%. Lakini vile vile *FBI* zetu zimeongezeka, mfumko wa bei umedhibitiwa. Lakini pia Mhe. Rais aliongeza kima cha chini cha mishahara kutoka laki moja hamsini elfu hadi laki tatu na hadi leo serikali hii inaongozwa na Mhe. Dr. Ali Mohd Shein tunaweza kuendelea kulipa mishahara bila ya kuchelewa. (*Makofi*)

Lakini pencheni za wastaafu nazo zimeongezwa kwa zaidi ya 100% pencheni za wazee nazo zinaendelea kulipwa kama ilivyotakiwa. Lakini pia taasisi zote zinapata mgao wake kwa mujibu wa *cash flow* zao. Mafanikio haya yote yanatokana na uongozi wa Mhe. Rais Dr Ali Mohd Shein kama alivyosema Mhe. Said Soud Said *Member* wa Baraza la Mapinduzi ni hakika kabisa. (*Makofi*)

Baada ya shukurani hizo na pongezi hizo pia nimshukuru sana Mkuu wa shughuli za serikali ndani ya Baraza Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Idd kwa kutuongoza vyema katika vikao hivi tunavyoendelea navyo katika Baraza hili. Nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kwa jinsi ulivyosimamia na kuendesha kikao chetu na mijadala ya leo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru Wajumbe wote waliopata fursa ya kuchangia taarifa yetu ya *PAC* ambayo imejumuisha wizara na taasisi mbali mbali za serikali. Niwashukuru wale waliopata nafasi ya kuchangia moja kwa moja akiwemo Mhe. Rashid Makame Shamsi, Mwakilishi Makini wa Jimbo la Magomeni, lakini aliwasilisha kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* lakini pia nae yeye alipata nafasi ya kutoa maoni yake. Nimshukuru sana

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
Mhe. Suleiman Sarahani Said
Mhe. Said Soud Said (*Member* wa Baraza la Mapinduzi)

Lakini pia kwa upande wa waliochangia kwa maandishi nimshukuru sana

Mhe. Simai Mohamed Said
Mhe. Shehe Hamad Mattar (wewe Mhe. Mwenyekiti) pia umeleta mchako kwa maandishi.

Kwa ujumla maoni yote niseme tumeyachukuwa tumeyapokea na kwa niaba ya wizara zote na taasisi zote zilizoguswa basi maoni na fikra za Waheshimiwa Wajumbe mlizozitoa hapa basi sisi tunazichukuwa na tutakwenda kuzifanyia kazi kikamilifu.

Labda niseme maeneo machache yaliyogusiwa moja liligusiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi linalohusiana na masuala ya *IFMS* na yeye alitaka kujua ni jinsi gani tunaweza tukalikamilisha ili kuondosha lile tatizo la ***Dummy.*** Na hili nimueleze tu kwamba ule mtandao wetu mfumo wetu unafanyiwa kazi mfumo wa *IFMS* na wataalamu wapo ili tuhakikishe kwamba *IFMS* inaweza kutumia kwa zaidi ya *current* moja kwa maana ya shilingi basi pia na malipo yanayotumika kwa fedha za kigeni yaweze pia kutumika kwa kutumia mtandao huo wa *IFMS.*

Lakini vile vile suala hili la kuchelewa kwa ripoti za ukaguzi kwamba ziko nyuma ambalo pia lilizungumzwa na Mhe. Suleiman Sarahani Said. Nalo hili niseme tunalichukuwa ni suala muhimu sana linafanyiwa kazi. Huko nyuma taarifa hizi zilikuwa zikitolewa zaidi ya hivi lakini kuna *improvement* kubwa, kuna marekebisho makubwa yamefanyika na jitihada zaidi zitachukuliwa ili kuhakikisha tunakwenda sambamba katika ukaguzi na kazi za *PAC*. (*Makofi*)

Lakini vile vile Mhe. Rashid Makame Shamsi alizungumzia suala la Mfuko wa Jimbo na hapa niseme kwamba Mfuko wa Jimbo jamani upo kwa mujibu wa sheria na ile sheria sisi Wawakilishi kama wenyeviti wa Kamati za Mfuko wa Jimbo tunahitajika sote tuzielewe, tuzifahamu, ndani yake kuna haja ya kushirikisha jamii katika kuibua miradi yenyewe maana yake sio miradi tunayoiibua sisi kwa fikra zetu. Lakini lazima wananchi wenyewe washirikishwe kikamilifu katika kuibua miradi hiyo. Lakini vile vile katika kusimamia matumizi ya fedha zinazotolewa.

Pia Waheshimiwa nadhani suala la fedha ambazo tunazungumzia za shilingi milioni ishirini kwamba zinafaa kurekebishwa hili lilizungumzwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said. Tulianza mbali huko nyuma ilikuwa chini ya Wizara ya Fedha zilikuwa zinatoka shilingi milioni tano kwa miradi midogo midogo. Lakini baadae serikali ikaongeza ikafikia milioni kumi, ikaongezwa tena ikawa milioni kumi na tano na sasa milioni ishirini. Mimi naamini kwamba serikali hii inayoongozwa na Mhe. Dr. Ali Mohd Shein hali ya fedha ikiimarika kuna mambo mawili.

- Hali ya fedha iimarike, kwa maana uwezo

- Tija ipatikane kwenye hiyo miradi inayosimamiwa kupitia kupita mfuko wa Jimbo. (*Makofi*)

Kwa hivyo, sisi tuna haja kwanza ya kuhakikisha tunaisimamia miradi ambayo tunaiibua katika majimbo, kwa sababu hiyo pia ni kusaidia serikali katika kuteleza miradi inayowagusa wananchi. Sasa kama kweli miradi itatekelezwa kwa uadilifu na ionekane kabisa miradi hiyo kwamba inaleta tija na inapunguza mzigo kwa serikali na uwezo wa serikali ukiimarika mimi sina shaka uwezekano wa kuongeza fedha hizo utakuwepo. Kwa sababu mwanzo ni jukumu letu la kuhakikisha tunasimamia miradi kwa ukamilifu, kwa uadilifu na hakuna fedha zinazopotea. Lakini vile vile tuhakikishe kwamba kuwasilisha *returns* zetu kwa mapema na *returns* za uhakika ambazo hazitokuwa na mashaka. Sasa hayo yakifanyika nadhani serikali ya Mhe. Dr. Ali Mohd Shein na uwezo wetu ukiimarika basi hakuna shaka suala hili litazingatiwa. (*Makofi*).

Mhe. Simai Mohamed Said yeye alizungumzia suala la ununuzi. Sheria ya ununuzi na kusema kwamba bado sheria hii manunuzi yanayofanywa na serikali gharama inakuwa kubwa na wakati mwengine inasababisha hasara kwa serikali.

Kwanza nikubaliane nae kwamba matumizi makubwa yanayofanywa na serikali asilimia kubwa kwa zaidi ya 70% ya fedha za serikali zinatumika katika masuala ya manunuzi ama ya huduma ama ya bidhaa mbali mbali. Sasa kuna haja kwanza ya watendaji kuelewa sheria hii mpya ambayo tumeipitisha sheria ya mwaka 2016 na kwa namna hiyo taaluma itatolewa zaidi.

Lakini vile vile niseme kama nilivyosema kama nilivyosema jana kwamba serikali Mhe. Rais tayari ameunda kamisheni ya kusimamia masuala ya ununuzi ya uondoshaji wa mali za serikali na tayari hivi sasa kuna Kamishina kwa ajili ya kazi hiyo. Lakini kupitia sheria ile ziko njia mbali mbali ambazo zinatumika au mtu anaweza kuzitumia kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa ama huduma za serikali.

Ya laiti kama tutaifata sheria kama ilivyo, mimi naamini kwamba bei hazitokuwa kubwa namna hii. Kwa sababu tunapozungumzia tenda ya ushindani *(competitive bid)* maana yake kwamba hawa wazabuni wawe wanatoa bei zao bila ya kuweko na vishawishi fulani fulani na kama kutakuweko na wazabuni watatu, wanne ambao watakuwa wanafanyakazi ya kutoa bei zao kiushindani basi unaweza ukapata wastani wa bei halisi wa bidhaa au huduma hiyo. Lakini kwa bahati mbaya sana katika baadhi ya mambo hutokea ujanja ujanja wa namna hiyo na ndio maana tunaweza tukakuta mfumko wa bei inakuwa bei kubwa sana tunapokwenda na tenda hizi za serikali.(*Makofi*).

Sasa kazi tunayoifanya ni kuhakikisha tunadhibiti vitendo vya namna hii kuwepo na uwazi, lakini vile vile na wajibikaji na kutoa taaluma ili tuhakikishe tenda zote, zabuni zote zinazotolewa zinatolewa bila ya kuwepo ghilba za aina yoyote ile na tungewaomba wazabuni wakawa wakweli. Lakini na watendaji wetu nao pia wakafanyakazi kwa kuzingatia maadili ya taaluma walizonazo na kazi zao.

Pia Mhe. Simai Mohamed Said alizungumzia suala la serikali labda ifikirie kuanzisha na vituo vyake vya mafuta vitakavyotumika kwa ajili ya kutia mafuta vyombo vya serikali. Hili niliseme huko nyuma ilikuwa likifanyika namna hiyo utaratibu ulikuwa huo. Lakini kulikuweko na hasara kubwa sana na mpaka serikali ikaamua kuondokana na kuwa na vituo vyake vya mafuta kwa maana vya petrol na kadhalika. Lakini ni wazo zuri, serikali ikiona kuna haja ya kurudi tena huko na kwamba mazingira ya sasa yanakubali kuwa na vituo hivyo, basi serikali italizingatia na ningemuomba tu Mhe. Simai Mohamed Said asiwe na wasi wasi na hilo, kama haja ipo na tunahisi tunahisi tutakuwa na faida zaidi ya kwenda huko, basi serikali italifanyia kazi wazo lake hilo.

Vile vile kuna suala zima jengine la Mhe. Suleiman Sarahan ambalo lilizungumzia masuala ya *asset register* na alitaka kwamba mbali ya kuwa na *soft copy,* lakini pia tuwe na hard copy na hili ni suala zuri na hivi sasa ndivyo linavyofanyiwa kazi. Wizara ya Fedha na Mipango imetayarisha muongozo na imetoa katika kila wizara na idara za serikali katika kuweka kumbukumbu hizi za *asset* za wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kupitia Idara ya Mitaji ya Umma tayari imeshazisaidia wizara tano katika kuanzisha daftari la mali za wizara hizo au taasisi za serikali. Hivi sasa niseme kwamba mtaalamu yupo chini ya ufadhili wa mradi wa usimamizi wa fedha za umma, *Applic Finance Management Reform Programme,* na tunakusudia kuhakikisha kwamba wizara zote zitapata msaada huu wa kuwa na asset register ndani ya mwaka wa fedha huu wa 2017/2018.

Suala jengine ni la Mfuko wa Barabara na miradi ya maendeleo. Nadhani hili Mhe. Suleiman nikuhakikishie kuwa tumekusikia, tumelichukua na tutayazingatia maoni yako na wizara zinazohusika nazo zimesikia, ikiwemo Mfuko wa Barabara ambao uko chini ya Wizara yetu ya Fedha na Mipango, lakini pia suala la kupitisha mabomba ya maji katika mitaro ya maji machafu. Nalo hili limesikika na wizara inayohusika na litafanyiwa kazi, na kuhakikisha kwamba tunasimamia kikamilifu fedha zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hilo masuala ya udhibiti wa matumizi ya fedha za serikali, ni suala ambalo Dk. Ali Mohammed Shein ndani ya mwaka wa fedha 2016/2017 alilisimamia kwa nguvu zote. Kutokana na kazi hiyo nzuri ya Mhe. Rais, hivi sasa matumizi holela ya fedha za serikali yamepungua sana. Fedha nyingi sana zinaelekezwa kwenye zile kazi za msingi au *function* za wizara na hata ukitizama kwamba fedha zilizokuwa zikitizama katika masuala ya safari nazo zimepungua sana kwa sababu ya udhibiti, sio suala la kuondosha lakini ni udhbiti wa kuhakikisha ni zile safari ambazo zinatija watu ndio wanazokwenda siku zote. *(Makofi)*

Vile vile kumetokea na udhibiti mzuri sana wa mikutano ambayo mingi yao ilikuwa ikifanywa katika mahoteli pasipokuwa na ulazima. Hivi sasa mikutano mingi na semina nyingi zinafanywa ndani ya kumbi zinazomilikiwa na serikali na hizo zimepunguza sana matumizi ya fedha za umma ambapo zilikuwa hazitumiki vile ilivyostahiki. *(Makofi)*

Kwa pamoja na hayo yote nirudie tu kusema Mhe. Mwenyekiti, michango yote ya Waheshimiwa Wajumbe tumeichukua na itafanyiwa kazi kikamilifu. Nawashukuru wajumbe wote kwa kunisikiliza, ahsante sana. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa. Wale wanaounga mkono hoja wanyanyuwe mkono. Wanaokataa hoja hiyo. Wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja imetolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

RIPOTI YA UTEKELEZAJI YA MAMLAKA YA MAJI (ZAWA) KWA MWAKA 2016/2017

1.0 UTANGULIZI

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Maji ZAWA kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji Zanzibar ni Taasisi iliyoanzishwa kisheria mwezi Agosti mwaka 2006, kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Maji Namba 4 ya Mwaka 2006. Sheria hii imeipa uwezo Mamlaka ya Maji kusimamia shughuli za uzalishaji maji, usambazaji maji, uhifadhi na uendelezaji wa rasimali maji.

Kimuhtasari, ripoti hii inaelezea utekelezaji halisi wa kazi za maendeleo na kazi za kawaida zilizopangwa kutekelezwakwa kipindi cha mwaka 2016/2017, mafanikio, changamoto pamoja na mikakati ya kutatua changamoto hizo.

Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika kipindi hichoni Programu tatu na miradi minne ya maendeleo kama ifuatavyo:

1.1 Kazi za Maendeleo

Programu

- Programu ya Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini
- Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini
- Programu ya Kulinda na kuhifadhi vianzio vya maji

Miradi

- Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na Kuijengea Uwezo Mamlaka kifedha
- Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)
- Mradi wa uchimbaji wa visima unaofadhiliwa na Serikali ya China
- Mradi wa Uchimbaji Visima unaofadhiliwa na Mtawala wa Ras Al Khaimah

1.2 Kazi za kawaida

- Ukusanyaji wa mapato
- uzibaji wa mivujo/upotevu wa maji (*leakages*)
- Kuvilinda, kuvitunza na kuviwekea uzio vianzio vya maji

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17, imepanga kutumia jumla yaTZS 2.8 bilioni na imeweza kutumia 1.5 bilioni sawa na asilimia 54 ya makadirio kwa kazi za maendeleo, na imepanga kutumia 12.8 bilioni na imeweza kutumia 4.9 bilioni sawa na asilimia 42 ya makadirio kwa kazi za kawaida.

2.0 UTEKELEZAJI

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Mamlaka ya Maji ilitekeleza kazi za maendeleo kupitia miradi na kazi za kawaida kama inavyosomeka katika taarifa hii.

2.1 Kazi za maendeleo

2.1.1 Programu ya Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji Mijini

Katika programu hii kuna miradi miwili ya Maendeleo ambayo ni:-

(i) Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Mkoa wa Mjini Magharibi (*Zanzibar Urban Water and Sanitation Project*) – *ADF* 12:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu wenye lengo la kutatua kero ya ukosefu wa maji safi na salama katika Mkoa wa Mjini Magharibi, hususan maeneo ya Mji Mkongwe na Ng'ambo ya Asili, unaogharamiwa na kutekelezwa kwa pamoja kati ya Benki ya Maendeleo ya Afrika *AfDB* na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwa gharama za jumla za Dola za Kimarekani 23.673 Milioni, ambapo asilimia 90% zinatolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika na asilimia 10 zinatolewa na SMZ. Fedha hizi ni Mkopo kutoka Mfuko wa *African Development Fund* 12, na Mradi una vipengele vikuu vitatu ambavyo ni:-

a. Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji
b. Ujenzi wa Vyoo na Usafi wa Mazingira
c. Kuijenga Uwezo Mamlaka ya Maji

Kazi kuu zilizofanyika hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2017 ni kama ifuatavyo:

a) Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji
Imeundwa na sehemu kuu mbili,

(i) Ukarabati na Uchimbaji wa Visima (Package No. I), kazi ambayo inatekelezwa na Kampuni ya *NSPT* Ltd kwa Gharama ya USD 5,428,418.

Mhe. Mwenyekiti, *NSPT* ni Mkandarasi wa Ukarabati na Uchimbaji wa Visima anaendelea vyema na utekelezaji wa Mkataba, ambapo alitakiwa achimbe jumla ya visima vipya 9, kati ya hivyo visima viwili ni kwa ajili ya uchunguzi na saba ni kwa ajili ya uzalishaji, Visima hivyo tayari vimeshachimbwa katika maeneo ya Bumbwisudi vishafanyiwa majaribio pamoja na kujengewa vibanda vya kuendeshea mashine na ujenzi wa uzio.

Aidha, katika ukarabati wa visima vikongwe, vya Welezo, Kianga na Mwembemchomeke vilivyomo katika mpango kazi tayari vimeshafanyiwa ukarabati na kufanyiwa majaribio (*Pumping test*) jumla ya visima vyote 23 kwa mujibu wa Mkataba. Vile vile uchunguzi wa visima (*Borehole Camera Inspection*) umekamilika kwa 98%. Kazi iliyobakia ni ya ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kuvutia maji (*pumps*) katika visima vyote vya mradi ambapo inatarajiwa kazi hiyo yote kukamilika ifikapo February 2018.

(ii) Ujenzi wa Matangi na Ulazaji wa Mabomba uliyokuwa unatekelezwa na Kampuni ya *SPENCON Services Ltd*, ambayo kwa sasa Mkataba wake umevunjwa. Mkataba mwengine umesainiwa tarehe 5/3/2017 na kampuni ya *Stecol Corporation Ltd* ya China kwa utekelezaji wa kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kufilisika kwa mkandarasi aliyepewa kazi ya Ujenzi wa Matangi na Ulazaji wa Mabomba, Mamlaka imelazimika kumtafuta mkandarasi mwengine baada ya kupata ridhaa kutoka Benki ya Maendeleo ya Africa na Kwa sasa kazi hiyo imekabidhiwa kwa kampuni ya *Stecol Corporation Ltd* ya China, kwa utekelezaji wa kazi hiyo ambayo ni Ujenzi

wa Matangi matatu ya juu (*Elevated Tanks*) yatakayokuwa na ujazo wa lita milioni tano (5,000,000L) kwa pamoja, pamoja na matangi mawili yenye ujazo wa lita milioni mbili (2,000,000 Lita) kila moja yatakayojengwa Saateni na tangi moja lenye ujazo wa lita milioni moja (1,000,000Lita) litakalojengwa katika eneo la Mnara wa Mbao na Ulazaji wa Mabomba yenye urefu upatao kilomita 68 makubwa na madogo kutoka visimani hadi matangini na kutoka matangini hadi kwa watumiaji, kazi hii imeanza kwa hatua za awali.

Mhe. Mwenyekiti, kazi zote hizi zinasimamiwa na Mshauri Mwelekezi wa Kampuni ya Don *Consult Ltd* ya Tanzania.

b) Ujenzi wa Vyoo na Usafi wa Mazingira Maskulini

Kazi hii inatekelezwa kwa Mikataba mitatu (3) ambayo ilihusisha skuli 24 za Mkoa wa Mjini Magharibi Msingi na Sekondari, katika kazi hiyo kulikua na ujenzi wa vyoo vipya na vya ukarabati (*Rehabilitation*). Ujenzi wa vyoo katika Skuli hizo umekamilika na tayari Skuli hizo zinafaidika na ujenzi wa Mradi huu chini ya Usimamizi wa Mshauri Muelekezi wa Kampuni ya Howard Humphreys kutoka Dar es Salaam. Skuli zilizofaidika pamoja na Wakandarasi waliotekeleza kazi hizo ni kama ifuatavyo;

i. Lot No. 1 - *SALEM Construction Ltd* ambayo ilijenga na ilikarabati vyoo katika Skuli za Mji Mkongwe ikiwemo Skuli za Hurumzi, Kiponda, Kajificheni, Kiswandui, Mkunazini, Ben Bella na Haile Selassie.

ii. Lot No. 2 – *ZECCON Company Ltd* imejenga na imekarabati vyoo vya Skuli za Makadara, Magogoni, ChumbuniSekondari, Mwembe Makumbi, Nyerere, Lumumba, Mwembeladu.

iii. Lot No. 3 – *Gendermix Enterprises Ltd* iliyojenga na iliyokarabati vyoo vya Skuli za Jang'ombe Msingi, Jang'ombe Sekondari, Kidongo Chekundu Msingi, Kidongo Chekundu Sekondari, Maungani, Migombani, Kisauni, Kiembe samaki na Muungano.

Ulipaji wa fidia

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hiki Mamlaka ya Majiimefanikiwa kulipa fidia katika maeneo yalioathiriwa naMradi wa Maji safi na Usafi wa Mazingira (*AfDB*) uliofadhiliwa na Benki ya maendeleo ambayo hayakuwahi kulipwa hapo awali. Maeneo hayo ni: Kidombo, Kilimani, Chutama, Pwani Mchangani na Matemwe kwa Unguja Kisiwani, Kizimbani, Wara, Mvumoni, Mfikiwa, Wawi, Madunguni, Mgelema, Uweleni na Minazini kwa upande wa Pemba. Aidha, ulipaji wa fidia unaendelea katika maeneo ya Jumbi – Mtwango na Kilimani Unguja, Mialeni, Mdongoni, Kivumoni, Mzimuni, Kalani na Zawadini kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, fedha zilizopangwa kwa mwakawa fedha 2016/2017 kutoka Serikalini ni TZS.billioni moja namillion sitini (1,060,000,000/-)na Fedha zilizopatikana kutoka serikali ni billion moja na million thelathini na moja laki tano na moja, mia saba thamanini na nane elfu (1,031,501,788/-) na zilizopangwa kwa Muhisani ni TZS.billion ishirini million mia saba thelathini na nane, laki mbili na thelathini na moja elfu (20,738,231,000/) na zilizopatikana ni

TZS. Bilioni kumi na nne million mia mbili thalathini na sita laki tano na elfu nne na arubaini na nane elfu (14,236,504,048).

ii) Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji (Awamu ya Pili)

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) Awamu ya Pili (The *Project for Enhancement of Water Supply Management Capacity of Zanzibar Water Authority (ZAWA)* unaogharamiwa na *JICA* kutekelezwa na *ZAWA*. Kazi ya ulazaji wa mabomba imekamilika katika maeneo ya Gulioni na Makadara, na Mradi unaendelea kufanya utambuzi wa wateja wa maji. Vile vile kukusanya taarifa za vianzio (visima) na miundombinu ya maji (matangi pamoja na mtandao wa maji) kwa kutumia *Global Positioning System* na kuzitunza taarifa hizo kwa kutumia program za Kompyuta kama vile *Geographic Information System na AutoCAD.*

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya ufungaji wa mita na ujenzi wa chemba maalum za kuhifadhia mita za watumiaji maji katika eneo la majaribio la Makadara inaendelea ambapo jumla ya Chemba 26 na Valves 36 zimejengwa na tayari zinatumika.

Fedha zilizopangwa kwa mradi huu kutoka Serikalini ni TZS. millioni mia moja nahamsini elfu (150,000,000/-) na Fedha zilizopatikana kutokaSerikali ni million mia moja na ishirini na tano elfu (125,000,000/-) na zilizopangwa kwa Muhisani ni TZS. million mia tano, (500,000,000/) na zilizopatikana ni TZS. million mia tano (500,000,000/-).

2.1.2 Programu ya Usambazaji wa Maji Vijijini

Katika programu hii kuna miradi mitatu ya uchimbaji visima kama ifuatavyo:

(i) Mradi wa uchimbaji visima vya Ras Al- Khaimah

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unaofadhiliwa na Mtawala wa Ras-Al-Khaimah kwa lengo la kuimarisha huduma ya maji safi na salama nchini kwa Unguja na Pemba, Mijini na Vijijini umechimba visima 150 (113 Unguja na 37 Pemba) katika Mikoa yote mitano ya Unguja na Pemba kwa Awamu tatu. Mradi pia umenunua pampu 150 (113 Unguja na 37 Pemba) na umejenga matangi 6 katika maeneo ya Chumbuni, Kianga, Tunguu – Kibele (Mjonga), Michamvi, Upenja na Mtende.

Hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi Juni 2017 Mamlaka ya Maji imefanikiwa kulipa fidia katika maeneo ya Upenja, Bandamaji, Jendele, Kwarara, Kinyasini, Moga, Dole, Ubago na Shakani Unguja kwa ajili ya visima vya Ras Al-Kheimah.

Jumla ya visima 24 (10 Unguja na 14 Pemba) tayari vimeshaendelezwa kwa juhudi za Serikali ya SMZ na vinatoa huduma kikamilifu na visima vyengine 12 (8 Unguja na 4 Pemba) vimo katika hatua mbali mbali za uendelezaji wakekama inavyoonekana katika viambatanisho A na B cha ripoti hii.

Uendelezaji wa visima vilivyobakia, kwa kazi za uvutaji umeme ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu na ulazaji mabomba makubwa na ya kusambazia, umepangwa kutekelezwa hatua kwa hatua kadiri fedha zitakavyo patikana, ukamilishaji wa visima vyote vilivyobakia unatarajiwa kugharimu jumla ya TZS. 8,884,033,000. Kiambatanisho C kinahusika.

Fedha zilizopatikana katika kipindi hiki kwa ajili ya uendelezaji wa visima 24 ni TZS 200,000,000/-

(ii)Mradi wa Uchimbaji Visima na Usambazaji Maji Zanzibar – *China-Aided Zanzibar Well Drilling and Water Supply Project*

Mradi huu unalengo la kuimarisha huduma za maji safi na salama katika maeneo ya Chaani, Donge na Kisongoni kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja na Kiboje na Miwani kwa Mkoa wa Kusini Unguja. Ujenzi wake unafanywa na Kampuni ya *China First Highway Engineering Co. Ltd.* chini ya usimamizi wa Kampuni ya *China Nerin Engineering Co. Ltd.* zote kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

Hadi kufikia Juni 2017 mradi umekamilisha ujenzi wa tangi la Kisongoni, Donge na Chaani,vibanda vya kuendeshea pampu na kutibu majipamoja na kukamilikaulazaji bomba katika maeneo ya Chaani (7.2 Km), Donge (12 Km) na Kisongoni (3.8 Km). Aidha, kazi za uchimbaji visima na ufungaji vifaa zimeanza na zinaendelea vizuri katika eneo la Donge.

Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imefanikiwa kulipa fidia katika maeneo ya ujenzi wa matangi na uchimbaji wa misingi kwa ulazaji wa mabomba katika maeneo ya Chaani Masingini, Gamba na Donge na kazi ya uvutaji wa umeme inaendelea katika eneo la Kisongoni, Donge na Chaani.

- Fedha zilizopangwa kwa mradi huu kutoka Serikalini ni TZS. millioni mia mbili (200,000,000/-) na zilizopatikana ni milioni mia moja tisini na tisa laki moja sitini na nane elfu, (199,168,000/-) na zilizopangwa kwa Muhisani ni TZS. billionsaba million mia tano arubaini na saba laki tisa thamanini elfu (7,547,980,000/) na zimepatikana zote.

2.1.3 Mradi wa Kijamii wa Nishati Mbadala ya Nguvu za Jua *(Community Solar Water Pumping Systems) - Volunteer Universal*

Mradi huu unaogharamiwa na kutekelezwa kwa pamoja kati ya Jumuiya ya *Volunteer Universal*ya Uturuki kwa kushirikiana na *ZAWA*. Lengo kuu la Mradi huu ni kuwapatia huduma ya maji safi na salama wananchi waishio katika maeneo yaliyojitenga (*Remote Areas*) ya vijijini kwa kujenga vituo vinavyoendeshwa kwa Nishati ya Nguvu za Jua (*Solar Energy*). Hadi kufikia Mwishoni mwa Mwezi Juni 2017 tayari vijiji viwili (2) vya Boma – Pangeni na Mgonjoni – Kilombero vimeshanufaika na Mradi huo na vituo hivyo vinaendelea kutoa huduma kwa wakazi wake.....

Mradi huu umejipanga kuanza utekelezaji wake katika Vijiji vyengine Sita (Vinne Unguja na Viwili Pemba). Vijiji hivyo ni Mikuyuni, Mlilile, Mapopwe na Bambi Kijibwemtu kwa Unguja na Mkiya wa Ng'ombe - Makangale na Tondooni – Mtambwe Kusini kwa Pemba. Vijiji hivyo vinatarajiwa kuendelezwa kwa awamu kwa kuanzia na Vijiji vya Mlilile na Mikuyuni.

KAZI ZA KAWAIDA.

KUTOA ELIMU KWA WATUMIAJI WA MAJI

Mamlaka ya Maji imefanya kazi kubwa ya uhamasishaji wa Jamii juu ya umuhimu wa kuchangia huduma ya maji na kutunza miundombinu ya maji. Maeneo yaliyohamasishwa ni: Paje, Bwejuu, Nungwi, Mkokotoni, Tumbatu, Donge - Kipange, Mahonda, Gamba, Jumbi, Dole, Kianga, Magogoni, Kilimani, Kihinani, Migombani, Pangawe, Kizimkazi Mkunguni, Kizimkazi Dimbani, Mtende na Kibuteni kwa Unguja na Shumba Viamboni, Tumbe, Mbuzini, Dodo, Matuleni Limbani, Kizimbani, Mgagadu, Jadida, Kiungoni, Wawi, Gombani, Ole, Kilindi, Kojani, Uweleni, Mtambile, Micheweni kwa upande wa Pemba.

UKUSANYANYAJI WA MAPATO

Mamlaka ya Maji Zanzibar katika kipindi kinachoripotiwa ilijipangia kukusanya jumla ya TShs bilioni 5.1 kutokana na mauzo ya maji na mauzo mengineyo. Hadi kufikia Juni, jumla ya TShs bilioni 2.739 zimekusanywa sawa na asilimia 53 ya makadirio.

Mamlaka haikuweza kufikia lengo iliojipangia kutokana baadhi ya maeneo kuwa na upungufu wa maji na hata yale maeneo ambayo huduma hii inapatikana vizuri wananchi walio wengi bado hawajaitikia vizuri wito wa kuchangia huduma hii.

Programu ya Kulinda na kuhifadhi vianzio vya maji

Miongoni mwa majukumu ya Mamlaka ya Maji ni usimamizi, utunzaji na uhifadhi wa rasilimali maji katika kutekeleza hayo Mamlaka ya Maji imeendeleza kazi ya upandaji miti katika maeneo ya Mwanyanya, Chumbuni na Kiashange ambapo jumla ya miti 400 imefanikiwa kupandwa na uzio umejengwa katika maeneo ya Chaani, Donge, Kiboje, Kisongoni, Bumbwisudi, Kinumoshi, Kianga na Mwembemchomeke.

MAFANIKIO YA ZAWA MWAKA 2016/2017

Katika kipindi hiki ZAWA imepata mafanikio mengi yaliyoimarisha huduma za maji visiwani Unguja na Pemba.

MAFUNZO YA WAFANYAKAZI

Katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2016/2017, ZAWA imefanikiwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwajengea uwezo wafanyakazi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kazi za kila siku. Idadi ya wafanyakazi waliopatiwa mafunzo inaonekana katika jadiweli lifuatalo:

Jadweli 1: ***Idadi ya wafanyakazi waliopatiowa mafunzo***

Ofisi	Muda mfupi nje ya Nchi	Muda mfupi ndani ya Nchi	Muda mrefu nje ya Nchi	Muda mrefu ndani ya Nchi	Jumla
Unguja	2	18	4	70	94
Pemba	2	0	3	15	20

MATENGENEZO YA MABOMBA

Mamlaka ya Maji imefanikiwa kufanya matengenezo ya mabomba katika maeneo ya Mwembeladu, Michenzani, Saateni, Kijichi, Kihinani, Kinuni, Dole, Dimani, Mfenesini, Vuga, Chumbuni, Makadara, Fuoni, Mwera, Chwaka, Koani, Makunduchi – Kibuteni, Migombani, M/Kwerekwe, Nungwi, Donge, Mahonda, Mkokotoni na Tumbatu kwa Unguja na Kwasharifu Ali, kwa Bimtumwa, Mgelema, Kironjo, Kijuki, Sizini, Mtambwe kaskazini, Darajani Mkoani kwa Pemba.

MAREKEBISHO YA UMEME

Mamlaka ya Maji Zanzibar katika mwaka wa fedha 2016/2017 ilifanikiwa kufanya marekebisho ya umeme katika vituo vifuatavyo: Welezo, Dimani, Mombasa, Mbweni, Kiashange No. 2, Magogoni, Kandwi, Kisongoni, Chaani *TASAF*, Kaburi kikombe, Mgeni haji *ADB*, Kibele, Kitogani, Jambiani, M/mchomeke, Chunga No. 9, Uroa – Pongwe, Makunduchi, Ukongoroni, Tumbatu, Dunga, Bumbwisudi, Bambi, Sebleni, Kinumoshi, Masumbani No 4, Fuoni, Kizimkazi, Kilombero, Bweleo, Mkorogo BH15, Umbiji, Kigongoni, Msikiti mzuri N10, Bwejuu, Mtopepo na Chwaka kwa Ungujana Ng'ambwa -2 na Kwapweza, Kijuki, Dawa na Mtambwe Kakazini, Bunguni, Wete - 5 Wete - 6 Toa B, Joho, Kwapopo, Mazrui, Kangani, Makombeni, Makangale kwa Pemba.

MATENGENEZO YA PAMPU NA MOTA ZILIZOUNGUA

ZAWA imefanikiwa kufanya matengenezo ya Pampu na Mota zilizoungua katika vituo vifuatavyo: Kibele, Msikiti Mzuri, Kizimkazi, Masumbani (Chukwani), Mbweni (Rais), M/Mchomeke No1, Binti Amrani No1, Kiashange *ADB* 4, Kisongoni, Tazari, Kaburi Kikombe, Kiembesamaki, Bambi *TASAF*, Mfenesini, Ukongoroni, Uroa/Pongwe, Bweleo, Mbweni BLW, Kwarara, Welezo, Chumbuni, *SEMUSO* na Mgambo kwa Unguja na Mahuduthi, Chambani, Mtambile, Kwa Changawe, Mbuzini, Mfikiwa, Mkanyageni, Finya, Tumbe Saninga, Wingwi Njuguni, Mtambwe Kaskazini. Kwa Bimtumwa Shumba Viamboni kwa Pemba.

KUJENGA/MATENGENEZO YA "*WELL – HEAD*"

Mamlaka ya Maji imefanikiwa kujenga na kufanya matengenezo ya "*Well – head"* katika maeneo ya Mwanakwerekwe C, Uwanja wa Mao Tse Tung, Chaani Masingini, Magogoni, Welezo *(RH)*, Jambiani Kivuli, Kigongoni, Kijitoupele, Kilindi No.2 na Ukongoroni kwa Unguja na Tumbe, Saninga, Shumba Viamboni Mbuzini, Changuo, Kwa Bimtuma, Junguni, Finya kwa Pemba.

UFUNGAJI WA MITA NA USAJILI WA WATEJA WAPYA WA MAJI

ZAWA katika kipindi cha Julai 2016 hadi Juni2017 imefanikiwa kusajili wateja wapya 3,118 Unguja na Pemba.

Aidha, imefanikiwa kufungamita 2,204 katika maeneo yaMigombani, Melinne Kihinani, Kizimkazi na Jambiani kwa Unguja na Limbani, Kizimbani, Mgagadu, Jadida, Kiungoni,

Madungu, Wawi, Gombani, Ole, Kilindi, Kojani, Uweleni, Mtambile, Michewenikwa upande wa Pemba.

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA MAJI ZAWA

ZAWA inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazopelekea kutokufikiwa kwa ufanisi na utoaji bora wa huduma za maji safi na salama, changamoto hizo ni kama ifuatavyo;

(i) Upotevu wa maji - Inakadiriwa takribani asilimia 30 ya maji hupotea kabla ya kuwafikia watumiaji.
(ii) Uchakavu wa miundombinu - Sehemu kubwa ya mtandao wa maji ni chakavu na ni ya zamani.
(iii) Ongezeko kubwa la mahitaji ya maji kulingana na uwezo wa uzalishaji.
(iv) Upungufu wa bajeti kwa ZAWA kukidhi mahitaji ya pampu za akiba
(v) Uchache wa fedha wa kuendeleza visima vilivyochimbwa na Mradi wa Ras- al Khaimah.
(vi) Uwezo mdogo wa kununua mita za maji za kutosha
(vii) Uvamizi wa vianzio vya maji
(viii) Mabadiliko ya tabia nchi

MIKAKATI INAYOENDELEA

ZAWA imejipanga kutekeleza mikakati ifuatayo katika mwaka wa fedha 2017/2018:

(i) Kutekeleza Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Mji Mkongwe wa Zanzibar "*ADF 12*", .

Mradi huu unamadhumuni ya kuimarisha upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira kwa Mji Mkongwe na baadhi ya maeneo ya Ng'ambo ya Asili. Mradi utajumuisha uchimbaji wa visima vipya 10, ubadilishaji wa mabomba wenye urefu wa kilomita 68, ujenzi wa matangi 4 ya juu ya ardhi *(Elevated Tank),* matengenezo ya visima vikongwe 30 na ufungaji wa mita mpya 6,900. Mradi huo unakadiriwa kuongeza uzalishaji kutoka lita 67 milioni kwa siku kwa Mkoa wa Mjini Magharibi na kufikia lita 81 milioni kwa siku ambalo ni ongezeko la asilimia 20.9.

(ii) **Ukarabati wa Miundombinu ya Maji Zanzibar**

Mradi huu utakaotokana na mkopo wa dola 92.1 milioni *(USD)* kutoka Serikali ya India. Mradi huu unatarajiwa kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu katika maeneo ya ng'ambu na kando ya Mji wa Zanzibar.
Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea na mazungumzo na Serikali ya India. Mradi huu utakapofanikiwa utaimarisha upatikanaji wa maji katika maeneo mengine ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

(iii) Mradi wa ukarabati wa miundombinu ya maji kwa baadhi ya maeneo ya Mkoa wa mjini Magharibi.Mradi utakaotokana na Mkopo wa Serikali ya Japani, umekamilisha upembuzi yakinifu *(Preparatory Survey).* Hatua inayofuata ya mradi huu ni utayarishaji wa andiko la mradi.

(iv) Mradi wa uchimbaji wa visima na usambazaji maji vijijini- Mradi huu utajumuisha uchimbaji wa visima, ulazaji wa mabomba, ujenzi wa matangi pamoja kuunganishwa na mfumo wa sasa wa maeneo ya vijijini Unguja (Donge, Chaani, Kisongoni, Kiboje na Miwani).

(v) Uendelezaji wa mradi wa uchimbaji wa visima wa wa Ras Al Khaymah- Visima vyengine 26 vitaendelezwa katika maeneo tafauti Unguja na Pemba.

HITIMISHO

Kutokana na utekelezaji wa kazi tulizozitaja za mwaka 2016/2017 *ZAWA* imeweza kuongeza utoaji wa huduma ya maji Unguja na Pemba Mjini na Vijijini na kufikia asilimia 87Mjini na asilimia 70 vijijini. Kutokana na mikakati iliyotayarishwa matarajio ni kuwa ifikapo 2020 usambazaji wa huduma ya maji unatarajiwa kufikia asilimia 97 kwa mjini na asilimia 87 vijijini.

Ongezeko hilo litatokana na miradi mikubwa iliyoainishwa pamoja na midogo ya wananchi. Inatarajiwa kwamba kukamilika kwa miradi hiyo na kupunguwa changamoto zilizotajwa kutasaidia kwa kiasi kikubwa juhudi ya Serikali katika uimarishaji wa huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ***" KILA TONE LA MAJI NI GHARAMA TUMIA MAJI KWA UANGALIFU"***

Baada ya uwasilishaji wa ripoti hii, kwa heshima kubwa Naomba kutoa hoja.(Makofi)

UTARATIBU

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mweyekiti, kuhusu utaratibu au muongozo wake, ripoti hii tumeiona ripoti nzuri sana, lakini katika ripoti hii nimetumia sheria N. 4 ya 2006 inatakiwa Mhe. Waziri, awasilishe *annual report* kifugu cha 34(1) lakini mpaka hapa katika ripoti hii hatujaona *annual report* ambayo iko *auditing report* kifungu Na. 3 *Minister shall table before the House of Representative the annual report with the auditing report and report of own authority.* Sasa sijaona katika ripoti hii kuw na *auditing report* naomba uongozi wako.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe Mhe. Waziri una jibu la hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Muwakilishi kuhusu suali hili, tumeweka *annuel report* kama nilivyoripoti mwanzo na kweli katika sheria pale imeandikwa haina tatizo na wakati naleta ripoti hii barazani niliandika kabisa kwamba ripoti hii nimeleta kwa mujibu wa taratibu zilizotakiwa lakini bado haijawa *auditing*, kwa hiyo hiyo naomba nitoe taarifa lakini ni vyema pia Baraza

likajua hali halisi ya utekelezaji ili waweze kujua hali ya *situation* nzima ilivyo na waweze kujua. Kwa hivyo bado tulikuwa tunaendelea kutekeleza yale maagizo au ushauri wanaoutoa katika kuhakikisha kwamba tunafikia lile lengo ambalo tumelikusudia.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri na nampongeza wakati wote kwa kuwa yeye ni mtu wa mwanzo, na hoja hii ya msingi ilikuja katika hoja yangu binafsi ya kuwa mashirika ya umma na taasisi za Serikali kuwa hazileti ripoti hapa, namshukuru yeye kwa kuwa mtu wa pili wa mwanzo akifuatiwa na mwalimu.

Lakini *argument* yangu ipo ripoti tumeiona lakini hakuna *accounting auditing report* haipo hii tutaipata wapi wakati vyote hivi vinafuatana kwa pamoja hiyo ndio *argument* yangu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu vizuri kaka yangu ndugu Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na anachokitaka, kwa maana ile taarifa ya Mashirika ya umma kw mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma, ile nadhani nilisema hapa kwamba kuanzia mwaka wa fedha ujao maana yake sasa tunajiandaa ili mashirika ya umma yote yalete ripoti zake Barazani pamoja na *ouditor* kwa mujibu wa sheria. Taarifa iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri ni taarifa maalum iliyotakiwa kuwasilishwa katika Baraza hili na sio taarifa ile aliyosema Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa mujibu wa sheria ya mashirika ya umma.

Hiyo itakuwa kuanzia mwaka wa fedha wa 2018/2019 kwa mashirika yote kama tulivyokwisha ahidi naomba kutoa taarifa hiyo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti nikuhukuru na nimshukuru sana kaka yangu Waziri wa Fedha na mtu ambaye namheshimu sana kupita kiasi, lakini hii sheria ndio iliyoundwa na ndio inayosema hapa kuwa inapoletwa ripoti barazani nailetwe *auditing na account report* yake sasa ukisema tunajitayarisha maana yake hii sheria tuliipitisha vipi, hii sheria tuliipitisha sheria halali na Rais wetu ndio aliyetia saini hii, sasa mimi sipati picha nataka kujua kwa nini auditing *report* haijaja.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nizungumze kidogo labda Mhe. Mohammed Said Mohmmed sijui lengo lake, lakini yeye alileta hoja na tukasema alisema hivi katika hoja yake naomba ninukuu na nilikuwa makini sana.

Alisema: Hatutoweza kupitisha Bajeti ya Wizara ya mwakani bila ya kuletewa report, sisi kawaida mimi nimeingia April 2017/2017 kawaida ukishakutengeneza ripoti sasa hivi lazima iende ka *CAG* na *CAG* hatoi ripoti leo, lakini sasa hivi tunakwenda kwenye *process* na wakati tunakwenda kenye *process* tukasema basi tulete taarifa maalum angalau kama alikuwa anataka kujua *highlight the situation* basi *situation* iweze kupatikana na aweze kukidhi ile haja, lakini taarifa hii tayari imeshakwenda kwa *CAG* na itakapokuja tu kama anahitaji basi tutampatika.

Lakini sasa hivi tulisema tujue kwa sababu humo ndani kilio kikubwa ni maji lakini tukipata ushauri tukipata mawazo yao na kile tulichokitekeleza kwa mwaka mzima uliopita basi waweze pia kukijua na hicho ndicho kilikuwa kilio kikubwa ambacho yeye pia alikuwa anakihtaji, sasa

kama alikuwa anataka mahesabu hicho kitu chengine sasa anaki-*request* leo mbele ya baraza lako ambacho pia hakina mjadala tuko katika kutekeleza.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa mara ya mwisho.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru mbona umeturuhusu watu wawili Mhe. Mwenyekiti umeniruhusu mimi au Mhe. Machano.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohammed Said Mohammed kaa kitako tusikilize utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, muda wa kawaida wa baraza umeisha ama tuongeze muda au tumalize tutoke,

Mhe. Mwenyekiti: Nimekusikia lakini saa yangu inaonyesha bado kuna dakika tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohammed Said Mohammed tumalizie hoja kwa mara ya mwisho.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru nilichokisoma mimi ni sheria hii na sheria No. 6 ya mwaka 2006 ndio sheria ninayoisoma mimi na hicho ndicho kinachotaka matakwa ya kisheria, tukiweza kufuata matakwa ya kisheria ndio tutaweza kubalance vitu hivyo, lakini kama hatutaweza kuleta matakwa ya kisheria mimi nakubali kuwa *annual report* ipo lakini *auditing report* iko wapi.

Sasa ninachotaka kusema mataka ya kisheria *annual report* imefuatwa lakini tumekiuka sheria hii tumeitunga sisi tumeikiuka katika kifungu cha 3.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa nimekusikia lakini hiyo hoja yako unaweza kuileta tena baadae lakini kwa muda huu naomba niakhirishe kikao hichi hadi Saa 11.00 jioni, nawashukru sana na niwaombe sana ana kwa kuwahi kwa wakati ili tuweze kuendelea na hoja yetu iliyoop mbele yetu ahsante sana.

(Saa 7.00 Mchana kikao kiliakhirishwa mpaka saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti

Ripoti ya Mwaka ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) Kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa kwanza naomba kabisa tumshukuru sote Mwenyenzi Mungu aliyeumba dunia hii na pamoja na viumbe vyake, kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kufika hapa siku ya leo mbele ya Baraza lako Tukufu, tukiwa wazima kabisa tena wenye afya njema na tukiwa na bashasha katika mioyo yetu kwa lengo la kujadili mambo muhimu yanayohusu maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, **k**ukutana huku pia kutatuwezesha kujadili Ripoti hii ya mwaka ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar yaani (ZAWA) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ambayo inatimiza matakwa ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2016), ambapo inazitaka Mamlaka zote zinazojitegemea kuwasilisha Ripoti zao za mwaka katika Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kujadiliwa.

Kwa hili niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tumpongeze sote Mhe. Waziri Salama Aboud Talib Waziri wa Ardhi, kupitia Mamlaka ya Maji (ZAWA) kwa mara ya kwanza kuleta ripoti ya utekelezaji ya mwaka na tunazitaka Mamlaka nyingine ziige mfano huu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniruhusu kusimama mbele ya hadhara hii ili niweze kuwasilisha Ripoti hii kwa niaba ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi, Hotuba ya Maoni kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar yaani (ZAWA) ya Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na taadhima kwa mara nyengine tena napenda tena kutoa shukrani zangu za dhati kwa kwako wewe Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuona umuhimu wa kuwasilisha Ripoti hii Hapa Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, kuwasilishwa kwa Ripoti hii ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) katika Baraza hili kunatoa fursa kwa wananchi kujua Miradi mbalimbali ya kuijengea uwezo Mamlaka, mafanikio yake japo kwa kiasi kidogo, lakini vile vile kuweza kujua changamoto zinazoikabili sekta ya maji hapa Zanzibar, sambamba na mikakati inayoendelea. Hali ambayo inapelekea kurudisha imani kutoka kwa wananchi kwa Mamlaka hiyo kwa utekelezaji wa majukumu yake ambayo hupelekea kuondosha kwa kiasi kikubwa tatizo la maji katika visiwa hivi vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya kutanguliza shukrani hizo, sasa niendelee kwa kusema kuwa, Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa kiasi kikubwa imejitahidi kutoa ushauri na nasaha kwa Wizara juu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka, kwa mantiki hiyo na kwa moyo mkunjufu kabisa naomba niwatambue, Wajumbe wa Kamati hii ambayo tumeshirikiana katika kuandika Ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa ruhusa yako, naomba niwataje wajumbe wa Kamati ikiongozwa na mimi mwenyewe ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati:-

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Suleiman Sarahan Said	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Khadija Omar Kibano	Mjumbe
4.	Mhe. Mohammedraza Hassanaali	Mjumbe
5.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
6.	Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
7.	Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil	Mjumbe
8.	Mhe. Said Omar Said	Mjumbe

Lakini Kamati hii ilikuwa vile vile, inasaidiwa na Makatibu wetu wawili.

9.	Ndg. Fatma Omar Ali	Katibu
10.	Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ni moja ya Wizara nyeti katika nchi yetu kutokana na ukweli kwamba inasimamia sekta muhimu ya maji kwa maendeleo ya nchi na viumbe hai katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kusemwa kweli Kamati yangu inaona jitihada za Serikali yetu ikihangaika kutafuta kila njia ya kuwaondolea wananchi wetu shida ya kupata maji kutokana na dhiki wanazozipata kila siku. Kupitia jitihada hizo Serikali hapo mwanzoni iliunda Idara ya Maji kwa ajili ya kusimamia na kuhakikisha inaondoa tatizo la maji.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, baada ya kuona huduma ya Maji bado inasuasua nchini, Serikali iliamua kwa makusudi kutunga Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Maji yaani (ZAWA), Sheria Namba 4 ya mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria hiyo ilipelekea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Uzalishaji na Usambazaji wa Maji hapa nchini Zanzibar, lakini pamoja na jitihada hizo za Serikali, inaonekana iko haja ya kuitupia macho kwa karibu kabisa Mamlaka hii ili kuipa nguvu zaidi iweze kutimiza malengo yake mazuri kwa Serikali yetu ya kuwapatia wananchi wetu maji wa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa heshima yako baada ya utangulizi huo sasa naomba nitoe maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano, kama ifuatavyo katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za Mamlaka ambapo Kamati yangu vile vile, itaweza kutoa ushauri pamoja na maelekezo.

Mhe. Mwenyekiti, Ripoti hiyo ya imeelezea programu mbali mbali za maendeleo katika mwaka huu ikiwemo:

a) Uhuishaji na upanuzi wa shughuli za Maji Mijini.
b) Programu ya usambazaji vijijini.
c) Programu ya kulinda na kuhifadhi vianzio vya maji.

Mhe. Mwenyekiti, Katika Programu ya Uhuishaji na Upanuzi wa Shughuli za Maji hapa Zanzibar, Kamati yangu imeona jitihada zinazochukuliwa na Mamlaka kwa kuanzisha miradi mbali mbali ya uchimbaji na uwekaji miundombinu ya maji, miradi ambayo inafadhiliwa na ADB, EXIM BANK ya CHINA, JICA, na Serikali ya INDIA lakini vile vile, kupitia Mkopo wa ADB pamoja na fedha za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, Kamati imeona jitihada nyengine zinazochukuliwa na Mamlaka ya kuchimba visima vipya pamoja na kukarabati vyengine vya zamani kazi iliyobakia ni ununuzi na ufungaji wa mitambo na pampu za kuvutia maji kama alivyoelezea Mhe. Waziri katika hotuba yake mradi huo ambao umefikia karibu asilimia 98 na unategemewa kuanza kazi mwishoni mwa mwezi wa Febuari, 2018.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu imeridhika na hilo lakini inaitaka Mamlaka kuhakikisha kuwa mradi huo ukimalizika ni kweli maji yatapatikana kwani tumeshuhudia huko nyuma miradi mingi inatiliwa fedha lakini ikimalizika faida yake inakuwa ni tofauti na vile ilivyokuwa inaelezwa, kwani tatizo la maji linabaki pale pale, kwa hiyo kazi iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha kwamba miradi hii mipya ambayo tunaiidhinisha hapa Barazani na inatimiza matarajio ya wananchi ambao tunawawakilisha hapa Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaamini mradi huu wa ADB na SMZ ambao umefikia karibu asilimia 98 ukikamilika kwa wakati na ujenzi wa matenki hayo mapya ya maji kwa kiasi kikubwa vinaweza kusaidia kuondoa tatizo la Maji katika Mkoa wetu wa Mjini na Magharibi, eneo ambalo lina watumizi wengi wa na maji yanatumika sana katika eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia imeridhika na utekelezaji wa wa program ya Ujenzi wa vyoo na kuimarisha usafi mashuleni jambo ambalo linasaidia kulinda afya za watoto wetu pamoja na walimu wao. Aidha, suala la ulipaji fidia tunaipongeza Mamlaka kwa kuweza kulipa fidia kwa mali za wananchi zilizoharibiwa kupitisha miradi hii karibu asilimia 80 tunaiomba Mamlaka hiyo, hiyo asilimia 20 iliyobakia waweze kuwalipa wananchi ili waweze kukidhi mahitaji yao kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia inaiomba na kuishauri Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji (ZAWA) kuhakikisha Miradi yote iliyokusudiwa kutekelezwa kwa mwaka 2016/2017 iwe imetekelezwa ipasavyo kwani kutotekelezeka kwa miradi hiyo ni kupelekea kuwakosesha huduma muhimu ya Maji wananchi wetu wa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Miongoni mwa Miradi hiyo naomba kwa kifupi niitaje:

1. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji na kujenga Uwezo Mamlaka kifedha, lakini vile vile,
2. Mradi wa Kuijengea Uwezo Mamlaka ya maji (Awamu ya Pili, Tatu),
3. Mradi wa Uchimbaji wa Visima unaofadhiliwa na Serikali ya China, na
4. Mradi wa Uchimbaji Visima unaofadhiliwa na Mtawala wa Ras al Khaimah.

Mhe. Mwenyekiti, Mradi wa Uchimbaji wa visima unaofadhiliwa na Mtawala wa Ras al Khaimah, Kamati bado hairidhishwi na utekelezaji wa mradi huo kwa upande wa Unguja na Pemba. Kwani Mradi huo umechimba zaidi ya visima 150 Unguja na Pemba kwa ajili ya kusambaza huduma za maji safi na salama kwa wananchi wetu wa visiwa hivi, likini vingi ya visima hivyo bado hadi leo havijaungiwa umeme na kuunganishwa na mitandao ya maji ili kuweza kupatikana maji kwa haraka kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka hii bado inakabiliwa na baadhi ya changamoto mbali mbali, ambazo zinakwamisha utendaji wa shughuli za Mamlaka na hii Mamlaka kuweza kutofanya kazi zake kwa ufanisi na utoaji bora wa huduma za Maji na salama.

Mhe. Mwenyekiti, Changamoto hizo ni upotevu wa Maji, Uchakavu wa Miundombinu, Ongezeko la ukubwa wa Mahitaji ya Maji kulingana na Uwezo wa Uzalishaji, Upungufu wa Bajeti kwa ZAWA, uchache wa fedha za kuendelezea Visima vilivyochimbwa na Miradi ya Ras al Khaimah, Uwezo Mdogo wa kununua Mita za Maji za kutosha, lakini vile vile na uvamizi wa Vianzio vya Maji pamoja na Mabadiliko ya Tabia ya Nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na Changamoto hizo zinazopelekea Mamlaka hii kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara kuisaidia Mamlaka hii hususan, katika suala zima la upatikanaji wa Bajeti kwa wakati ili Mamlaka iweze kufikia yale malengo yake waliojiekea.

Mhe. Mwenyekiti, panapo changamoto hapakosi mafanikio hivyo basi, miongoni mwa Mafanikio waliyoyapata (ZAWA) katika mwaka ni kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake 114, kwa upande wa Unguja na Pemba kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, mafunzo hayo ni ya muda mfupi na muda mrefu ambayo yanaweza kuwajengea uwezo wafanyakazi wake katika utekeleza majukumu yao ya kazi za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, vilevile, Kamati yangu haikuridhika kabisa na makusanyo ya mapato kwa mwaka huu wa 2016/17 kwa kuweza kukushanya kiasi cha Tshs Bilioni 2.7 kati ya fedha zilizotarajiwa za Bilioni 5.1, lakini hii yote inasababisha wananchi wanakuwa wagumu kuweza kulipia maji kwa wakati kwa sababu muda mwingi hayo maji yenyewe yanakuwa hayapatikani, na ndio maana tukaiomba Serikali itoe pesa za pamoja kwa kuviunga visima vya Ras al Khaimah ili maji yaweze kupatikana kwa wingi na wananchi wetu waweze kupata nguvu ya kuweza kulipa huduma hiyo muhimu ya maji.

Pamoja na hayo, Kamati inaitaka Mamlaka kuongeza kasi ya ufungaji wa mita na bili za maji jambo ambalo litaweza kusaidia ongezeka la makusanyo kwa haraka, pia kuweza kuunganisha wateja watakaopatiwa huduma hiyo kwa kulipia bili za maji kwa njia ya simu za mkononi jambo ambalo pia litasaidia kurahisisha ukusanyaji wa mapato na kuongeza makusanyo katika bili za maji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia Kamati yangu inaiomba Wizara kufanikisha utekelezaji wa mikakati inayoendelea kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambayo ni pamoja na Utekelezaji wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira ya Mji Mkongwe, Uratibu wa Miundombinu ya Zanzibar, Miradi ya Ukarabati wa Miundombinu ya Maji kwa baadhi ya Maeneo ya Mkoa wa Mjini

Magharibi, Mradi wa Uchimbaji wa Visima na Usambazaji Maji Vijijini pamoja na kuendeleza Mradi wa Uchimbaji wa Visima kwa Maeneo ya Unguja na Pemba kwani kufanya hivyo kutapelekea kumaliza kabisa tatizo la maji hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya hayo yote tuliyoelezea katika kuichangia ripoti hii iliyowasilishwa na Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, Kamati inakuja na mapendekezo haya makhsusi ambayo tunaamini kama yatatekelezwa ipasavyo na Serikali, basi tatizo la maji hapa Zanzibar litakuwa historia. Hivyo basi, ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe waunge mkono mapendekezo ya Kamati ili Serikali iweze kuyatekeleza kwa faida ya wananchi wetu. Miongoni mwa Mapendekezo hayo Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yao naomba niyataje:

1. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ripoti ya Mhe. Waziri imeeleza miradi tofauti inayotekelezwa kupitia pesa za mikopo kutoka taasisi na nchi mbali mbali lakini bado programu hizi zitachukua muda kuweza kukamilika kwake kutokana na ukubwa lakini vile vile, na mikataba yenyewe. Kwa hiyo, Kamati inakuja na suluhisho la haraka kuweza kupunguza au kumaliza tatizo la maji katika maeneo yetu. Kwa hivi sasa kuna visima vingi zaidi ya 120 kati ya visima 150 ambavyo tayari vimeshachimbwa kwa msaada wa Ras al Khaimah, na kwa kuwa visima hivi vinayo maji ya kutosha ya kuondoa tatizo la maji kwa kiasi kikubwa katika nchi yetu na ili viweze kukamilishwa vyote zinahitajika kiasi cha fedha karibu Bilioni 8.8 Kamati yetu inaiomba Serikali kuipa fedha Mamlaka ya Maji ndani ya kipindi cha miaka miwili. Fedha ambayo, kwa mwaka huu waweze kupatia bilioni 4, na mwakani waweze kupatiwa bilioni 4 nyengine baada ya kufanya tathmini ya awamu ya mwanzo ya kukamilisha hizo bilioni 4 za mwanzo lakini vile vile, Kamati inaamini kwa kiasi kikubwa matatizo ya maji katika visiwa hivi vya marashi ya karafuu itaweza kuondoka kabisa iwapo Serikali itakubali wazo letu hili la kutoa fedha kwa ajili ya kuweza kukamilisha mradi huu wa wa Ras al Khaimah.

2. Mhe. Mwenyekiti, Kwa kuwa hivi sasa pampu karibu nyingi visima vingi ambavyo maji yamo pampu za kuvutia na kusukumia maji zimekufa kabisa, basi kupitia fedha hizo wataweza kununua pampu za kutosha na nyingine kuwepo za akiba ili isiwe kama ilivyo hivi sasa pampu ikiungua inachukua miezi 4 mpaka miezi 6 bila ya kupatikana pampu nyingine jambo ambalo linapelekea wananchi kupata taabu ya upatikanaji wa maji safi na salama wakati ndani ya visima maji yapo ya kutosha.

3. Mamlaka kuanzia sasa kuacha kununua pampu wao wenyewe na badala yake kutafuta *“SUPPLIER”* ambae ataweza kusambaza pampu hizo kwa kuweza kupata *“Garantee”* na uhai na umadhubuti wa pampu hizo kwa mamlaka.

4. Aidha, Kamati inashauri Karakana ya kutengenezea pampu iliyopo hapo Saateni iweze kupatiwa nyenzo za kutosha tena za kisasa zikiwemo mashine za kisasa, pamoja na mafunzo zaidi kwa mafundi wetu ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi wa kutosha.

5. Kutokana na Mamlaka kuwa na majukumu mengi ambayo yanasababisha kushindwa kuyasimamia vizuri na kwa wakati muafaka, Kamati yangu kupitia ziara ya

kimafunzo tuliyoipata kupitia kwa wenzetu Tanzania Bara basi ni vyema tunashauri taasisi nyingine ambayo tunapendekeza Serikali kuanzisha ambayo itakuwa Wakala wa Serikali yaani ZAWASCO ili ZAWA ibakie na jukumu la kuandika, kubuni na kuandaa miradi mikubwa ambayo yenye manufaa kwa nchi yetu. Hivyo, Kamati yetu inashauri Mamlaka kuwa na Wakala wake na kazi zake zitakuwa huyo Wakala kazi zake itakuwa ni uwekaji wa miundombinu ya maji pamoja na usambazaji wa kama ilivyo kwa wenzetu Tanzania Bara yaani DAWASCO. Kwa hiyo, itakuwa vyema iwapo na sisi Zanzibar kuwa na Taasisi mbili, moja ni Mamlaka ZAWA lakini vile vile, Taasisi ya Usambazaji wa Miundo mbinu ya maji ZAWASCO ambapo kila mmoja itakuwa na jukumu lake tofauti na tunategemea ufanisi utaweza kupatikana.

6. Mhe. Mwenyekiti, serikali kwa kushirikiana na Wizara kuanzisha Taasisi au Bodi kwa mujibu wa sheria na itakuwa kazi ya kuvilinda na kuviendeleza na kuvitunza vianzio vya maji hapa Zanzibar. Ili kunusuru uvamizi wa vianzio hivyo vinavyoendelea katika maeneo ya nchi yetu katika maeneo mbali mbali. Sheria hiyo iweze kuwapa mamlaka au uwezo dhidi ya mtu yeyote aliyejenga katika vianzio vya maji, aliyevamia katika shughuli za kilimo au uharibifu kwa njia yoyote katika vianzio vya maji basi sheria hiyo iweze kuchukua hatua mara moja kwa kuweza aidha kuzivunja nyumba hizo zilizojengwa katika vianzio vya maji au kuteketeza kitu chengine chochote kilishowekwa katika vianzio hivyo vya maji bila ya kuoneana muhali. Hii itapelekea wananchi kuheshimu vianzio hivyo vya maji ikiwemo chem chem na mapango ya maji. Sambamba na hilo kamati inaishauri serikali kukaa pamoja na wizara kuweza kuunda Kamati maalum itakayoweza kudhibiti uhifadhi kwa vianzio vya maji ambavyo vinaonekana kuvamiwa kwa kasi kubwa na kwa asilimia kubwa katika hizi siku za karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi ya Kamati sasa nitaomba unigaiye japo dakika tano ili na mimi niweze kutoa maoni yangu binafsi kupitia ripoti ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyoeleza katika ripoti yetu kwamba tatizo la maji Zanzibar lipo katika kila eneo. Lakini kutokana na jitihada yenyewe ya serikali hasa katika kuchimba hivi visima vya Ras al Khaimah, Kamati yangu imetembelea visima mbali mbali katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Sasa ndiyo maana tukaja na ushauri kwa kuwa ZAWA wenyewe wameshaweka bajeti karibu bilioni 8 kuweza kuifanyia *installation* kuviunganisha visima hivi vyote.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika *research* fupi tuliyoifanya kwa upande wa maeneo ya Dimani, kuna visima karibu sita (6) ambavyo tayari vimeshachimbwa vina maji ya kutosha lakini hakuna pampu wala havijaungwa umeme kwa ajili ya kusambaza kwa wananchi. Ukija Chumbuni kuna visima karibu vitatu (3), visima vile vikiweza kuunganishwa wananchi wa maeneo ya jimbo la Chumbuni, Shaurimoyo, Makadara, Rahaleo, mpaka Mjimkongwe, majimbo haya yatakuwa hayana tatizo la maji. Lakini ukija katika maeneo ya hapa Welezo kuna visima karibu vitatu (3) vimeshachimbwa bado havijaweza kuunganishwa. Vile vile katika eneo la Mwembemchomeke, kuna visima karibu vitatu (3) navyo vimeshakuwa tayari bado havijaweza kuunganishwa na miundombinu ya umeme pamoja na pampu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaamini serikali kama hili wazo letu tulilotoa kama Kamati kuweza kuingiza fedha kuwapa ZAWA kuweza kukamilisha kuunganisha miradi hiyo, tunaamini matatizo yataweza kuondoka. Hayo nimeyazungumza kwa Mkoa wa Mjini wa Magharibi peke yake. Vile vile kuna eneo la Michamvi ambalo Mhe. Jaku Hashim Ayoub siku zote hapa Barazani amekuwa akipiga kelele, wakati mwengine Mhe. Jaku anatumia gharama kubwa kwa wananchi wake na wakati mwengine ukiangalia hata huwo mfuko wa Jimbo anautumia katika kusambaza maji. Leo kisima tayari kipo serikali imeshachimba kisima, lakini visima vile havijaunganishwa na maji.

Mhe. Mwenyekiti, tunategemea kwa *geography* ilivyo Zanzibar visima vya maji vipo Zanzibar nzima tena vimeshachimbwa vina maji ya kutosha. Naomba sana Wajumbe wa Baraza hili tuunge mkono mapendekezo ya Kamati, serikali na tumependekeza kwa sababu fedha zimo ndani ya bajeti. Kama fedha ambazo hazitoshi kwa mwaka huu Mhe. Waziri alete *supplementary budget* sisi tuipitishe na hayo ndiyo majukumu yetu hapa Barazani, tuweze kutoa fedha katika mfuko Mkuu wa Serikali tuingize ZAWA ili tuweze kupata fedha kwa ajili ya kuondoa tatizo la maji.

Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, kwa kutegemea miradi ambayo inaendelea na tunagemea mengine inamaliza mwaka 2019. Mwaka 2019 sisi tunakwenda katika uchaguzi maji hayajapatikana tutakaa vipi. Mimi naomba sana visima vya Ras al-Khaimah havitaki *feasibility study* havitaki uchambuzi yakinifu, havitaki *consultancy*, vinataka fedha viunganishwe wananchi tupate kunywa maji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache ambayo nimetumwa na wananchi wangu wa jimbo la Shaurimoyo lakini vile vile na Kamati baada ya kufanya hiyo ziara, tunaamini mapendekezo yetu yatakuwa ni muarubaini wa kuweza kumaliza tatizo la maji. Naamini Mhe. Waziri makini Mhe. Salama Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira Mhe. tunaamini pengekezo letu hili akija hapa tunaamini ataweze kulikubali.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia Mhe. Waziri kazi aliyopewa ni kubwa sana, mimi nataka niseme kama kule Bara kuna Kairuki na sisi tuna Kairuki wetu Kairuki wetu sisi ni Salama Aboud Talib, tunaamini tukimpa nyenzo ataweza kufanya kazi na maji yataweza kupatikana.
Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono ripoti ya kamati na naunga mkono pamoja na mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Mazingira. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa uwasilishaji wako. Waheshimiwa Wajumbe sasa mchangiaji wetu wa pili baada ya Mhe. Hamza Hassan Juma naomba nimwite Mhe. Machano Othman Said atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajiandae.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini pia nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na uziima jioni ya leo kuweza kuzungumzia ripoti hii ya Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, upo usemi unaosema kwamba maji ni uhai na bila ya maji mambo mengi hayendi vizuri. Waheshimiwa wengi wenye majimbo jambo kubwa ambalo linalowahangaisha majimboni ni ukosefu wa maji safi na salama, inawezekana majimbo mengine maji yapo kidogo lakini siyo yale salama na ndiyo maana leo asubuhi Mhe. Waziri wa afya alivyokuwa akizungumzia kipindupindu aligusia sana maradhi haya yanasababishwa na ukosefu wa maji safi na salama.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake lakini nahisi bado kazi kubwa tunayo kuhusu sekta ya maji. Hata ripoti yao ukiisoma unaona kwamba bado lipo tatizo. Vipo visima vya Ras al-Khamah 139 lakini visima vilivyokamilika ni 24 Unguja na Pemba, Unguja 10, Pemba 14, visima 114 bado havijakamilika na havifanyi kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mradi huu Ras al-Khaimah jimboni kwangu mimi kuna visima 5, visima vitatu kwa ajili ya Kihinani na maeneo ya karibu, kisima kingine kipo Chuini na kuna kisima kipo Mwakaje Mwachalale. Hivi visima vyote vitano havifanyi kazi. Sasa kama tungeliweza kuvimaliza visima hivi nina hakika matatizo ya maji yangepungua sana katika maeneo yetu. Katika ripoti hii hii wamezungumza kwamba pia wanalo tatizo la upoteaji wa maji kwa 30% kama ukifanya hesabu wastani huo ambao unaodaiwa tunayo maji ya 75% kama ukitoa 30% ya upotevu njiani basi tunakuwa tunapata maji karibu 49.5% chini ya 50% ya maji.

Mhe. Mwenyekiti, jimboni kwangu mimi ukienda leo maeneo ya Mfenesini Kama kuna mabomba makubwa yamepasuka kuliko mwaka mzima na hayajatengenezwa na maeneo mengine hali kama hiyo, kwa hivyo hapa lipo tatizo. Mimi naomba kwanza Mamlaka iwekeze nguvu kufanya matengenezo ya mabomba makubwa wakati wakisubiri hiyo miradi yao mengine. Pia kuna tatizo la uharibifu wa mara kwa mara ya pampu na moto zake. Kitabu chake Mhe. Waziri ukikisoma kwa ujumla karibu pampu 35 zimeharibika. Sasa haya mambo yatakuwa magumu hayaendi. Labda kuna tatizo katika ubora wa pampu au labda watueleze kuna nini mpaka hizi pampu zinaharibika mara kwa mara au pengine kuna matatizo ya umeme. Tunaomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atueleze tatizo hasa ni nini.

Mhe. Mwenyekiti, lakini maji na katika nchi yetu tunakubaliana kwamba pato la taifa ligawanywe kwa wananchi wote, maendeleo yaende kwa wananchi wote, huduma za jamii ziende kwa wananchi wote. Sisi katika jimbo letu, Bumbwisudi vimechimbwa visima 9, kisima kimoja ambacho kilichochimbwa Bumbwisudi tumeambiwa ndio kisima ambacho kina maji mengi kwa Zanzibar nzima. Leo hii habari ambazo tunazo kwamba visima vile maji yote yaje Mji Mkongwe halafu watu wa Bumbwisudi, Kitundu, Mwakaje, Mfenesini, maji yale yapite yanaelekea Mjimkongwe hivyo itakuwa siyo haki.

Mimi naomba Mhe. Waziri namuomba sana kama visima vile 9 basi vitatu vibakie kwa wananchi wa jimbo la Mfenesini na majimbo jirani ya Wilaya ya Magharibi (A) na hivyo sita wapeleke maji Mji Mkongwe ambapo kila siku yanapelekwa.

Mhe. Mwenyekiti, Mji Mkongwe hakuna kipindupindu, hakuna lolote kwa sababu wanapata maji safi na salama lakini sisi majimbo yetu ambayo hayana maji safi na salama watu wanapata vipindupindu na wanapata maradhi mengine. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri azingatie

katika ugawaji wa visima 9 vile itakuwa siyo haki visima 9 vyote kuletwa maji mjini zaidi Mji Mkongwe, visima vitatu vibakie kwa jimbo la Mfenesini.

Mhe. Mwenyekiti, tuna bahati sana kwamba pamoja na juhudi za serikali za kutoa fedha lakini serikali hiyo hiyo inafanya juhusi na tunapata Washirika wa maendeleo wengi, kuna miradi kutoka China, kuna miradi ya Japan, ADB, na sasa tunatarajia mradi wa India.Hivi kweli bado Zanzibar kisiwa kidogo cha watu milioni moja na laki tano fedha zote na vyanzo vyote vya maji tunashindwa kupata maji angalau 90% kwa sababu hatuwezi kufika 100% lakini angalau 90% ya maji wananchi wetu wapate Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri tunaelekea uchaguzi wa 2020 katika jambo ambalo litakalowahangaisha sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa majimbo yote mwanzo maji kuliko jambo jengine. Mambo mengine tunayaweza, mengine tunasaidia lakini miradi ya maji ni mikubwa, kama serikali haikuweka umakini katika maji tutakuwa tunapata tabu sana. Tunamuomba Mhe. Waziri hili alishughulikie. Tunamuamini anaweza akalishughulikia vizuri na tunamuamini yeye na msaidizi wake Mhe. Naibu Waziri wanaweza na Katibu Mkuu wakafanya mambo ya maana sana kuelekea 2020. Tunaomba basi Mhe. Waziri utupie jicho muwone hali ya majimbo na ikiwezekana muwe na ramani ya kuangalia maeneo gani maji yanapatikana kwa wingi na maeneo gani bado wanamatatizo ya maji ili wananchi wale waweze kuona kwamba serikali yao inawasaidia katika suala la maji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sikutaka kuzungumza sana katika suala hili isipokuwa;

1. Mabomba yaliyoharibika yatengenezwe.
2. Visima vya Ras al-Khaimah wavimalize haraka.
3. Visima vipya vya Bumbwisudi kati ya 9 basi vitatu (3) vibakie kwa wananchi wa jimbo la Mfenesini.

Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Machano kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe Nadir Abdul-latif Yussuf atafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Shekhe Hamad Mattar ajitayarishe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia taarifa ya utekelezaji ya Mamlaka ya Maji ambayo iliyoletwa mbele yetu inayohusiana na taarifa zao binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitapenda kuzungumza hali halisi tuliyokuwa nayo kuhusiana na suala la maji na mengineyo. Wizara hii ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ni Wizara nzito lakini uzito wake sio kwamba kazi haziwezekani kufanyika bali ni baadhi tu ya vitu ambavyo vinavyochangiwa na watu kuweza kuzorotesha hizi kazi za muhimu katika jamii.

Tukenda kwenye suala la maji, kwanza niliwahi kuzungumza kwamba sisi tumepata bahati sana kwamba Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye anajali sana wananchi na hata kwenye masuala haya ya jamii kwenye suala la afya, maji

na umeme, anajitahidi sana kutoa fedha kwa njia yoyote muhimu zipatikane ikiwa zake yeye binafsi, ikiwa za serikali, ikiwa za kukopa, na kuweza kuorodhesha kupitia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Waziri wa Fedha ukijiuliza mabilioni mangapi hadi hivi leo Mhe. Rais keshaorodhesha au keshasaini kwamba Wizara hii ipatiwe zile fedha ziweze kufanya miundombinu ya maji, tutakuja kulala sote humu ndani bila ya kupata majibu. Ni fedha nyingi sana ambazo Mhe. Rais keshaziwachia kwa kutaka mambo haya yamalize na chambamoto hizi ziondoke kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini cha kushangaza shirika hili la ZAWA limekuwa na tabia kama ZECO. Wizara ndiyo hii hii mzigo wote wanawaachia wananchi au kuwaachia Waheshimiwa katika Majimbo. Kuna vitu ni wajibu wao kuvifanya ZAWA. Nitatoa mfano mmoja, ukienda jimboni kwangu Chaani kuna eneo Kinyasini nimeshawaeleza sana mwisho mpaka Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi nimeshamueleza sana suala lile la kununua mabomba ni lenu nyinyi ZAWA kupitia Wizara yenu sio la Mwakilishi au Mbunge. Leo mabomba ya *main line* ambayo ya maji wananchi wa jimbo langu Kinyasini hawana mnataka tununue sisi. Cha kushangaza basi mabomba yale wameleta hesabu milioni kumi na tatu na laki tano na zaidi, yanunuliwe, hayo ni mabomba ya *main line* ambayo hayapo. Kuna mbali ya kusambaza ndani ya jamii hiyo pia wanataka watuachie sisi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nathubutu kusema iko haja ya Mhe. Rais kufikiria tena kitengo hiki kukivunja na kukiunda upya kwa sababu hakifanyi kazi ya kutosha kwenye jamii ZAWA, ZECO tuko vibaya sana kwenye utekelezaji wa kuimarisha kwenye masuala ya kijamii. Mhe. Rais mimi nataka niwambie wananchi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein anatoa fedha za kutosha, anahangaika kwenye kuangalia vipi vya kutatua matatizo ya wananchi, lakini kuna watu ambao wachache tu kazi yao kuharibu haribu kila siku, hii ndiyo tunarudishana nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, kunaripoti wanazitoa humu haziridhishi sio za kweli, ripoti ya *statistics* ambazo za maji ambazo wanazo siyo za kweli. Maji Zanzibar sehemu ambazo zinapata maji ni sehemu chache sana kuliko ambazo hazina maji. Leo ukienda jimboni kwangu kuna sehemu inaitwa Kikobweni, kuna sehemu inaitwa Kandwi kabla ya Mapinduzi mpaka leo ZAWA wameshindwa kuwapelekea mabomba ya maji na hawana maji, wale watoto wakiona mfereji wanakimbia mbio wanafikiri labda silaha au kimewekwa kitu cha hatari, hawajui hata mfereji kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ZAWA haifai, hayo yalifanyika kama yamefanyika mambo mazuri basi anayafanya Mhe. Rais kupitia na watendaji wengine, lakini hawa wanazorotesha kazi. Kwa kweli inasikitisha mimi ningeomba ZAWA wenyewe wakatie mabomba yale ya Kinyasini jimboni kwangu na kazi ya kusambaza ndiyo waje watuombe sisi tufanye. Lakini leo Wizara hii imekuwa ndio namba moja kila kitu kurushia mpira viongozi wa majimbo, fanyeni fanyeni wakuleteeni bili, hicho kitu hakipendezi ni kitu ambacho siyo cha busara kabisa katika jamii. Sisi tunataka tuwape wananchi wetu wafaidike.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine tuzungumzie suala la miradi ambayo inajengwa na Serikali ya China ambayo imezungumziwa humu ndani ni Kinyasini pamoja na Chaani Tangini. Mimi niipongeze sana Serikali ya Jamhuri ya China kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar kwa kuweza kusaidia suala la maji sasa hivi. Tuangalie Wachina wamejenga matangi machache tu sasa hivi watapata maji sehemu nyingi sana. Lakini tuangalie ZAWA wenyewe walioachiliwa mabilioni ya mafedha mpaka leo kuna miundombinu inawashinda.

Mimi nikizungumzia ZAWA sizungumzii wote, najua kuna watu wazuri lakini kuna watu wambao wanaharibu vile vile, sasa wale wazuri watajijua kwamba sisi ni wazuri na wale walioharibu hii *message* ndiyo yao wao. Kwa sababu siwezi kumtaja mmoja mmoja hiyo ni kazi yao wenyewe watajijuwa kwamba mimi kazi yangu kuharibu, mimi kazi yangu kufanya vizuri. Lakini hii ni kuiangusha Serikali kwa namna nyengine viongozi wanajitahidi kutoa fedha, kuhangaika kwenda kufanya hivi lakini wakiachiwa watendaji wanaharibu na kushangaza kuna baadhi ya vitu haviko ukweli haviko ukwelini, leo jimboni kwangu ukienda asilimia sitini haina maji asilimia arubaini ndio ina maji halafu wanakuja kusema Chaani hivi na hivi tumshukuru Mwenyezi Mungu na tumpongeze Mhe. Rais kwa kuweza kuweka matangi sasa hivi ya China yake yatasaidia sana wananchi wa Jimbo la Chaani.

Lakini bado kuna tatizo Kinyasini ambalo hilo ni wajibu wao kufanya na kuna tatizo Kikobweni ambao hawana maji toka wakati huo niloutaja sasa ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja aje anijibu mabomba yale ni kazi ya nani kununua mabomba ya *main line* yetu sisi Wawakilishi au yake yeye Wizara na lini kazi hii itafanyika kwa sababu tujuwe kama nilivyoeleza kuna kazi mbili kuna kazi ya *main line* na kuna kazi ya ku *supply* ndani huko kwenye vijiji, hiyo pia bado kwa upande wa Kinyasini kwa upande wa Kikobweni hali kadhalika vipi ataweza kutatua haraka iwezekanavyo changamoto hii kuliko kuja tu hapa kujisifu sifu tumefanya hivi, tumefanya hivi wakati vitu vyengine sio kweli na hili linaangusha wananchi wanaona siye tunajisifu wakati huko nje uongo hakuna kitu baadhi ya vitu vya uongo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza mimi niwapongeze sasa kwa sababu haya masuala ya maji yamechangiwa kwa sehemu tatu kuna watu binafsi ambao wamejitolea kuchimba visima na kutia mashine hao tuwashukuru sana na tuwapongeze, lakini pia kuna Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ndio inayofanya kazi kubwa sana kuliko watu wote ndio inayoweza ku *invest* kwenye masuala haya ya maji. Lakini vile vile kuna wafadhili wengine ambao wanasaidia lakini isitoshe hatujafika mimi ningetoa ushauri wangu kwa Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein ni vyema basi akakaa na Serikali ya China miradi yote ya maji iliyobakia ikabidhi Serikali ya China ifanye kazi kwasababu ZAWA washashindwa kiukweli, ZAWA wameshindwa kwenye masuala ya maji ni vyema basi Mhe. Rais kwa ushauri wangu namuomba aikabidhi Serikali ya China kwenye miundombinu ya maji ifanye kazi yake kuliko kuja kupewa fedha yenyewe hapa kwenye taasisi kwenye Wizara matokeo yake hatufanyi chochote.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyingi hazina maji hasa hata mjini pia sehemu nyingi maji bado hiyo ni *reality* kweli hivyo ndivyo ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikizungumzia suala jengine Kandwi iliharibika mashine ya maji mashine ile mpaka hivi leo nitaomba nipate jibu wamefanya kitu gani hadi hivi leo maji hayako vizuri kuna sehemu wajua hasa hii sehemu inatakiwa mashine kubwa lakini mashine wanazoziweka ni ndogo za maji. Isitoshe mashine ikiharibika unaambiwa hakuna mashine ya *reserve* hii ZAWA ina maana gani kuwepo, kitu chochote lazima kuwe na *emergency* kiweko na *budget* ambayo ni ya

reserve kitapoharibika kitu kiwepo lakini utaambiwa mashine hamna ikatafutwe Dubai *spare part* hakuna kuna haja gani ya kuwepo hii ZAWA.

Mimi ningemuomba Mhe. Rais hii ZAWA ingevunjwa wangekabidhiwa Wachina ndio watendaji wa kweli tunawaona wamejenga matangi mazuri kazi yao iko vizuri waenda kwa wakati, lakini ningemuomba Mhe. Rais vile vile kwenye wizara hii hii suala ambalo linasikitisha jengine ukuacha hii ZAWA. ZECO hii naruka kidogo tuu miundombinu ya ZECO wanataka kuingiza lakini mimi huko siendi mimi naenda kwenye masuala ya miundombinu ZECO, ZAWA yote mtihani kwa wananchi...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir naomba umalizie una dakika mbili

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tena kwa Mhe. Rais ZECO, ZAWA ni vyema ni bora zikavunjwa zikatengeneza upya hivi kweli nguzo mbili analipishwa milioni 2,600,000/= akavute *line* hii kazi ya nani wananchi kazi yao ZECO.

Mhe. Mwenyekiti, tuko vibaya hii Wizara mimi sitaki kum-*point* mtu wala simsemi mtu vibaya lakini Wizara hii ni *automatically* ni nzito katika *department* zake ni mbaya ukiangalia Ardhi kuna mashaka, ZECO umeme kuna mashaka, Maji kuna mashaka hatujaenda huko kwenye masuala mengine Mazingira na masuala ya Nishati.

Vile vile mimi ningetoa ushauri wangu mwengine kwa Mhe. Rais basi kuna mambo magumu Wizara nzito basi hii ZECO na ZAWA bora ingetafutiwa Waziri mwengine ikashughulikia vitu hivi tu kwa sababu hii hali ni nzito sasa hivi. Leo wananchi wanatoleshwa mafedha mengi Mhe. Mwenyekiti mimi Mhe. Mwenyekiti leo sikuchangia asubuhi kwenye PAC kwasababu nilikuwa sikusoma na mimi napenda niongee kitu ambacho nakifahamu na ndio maana nikakataa kuchangia lakini kwa suala hili lipo mimi nashukuru sana na ripoti hii juu ya hivyo kwamba nishasema sana nangoja majibu naikubali kwasababu sina ugomvi na mtu wala simuonee mtu vibaya lakini tutekeleze wajibu wetu hali si nzuri nje.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Nadir Abdul-latif Mwakilishi wa Chaani kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji ni wengi katika Wizara hii au katika Ripoti hiyo sasa naomba kila mmoja atakayesimama na kuchangia ajali sana muda na kila mchangiaji wa siku ya leo kwa vile ni wengi badala ya dakika kumi na tano nitampa dakika kumi ili kila mmoja apate nafasi ya kuchangia dakika kumi. Mheshimiwa Jaku nimekuona kuhusu Utaratibu.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ningeomba kwa idhini yako tukatumia kanuni ya 147 ya kutenga kanuni kando ibara ya nne kanuni yoyote itatengwa kando kwa madhumuni yaliokusudiwa tuu kwa kutenga kando huku na sio kwa madhumuni mengine yoyote. Nia ya hii Wizara kila mtu anataka kuchangia ni Wizara inayomgusa Jimboni kwake vyenginevyo hatutowafanyia haki

wananchi wetu, tungetenga muda kama utaridhika hata saa tatu tukaridhika ili tuchangie nikuombe kwa muongozo wako, hii imegusa wananchi na wanoumia ni kina mama vijijini kwetu. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nimekufahamu kuhusu utaratibu na kanuni hiyo lakini kanuni hiyo hiyo mpaka mimi nitowe ruhusa pia kwa ajili hiyo, kwa hiyo ndio maana nikasema kwa wachangiaji ni wengi kwasabau kanuni ina dakika kumi na tano kila mchangiaji wa ripoti hii badala yake nimetoa kumi kwa kila mchangiaji ili apate nafasi ya kuchangia. Kwa hivyo tayari nimeshaikubali hiyo kwa hivyo kila mmoja atachangia kwa dakika kumi ili hao wachangiaji wengi wapate kuchangia. *(Makofi)*

Tunaendelea Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarhan atafuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Bahati Khamis Kombo ajiandae.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii lakini mimi ambacho kwa sababu wa muda ambao umekwenda nataka niwahi kuzungumza mambo machache kidogo, mimi nilikuwa nazungumza kwa suala la ZAWA kwamba katika jumla ya mipango yetu ambayo tunaipanga hapa katika Baraza letu la Wawakilishi hatukuja kukomoana, hapa tumekuja kutafuta mustakabali wa nini ambacho kina matatizo kwa wananchi wetu tuweze kukitafutia ufumbuzi na tuweze kufuata utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza tulitakiwa kufahamu utaratibu mzima wa matatizo ya maji, maji Mheshimiwa hayatoki kwa sababu ya kiwanda Mheshimiwa maji yanaletwa na Mwenyezi Mungu anaweza kuyaondosha yasiwepo na anaweza kuleta mengi yakawepo ni sawasawa na vile inaponyesha mvua kama wakati mwengine tunakosa mvua na wakati mwengine mvua zinakuwa nyingi mpaka zinaleta mafuriko.

Mhe. Mwenyekiti, Rais wetu alishatuambia katika mikutano mingi maji sasa hivi katika utafiti uliofanyika tayari katika vifaa vyetu yamepungua sana na katika vyanzo vyetu vya maji yamepungua sana na inawekana hata katika ardhi tukiachia vyanzo vya kutoa maji lakini hata katika ardhi yanaonekana maji yamepungua kwa sababu zamani maji yalikuwa yakichimbwa mita moja, mita mbili vilikuwa na visima vya kata sasa hivi visima vya kata vyenyewe havipo tena.

Kwa hivyo sasa hivi ni visima ambavyo vinachimbwa kuanzia mita ishirini kwenda mita arubaini, hamsini na kama Ras al-Khaimah katika utafiti wake amekwenda mpaka mita sabini kutafuta maji, sasa tuangalie kwamba maji yamekimbia sana katika hatua za juu maji yako chini sana. Kwa hivyo ningeomba wananchi pamoja na Wawakilishi tujue utaratibu mzima wa maji pamoja na kuweza kuyalinda maji hayo tukiachia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze kwamba maji yanahama kwa kujenga sasa hivi Zanzibar inajengwa sana, miti inakatwa, mvua zinakuwa za mashaka mashaka kwa hivyo maji yanazidi kupungua nyumba inakunywa maji kila ukijenga yanaondoka maji Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo tuangalie kwamba hata tunapojenga katika vyanzo vya maji tunayakimbiza maji sana, mimi nilikuwa nataka nitoe utaratibu wa kuweza kuangalia kwamba matatizo ya maji tusitupia kwamba ZAWA ni tatizo la maji ZAWA wana matatizo yao lakini tuweze kujua na nini

ambacho kinaweza kutusaidia kwa sababu utafiti umefanyika kwamba maji sasa hivi ni yana tabu zake, hasa kwenye vyanzo vikuu.

Mimi ningeishauri ZAWA sasa hivi kusaidia visima hivi vya Ras al-Khaimah ambavyo vimechimbwa ambavyo tayari utafiti wake umepatikana vikaweza kufanyiwa *installation* ya uhakika vikaweza kutumika ili kuweza wananchi kupata maji baada ya kutafuta miradi mikubwa ya mabilioni na trilioni kwa wakati huu kwanza tukawa tunaenda nayo upande mwengine lakini visima hivi vikatafutiwa mfuko maalum ambao kwa hakika unaweza kutusaidia kwasababu tayari miundombinu yake ipo ni *just* ni kuweka mashine na mabomba ya karibu karibu kuweza kuviunganisha.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nizungumze kwamba tatizo la maji liwe letu sote lisiwe la mmoja kwa sababu kama maji hayakuwepo ina maana tunakosa sote. Kwa hivyo ningeomba sana hili suala likatizamwa katika hatua ambayo itakuwa inaangaliwa, lakini hatua nyengine ni kutafuta ukarabati Mheshimiwa katika kwanza niisifu hiyamaoni yao kutoka katika Ripoti ya Wizara wamesema changamoto ambazo zimewakabili wamesema waziwazi Mheshimiwa kuna changamoto kama nane ambazo kwa kweli zinaonekana waziwazi kwamba moja ni upotevu wa maji kwa asilimia 30.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunayatafuta maji basi tumeshayapata lakini asilimia 30 yanapotea ningeiomba ZAWA wakachukua juhudi za makusudi katika kulitafutia ufumbuzi suala hili ili maji haya yasipotee na yaweze kutumika. Kwa hivyo ningeomba sana kwamba tusizungumze tu kwamba maji yanapotea lakini tuweze kuyafatilia kwa kina ili maji haya yasipotee.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kwamba pamoja na hayo ZAWA sasa hivi katika kipindi cha nyuma walikuwa na mapikipiki wakitembea sana katika maeneo kuangalia maeneo ya maji, vyanzo na vijijini kupita. Sasa hivi wana magari yanatumia *cost* nyingi wanunue na mapikipiki kwa ajili ya wale ambao wanatumia katika ziara zao wapate kupita ili kuangalia matatizo ambayo yanawafika. Wengine katika vijiji Mhe. Mwenyekiti, maji yanakuwa yapo lakini *sabotage* za makusudi za baadhi ya watendaji, sasa ningeomba ZAWA pamoja na kutafuta mbinu za kutafuta maji mengi lakini haya maji yaliopo kwanza yapate kutumika kwa hivyo ningeomba sana, kuna watu ambao wanafanya uharibifu katika vyanzo hivi vya maji au katika maeneo ambayo maji yapo katika ile *stopcock* ambazo zinafanya ili kutia Serikali au kuipaka matope kwamba Serikali haina maji, ningeomba sana ZAWA wawe karibu katika kutafuta masuala kama hayo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu mimi nina uhakika visima vya Ras al-Khaimah vikikarabatiwa tatizo la maji litapungua asilimia thamanini (80%) nina uhakika Mheshimiwa visima ni vingi sana viko Chambani kule kuna ukuosefu wa maji watu wanalia maji lakini pana visima pale karibu viwili au vitatu vimechimbwa vimefungwa tu hamna na wanasema pale Chambani kuna maji ya lulu pale yanaongeza nguvu za kiume na nini wanasema sana watu, kuna maji ya uhakika pale ambayo ni lulu fulani ya maji.

Mheshimiwa pia waingalie kwamba utaratibu ni huo lakini pia kama tulivyosema kwamba katika utaratibu mzima wa manunuzi wa mashine Mheshimiwa mashine zinazonunuliwa kwa sababu ZAWA walikosa pesa wakawa hawana pesa za uhakika, wananunua mashine labda naweza

kusema mkononi mkononi au mashine za tenda sasa hivi na mimi niungane na Mwenyekiti na mimi niungane na Mwenyekiti kwamba watumie *supplier* wa-*guarantee* ambaye atatoa mashine zitakazoendana na kama kutakuwa na tatizo wanatoa *guarantee* ya mwaka mmoja basi siye tutakuwa tumepiga hatua sana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naenda mbio mbio usinitizame sana kwasababu najitahiti kupapatua masuala ya maji.

Mhe. Mwenyekiti, katika masuala mengine ni kwamba suala la ukaguzi wa mara kwa mara Mheshimiwa wenzetu katika maeneo mengi hata Bara huwa wanatumia kama kila kijiji, kila eneo wanaweka mtu wao wanakuwa kama ni kujitolea kwao wanamuweka mtu wao wa kutizama hali halisi ya maji ama uharibifu ama tatizo akawa anawapigia sasa ZAWA ningewaomba baadhi ya maeneo wanayoona wana matitizo sana ya maji wakatafuta mtu akaweza kuagalia ili kuweza kuwapa ripoti ya kila siku hatua ya maji inayoendelea ama kupasuka kwa mabomba au tatizo gani ambalo limetokea.

Lakini jengine ni kwamba Mhe. Mwenyekiti...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie dakika moja.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Sawa Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba tatizo la ufungaji mita Mheshimiwa tatizo la mita bado linaongeza uharibifu wa maji, maana yake maji yanatumika ovyo kuna mtu mwengine anaweza hapo kwenye nyumba anayafungulia maji kwasababu hayana mita anaachia tu anasema huria. Kwa hivyo ningeomba pamoja na hiyo asilimia thelathini (30%) lakini na maji mengine yanakuwa yanamwaga makusudi kwa sababu hayana mita kwa hivyo ningeomba hivyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa natazama utaratibu wa zamani sasa hivi ZAWA wamefuata utaratibu wa kutia mashine katika kisima na kuunganisha moja kwa moja kusukuma maji Mheshimiwa mashine zinakufa haraka, pamoja na matatizo ambayo wanataka kuyakomboa ni lazima wawe na *storage* katika eneo la kisima la minara, lazima Mhe. Mwenyekiti mashine zinafanya kazi *overtime* kwa hivyo pale ni lazima *tank* ziwepo kuipumzisha mashine *otherwise* tutanunua mashine kila siku hata ziwe na *guarantee* zinakuwa haziwezi kuangalia.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa vyovyote vile ningeomba wabadilishe mfumo wao lazima ma *tank* yapo ya maplastiki katika maeneo ambayo ya vijijini waweze kuangalia kwamba nini ambacho kitatumika.

Lakini Mhe. Mwenyekiti watu wa zamani walikuwa na utaratibu na maji yalikuwepo tele nashukuru Mhe. Mwenyekiti dakika moja tuu....

Mhe. Mwenyekiti: Naomba umalizie Mheshimiwa

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, lazima kidogo niseme Mhe. Mwenyekiti tatizo tunatafuta maji ambayo tunachimba lazima yatoke chini Mheshimiwa Mwenyezi Mungu anatuletea maji ya mvua, watu wa zamani wengi walikuwa na mahodhi katika maeneo yao walikuwa wakikinga maji ya mvua na yakiwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba ZAWA nao wajitahiti kutafuta mbinu ya kuyavuna maji ya mvua baadha ya kutugharikisha waweze kuyatumia katika mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Suleiman Sarhan kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar atafuatiwa na Mhe. Bahati Khamis Kombo na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajiandae.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii na mimi nitowe mchango wangu mchache katika Wizara hii katika Mamlaka hii ya Maji.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi sitokuwa mchoyo wa shukrani kwa Serikali yangu ya Mapinduzi ikiongozwa na Dk. Ali Mohamed Shein kwa nia thabit ya kuona kwamba maji yanapatikana vijijini mote, lakini tu ni matatizo ambayo kuwa yamejitokeza na bado Serikali yangu inaona inafanya juhudi kubwa sana. Nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kufanya juhudi kubwa kuona kwamba watu wake wanapata maji ya kutosha kama ilivyo nia ya Chama cha Mapinduzi. Lakini pia vile vile na wale wahisani wetu ambao kuwa wanatulia misaada mbali mbali kuona kwamba maji yanapatika katika sehemu mbali mbali ya vijijini na mijini kwamba maji ni uhai.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nakwenda moja kwa moja kwenye ukurasa namba 4 katika sehemu inayosema ujenzi wa vyoo na usafi wa mazingira maskulini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niwapongeze Mamlaka ya Maji kwa kujenga vyoo katika maskuli yetu kwa kweli kuna mradi ule wa ADB wamejenga vyoo katika maskuli yetu na walianza kuweka michoro ya kujenga ma *tank* ya maji lakini hadi leo hii kama alivyosema itamalizika mwezi wa Juni lakini hadi leo hii ziko skuli ambazo kuwa hadi sasa hazijakuwa na minara ile wala ma-*tank* ya kuhifadhia maji. Hivyo kunaleta usumbufu sana wa kupatikana maji kwenye vyoo kitu ambacho kwa huo usafi hautapatikana na hayo mazingira ya skuli yatakuwa ni machafu.

Mhe. Mwenyekiti, vyoo kukosa maji ni tayari umeanza kuchafua mazingira kukosekana kwa maji katika vyoo kwa kutumia maji ambayo kuwa yanakuja siku mbili wiki nzima hapana mazingira yale yatachafuka na pale panapoishi vijana wetu kwa muda mrefu na kwamba ukitizama wengine ni walemavu hata akienda kujisaidia pale inakuwa ni shida kupata maji. Lakini kama yale matangi yaliyokusudiwa yatawekwa basi yataweza kuwasaidia hata wale wenzetu ambao wenye ulemavu, kwa sababu mlemavu anaweza kutoka darasani kutaka kwenda kupata huduma hiyo, lakini akifika kwenye choo hakuna maji, yale mazingira ya usafi yatakuwa hayapatikani. Kwa hivyo, naiomba sana Mamlaka ya Maji ule mradi kama umemaliza watafute namna yoyote ile kuweza kufanya yale matangi yaliyokusudiwa kuwekwa kwa ajili ya vyoo walivyovijenga yapatikane ili lengo likamilike. Kukosekana kwa matangi haya ya maji itakuwa ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile mimi niwapongeze watu wa *ZAWA* kwa kuona tayari matayarisho ya kisima cha Matangatuwani pale Pemba, tayari wameanza kuchukua hatua na watu wa Mgogoni, Kifundi, Kwale wanapata maji. Mimi niwapongeze sana kwa hali hii nawaomba waendeleze kwa

sababu hapa waliwaahidi wananchi, mimi mwenyewe Mwakilishi wa Konde na Mwakilishi wa Mgogoni tulichangia pale, lakini pia alipokuja Mhe. Rais katika ziara yake wananchi waliomba tatizo hili liondoke na Mhe. Waziri akaliahidi kwamba hili suala litaondoka tokea mwezi wa nane. Lakini nafurahi sana kuona sasa hivi matayarisha ni mazuri naomba wasirudi nyuma na hizo fedha waendelee kuwapokea.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya Mgogoni ni sehemu muhimu sana kwanza kwa hivi sasa kukosekana maji ni tatizo, kwa sababu ni sehemu ambayo uchumaji wa karafuu ni mkubwa sana, wageni ni wengi wanaofika pale, kwa hiyo mazingira yale kukosa maji ni tatizo. Lakini kama hiyo haitoshi ile sehemu ya shule pale kukosekana maji ni tatizo vijana pale wanaleta usumbufu kwa nyumba za jirani kila mara kwenda kuomba maji kwa ajili ya kujisaidia na kwa ajili ya huduma mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wanafunzi hawa hawa wanatoka kwenda mabondeni kutafuta maji, yale matatizo tunayosema mambo ya kudhalilishana yanaweza kutokezea. Namuomba sana Mhe. Waziri asirudi nyuma huu mkakati aliouweka kwamba kisima kiweze kupata maji, Skuli ya Mgogoni waweze kupata maji ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende kwenye suala zima la ulipaji wa fidia. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika ripoti yake hii kwamba kuna ulipaji wa fidia umefanyika, kwa kisiwa cha Pemba imeonesha Kisiwani, Kizimbani, Wara, Mvumoni, Mfikiwa, Wawi na Madungu, Mgelema, Uweleni na Minazini kwa upande wa Pemba, lakini sijaona katika kijiji cha Taifu. Kijiji cha Taifu kuna visima vingi vilivyochimbwa pale na pale pana sehemu kubwa ya maji ambayo yanapelekwa Mjini Wete kuna tenki moja kubwa sana pale. Lakini je niulize Mhe. Waziri katika uchimbaji huo ni kweli kijiji cha Taifu visima hivi havikuleta athari, ninavyoona kuna mikarafuu ambayo lazima itakuwa imeathirika. Je, wamelipwa fidia? Kama hawajalipa fidia wana mpango gani? Naomba atakapokuja anieleze kwamba je kijiji cha Taifu hakikuathirika na uchimbaji huu wa visima.

Mhe. Mwenyekiti, kijiji cha Taifu ndio sehemu maji yanayotoka yanapokuwa yanapelekwa Mjini, lakini la kushangaza wao wenyewe hawapati maji yale. Hii sio haki kabisa mimi nasema. Sio haki kabisa kuona kwamba maji yanapotoka wao wenyewe hawafaidiki wanaweza kushawishika hata kwenda kuharibu ile miundombinu, siombi wafanye hivyo lakini si vizuri tufanye vyovyote vile itakavyokuwa na wao tangi lile lililopo pale waweze kufaidika au itafutwe namna mbadala ya kuona kwamba visima vilivyokuwa havijaungwa hivi sasa viunganishwe na mabomba yaliyopo yaweze kupata maji kwa urahisi na wepesi kabisa. Haiwezekani kabisa wao maji yatoke pao halafu wao wakose maji, na hiyo shida ipo hivi sasa, maji yaliyopo yanatoka Finya nayo ni ya mgao. Naomba sana Mhe. Waziri kushirikiana na Mamlaka ya Maji ione kwamba tatizo hili lipo katika kijiji cha Taifu.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kutoa ushauri wangu katika masuala ya maji ni kwamba maji kwa kweli tunasema yako chini, lakini yamepungua. Na yamepungua kwa sababu ya kuona kuwa miti tumeikata mingi sana, hivyo vianzio vya maji vimepotea. Kwa hivyo, naomba sana kwa wananchi sote tushirikiane katika kupanda miti maeneo ambayo kuwa tumeiathiri bado hatujachelewa, tukiweza kurudisha haiba ile ya mito yetu, milima ambayo sasa hivi ukiikuta ni meupe utakuta mabonde bado yataweza kujirudi na maji yatapatikana na huu usumbufu utaweza

kupungua pamoja na kuhakikisha kwamba vile visima ambavyo kuwa vimechimbwa tunaviunganisha.

Mhe. Mwenyekiti, visima vilivyochimbwa kama hatutaviunganisha mapema vinaweza vikakosekana kabisa kabisa. Sifa ya kisima kile ili kiweze kufanya kazi ni kuchotwa yale maji, kama yatabakia vile vile unaweza kuyakuta maji yaliyokuwepo ni mengi lakini hatimae havipo. Kwa hivyo, naomba sana serikali tufanye nia ya makusudi visima vile tuviunganishe na vile ambavyo kuwa tumeviunganisha kwa kweli ni tatizo *pump* zote zina matatizo, na hii inatokana kwamba mashine hazipati kupumzika. Ushauri wa kujenga matangi ya maji ni muhimu sana, maji yapandishwe kwenye matangi na baadae mashine iweze kupumzika. Utaratibu huu utaweza kusadia mashine ambazo zitawekwa katika visima hivyo viweze kudumu kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ushauri wangu ni huo, na mchango wangu ni huo naomba sana na naunga mkono ripoti hiyo mia juu ya mia lakini Mhe. Waziri suala la kisima cha Mgogoni aendelee kukipa kipaumbele. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Bahati Khamis Kombo atafuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Ali Suleiman Ali ajiandae.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu jioni hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii ya kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Makamu wake Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa juhudi zao kubwa wanazozichukua kutuletea maendeleo wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa juhudi zake anazozichukua yeye pamoja na watendaji wake wote. Mhe. Waziri ni mchapakazi anafuata zile nyendo za Mhe. John Pombe Magufuli aliposema “hapa kazi tu”. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niendelee moja kwa moja katika ukurasa wa 4(b) ujenzi wa vyoo na usafi wa mazingira maskulini. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) kwa juhudi zao kubwa wanazozichukua kwa kupata ufadhili wakaona kwamba waendelee kuvishughulikia vyoo vya skuli kutokana na kwamba kuna mkusanyiko mkubwa wa wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, nikisema hayo ni kwamba ninalo na mimi tatizo hili katika Skuli ya Ngwachani juzi nililisemea na leo pia nalisemea tena. Namuomba Mhe. Waziri atakapopata tena wafadhili wetu kuja kutusaidia, basi naomba Skuli ya Ngwachani aikumbuke. Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza sana wafadhili wetu kwa jitihada kubwa wanazozichukua na pia namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie imani zaidi waweze kutusaidia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika ulipaji wa fidia. Hapa Mhe. Waziri katwambia kwamba katika kipindi hiki Mamlaka ya Maji imefanikiwa kulipa fidia katika maeneo yaliyoathiriwa na Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira, uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ambayo hayakuwahi kulipwa hapo awali.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile anaendelea kusema kwamba ulipaji wa fidia unaendelea katika maeneo ya Jumbi, Mtwango na Kilimani Unguja, Mialeni, Mdongoni, Kivumoni, Mzimuni, Kaalani na Zawadini kwa upande wa Pemba. Mhe. Waziri nikwambie tu kwamba katika kulipa fidia hii kijiji cha Tumbi umekisahau, kwa hivyo Mhe. Waziri nakukumbusha kwamba kwamba kijiji cha Tumbi na wao wako wananchi ambao walipata athari hii.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo jema la kuwalipa wananchi kwa sababu sisi wawakilishi wa majimbo wanatupa maelezo makubwa sana kwamba wao wamesahauliwa kabisa kulipwa fidia zao. Lakini tu nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuliona hili kwamba wakati wowote wananchi hawa watalipwa fidia zao. Naamini leo wananchi wa Zawadini wakilisikia hili kwamba tayari wakati wowote wanaweza wakalipwa fidia zao, basi watafurahi na naamini watakupongeza sana Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika ukurasa wa 5, programu ya usimamizi wa maji vijijini. Katika programu hii kuna miradi mitatu ya uchimbaji wa visima kama ifuatavyo.

Mradi wa Uchimbaji wa Visima vya Ras al-Khaimah. Mhe. Mwenyekiti, mimi naendelea kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa sababu juhudi zake kubwa tunaziona na watu wamesema mti hawendi ila kwa nyenzo. Tunaamini kwamba Mhe. Waziri yeye ana hamu sana ya kufanya kazi yake na kumaliza kwa haraka, lakini zile nyenzo hana za kufanyia kazi. Hapa naiomba serikali itenge fedha maalum ili viweze kumaliziwa visima hivi vya Ras al-Khaimah, ili Mhe. Waziri tuendelee kumpa majukumu mengine na suala hili la visima vya Ras al-Khaimah limalizike. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niendelee kidogo mbele dakika zangu ni tatu kama unavyozijua.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 6 hapa pana viambatanisho (a) na (b) ya ripoti hii. Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuipongeza sana serikali kwa kuviendeleza visima hivi vya Ras al-Khaimah bila ya kuona kwamba lazima waje wale wale waliovianza ndio wamalize. Hapa wamefanya jambo kubwa sana na tunaamini kwamba visima hivi vitamalizika kwa uharaka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono ripoti hii mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Bahati Khamis Kombo kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub, akifuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) na Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) ajiandae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi bila ya kupoteza muda nichukue fursa hii kwanza kwa dhati kabisa kumshukuru Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuwajali wananchi wa visiwa hivi vya Unguja na Pemba katika huduma za jamii. Sisi sote mashahidi elimu kuona umuhimu wake baada ya watoto wa wanyonge kuteseka kuwa elimu inalipiwa akaondosha gharama za maskuli katika kipindi chake cha mwanzo cha miaka mitano iliyopita. Tumeshuhudia kanunua meli katika sekta ya usafiri kwa

kuwajali wananchi wa Pemba, tumeangalia katika sekta ya afya nini anafanya Mhe. Rais. Sijipendekezi kama nataka Naibu Waziri wala Uwaziri aah, *Waama Binighmati Rabika Fahadith* na neema zisimulie. Narudia tena sijipendekezi kwake kuwa nataka Naibu Waziri wala Uwaziri aah aliyoyafanya tumeyaona. Sekta ya afya nasema tena hata saa tisa za usiku nikaamshwa Dkt. Ali Mohamed Shein kafanya nini katika sekta ya afya, jawabu sipepesi macho amefanya kazi kubwa katika sekta ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niungane na Mwenyekiti Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kumpongeza Mhe. Waziri. Mhe. Waziri jitihada anazozifanya tunaziona, lakini kuna baadhi ya watendaji wako wanakurudisha nyuma na hii hali ukiiona huruma itakuja kuharibia. Kazi unayoifanya tunaiona lakini baadhi ya watendaji wako wanakurudisha nyuma. Sina mashaka na utendaji wako.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii tena kumpongeza Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji Bwana Mustafa Ali Garu. Mhe. Waziri kabla hujawa waziri hiki kitengo cha *ZAWA* ninakielewa nimeshafanya kazi nacho sana, na ukienda pale historia yangu utaikuta. Kuna mafundi kama fundi Haji Said sasa hivi yuko Uingereza yupo likizo, huyu kijana anapiga kazi bila ya kujali mvua wala jua, fundi Haji Said. Lakini kuna Mkurugenzi Maulid na yeye nimpongeze kwa dhati kabisa, kuna fundi mkuu pale Njuma Mhe. Waziri usishangae hawa watu nawajua nimeshafanya nao kazi kabla hujawa waziri, kuna wengi kuna fundi Rashid lakini muda na kazi wanazozifanya ni ngumu mno lakini watafanya nini uwezo ni mdogo, hata tungewapigia kelele hapa na niipongeze serikali kwa kuweka msaada huu peke yake kuujadili kwa kujali na kuwafikiria wananchi. Suala la maji kila mtu limemgusa hata katika Suratul *Anbiyai* aya ya 30 *Wajaalna Minal-mai kulishaiin*. Nini maana yake? Tumejaalia kila kitu kinapatikana kutokana na maji.

Mhe. Mwenyekiti, huwezi kulala na mama bila ya kuwa na maji, umeme unaweza kuzima ukawasha kibatali, lakini maji ndio *engine* ya kila kitu. Gari inataka maji, ndege inataka maji, buku anataka maji, panya anataka maji, maji huwezi kutoa *definition* yake, *definition* chungu nzima za maji, hata kwenye kur-ani imetajwa Suratul *Anbiyai* aya ya 30 kama sikosei. Sasa hapa tutapiga kelele kwamba serikali iongeze nguvu, hawa Wakurugenzi tutawalaumu bure huku juu kazi wanayoifanya mimi naiona. Mimi haifiki wiki mbili lazima nikasalimie pale Mwenyezi Mungu akinipa uhai, ndege anahitaji maji haya maji hatuwezi kutoa *definition* zake sera ya maji ni kubwa sana. Serikali hapa ijipange lakini naamini hivyo hivyo nimefatilia sana hotuba ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein juzi alikuwa anafungua Msikiti Chaani Bandamaji akazungumza suala la maji. Tulikuwa nae siku moja katika Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nikalia sana suala la maji Michamvi nililia sana mimi. Nikamuuliza hata yale maji Mhe. Rais yaliyotiliwa udhu unajua yametokea wapi, alifiliwa kule ndugu yake au jamaa yake Michamvi.

Mhe. Mwenyekiti, watoto Michamvi wanakosa elimu sasa hivi kwa kusaka maji, watayapata wapi maji na wanaoteseka ni akina mama hao ndio waathirika wakubwa, na ilani ya Chama cha Mapinduzi iliahidi kwa wananchi. Naamini muda upo na Mhe. Rais hili naamini linamkera ndani ya nafsi yake nishamsikia si mara moja wa mara mbili wala si mara tatu, kwa hiyo naamini hatua zitafanyika huko tumeona jitihada alizokuwa akizifanya. Lakini haya maji ni msingi wa binadamu, mimi Mwenyekiti hakuna kitu kinachoninyima usingizi hata Mhe. Hamza Hassan Juma hapa kalitetea.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Mradi wa Maji ya chumvi nimepoteza pesa mimi Mamlaka ya Maji waulizeni niko tayari kuja kuadhibiwa humu ndani mimi kama nasema uongo. Nimeambiwa miezi mitatu tu au sita huu mwaka wa tatu waziri ulikuwa huna nia hata ya kupata uwaziri. Miaka mitatu nimetia pesa pale ndio sukari huwezi kutia kwenye maji ya chumvi ukapata maji matamu ndio yaliyonikuta mimi. Waulizeni watendaji niko tayari kuja kuadhibiwa kama sijapoteza pesa katika Mradi wa Maji ya Chumvi. Leo wananchi wa Michamvi katika watu wanaotia huruma ni wale hali hairidhishi kina mama wanateseka Michamvi, serikali imefanya mambo mengi mazuri. Niiombe serikali iidhinishe pesa kwa watu wetu wa Michamvi tumeshuhudia mambo chungu nzima yamefanyika mazuri. Mhe. Mwenyekiti, watoto wanashindwa kupata elimu, watoto wanashindwa maji wakayatafute wapi, chai inakuwa ufikirie maana yake, huu mtihani mkubwa kweli maana yake isije ikafika pahali nikaja nikataka kulia nikaonekana kama nafanya uchepe humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, nikuombe sana Mhe. Waziri hata hivi sasa nataka ile *hansard* Mhe. Naibu Waziri ukaifanyie kazi umeniahidi jioni hii yatafika maji, hii hapa *hansard* yako. Naomba kuisoma Mhe. Mwenyekiti.

"Mhe. Naibu Spika, maji ya dharura tutakuwa tunayapeleka na tutaendelea kupeleka sasa nimwambie kwamba tukitoka hapa tuonane kwa sababu tunaweza tukapeleka akaja akasema hayajapelekwa. Tutawasiliana naye kusudi ahakikishe kwamba tunapeleka maji. Leo hii tokea tarehe 9/10/2017 hii *hansard*, hakuna dalili, nimempa namba ya Naibu Waziri, nimempa namba ya Sheha ananambia leo jua halitui lakini labda jua halijatua. Hakuna dalili ya maji wananchi wale wanapelekwa maji kule Mwezi wa Ramadhani mpaka Ramadhani na wakati mwengine hata huo Mwezi wa Ramadhani hayapelekwi inabidi wananchi wale wa Michamvi waishi Ramadhani hadi Ramadhani kwa maji?

Mhe. Mwenyekiti, uongozi ni dhamana na tunakwenda kuulizwa siku ya siku. Mimi watu wa Michamvi wamenituma nije niseme matatizo yao itafika watakwenda kunambia tulichokutuma Baraza la Wawakilishi hujakizungumza mimi ni mwakilishi wa kuja kusema matatizo yao sio sehemu ya kuwatumikia wananchi tatizo kubwa na kuna mahoteli ya wawekezaji kule. Mimi niiombe sana serikali kwa jicho la huruma, kwa jicho la imani wafikirie suala hili wanaoteseka ni akinamama ni mtihani mzito.

Mhe. Naibu Waziri nimuombe maji hayajafika Michamvi hiyo gari kama alitaka kupeleka tatu au nne kwa wiki lakini bado hakuna. Nimuombe kabla ya majumuisho yake hapa, nitakuja kuinuka mara mbili au tatu hii ni kauli yake na ameizungumza katika chombo kizito itakuja kumsababisha hata aje ajiuzulu huko mbele. Nimuombe uheshimu kauli yake vyenginevyo huko mbele itakuja kusababisha aje ajiuzulu. Anaona umuhimu wa maji hata yeye Naibu Waziri sasa hivi anakunywa maji kwa kuona umuhimu wake, ndio umuhimu wa maji tusingezaliwa sisi bila ya maji.

Mhe. Mwenyekiti, niombe nimalizie hapo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na mimi kuchangia kidogo taarifa ya utekelezaji kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii za makusudi kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na watendaji wote wa *ZAWA*, tunaamini bila ya maji huwezi kuishi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba leo sina mengi sana isipokuwa nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati kwa taarifa yao nzuri na kusema kwamba kubwa wanalolitaka au tunaloliomba serikali itoe fedha ili Mamlaka ya Maji ifanye kazi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kidogo nitatoa historia ndogo, nasema Mamlaka ya Maji imepata misaada mingi sana, sioni wivu kwa sababu misaada ya maendeleo, lakini mafanikio yamekuwa madogo sana huko tunakotoka. Kwa hivyo, tunajenga hofu wakati mwengine unatoa fedha hizi mabilioni yafanye kazi fulani lakini mahitaji yake yanakuwa hayapatikani hiyo ni hatari. Sina shaka nao nina mashaka kidogo kutokana labda kuna matatizo ya hapa na pale naomba wayaondoe ili wafanye kazi ipasavyo mahitaji haya ambayo tunahitaji kila jimbo katika nchi hii yapatikane.

Mhe. Mwenyekiti, mimi huwa ninakasirika sana wakati mwengine kuangalia uwezo wa kuboresha maji kwa eneo la mjini tu, yaani Manispaa ya Mjini. Sina wivu lakini nasema hivyo ndivyo ilivyo, kumbe sivyo ilivyo kwa upande mwengine. Mheshimiwa asilimia kubwa ya Wazanzibari wenye shida vijijini, wenye shida Magharibi 'A' na 'B' huko maji hakuna kabisa. Mheshimiwa maeneo haya ndio rasilimali ya maji inakotoka lakini la kusikitisha maji hakuna, maji shida, sijui kuna kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwa ufupi kabisa ukurasa wa 14 tumeambiwa kwamba idadi ya vianzio vya maji viliopo vinavyotumika na *ZAWA* mwaka 2016/2017, eneo, Unguja chemchem mbili, mapango sita, visima vilivyounganishwa 129, visima visivyounganishwa 118. Pemba chemchem mbili, mapango hawana, visima vilivyounganishwa 105, visima visivyounganishwa 59; ukichukua visima vilivyounganishwa vyote Unguja na Pemba 234, visima visivyounganishwa Unguja na Pemba 177.

Mhe. Mwenyekiti, tathmini hii ni hatari tutasema vianzio vya maji havipo visima vishachimbwa hivyo Ras al Khaimah na wengineo lakini vimekaa hadi leo havijaunganishwa. Kwa hivyo, mimi ningeomba Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kutafuta visima vipya 29 vya Ras al-Khaimah vinavyotaka kuchimbwa tuviunganishe hivi kwanza wananchi wetu wapate maji. Naamini uhaba wa maji au upungufu wa maji umo, lakini la kushangaza kuna visiwa hivi 177 mimi kwangu Jimbo la Kijitoupele nina visima vitano, visima hivi vimo katika mradi ambao umo katika matarajio ya kuunganishwa hapo baadae. Lakini Mheshimiwa niseme kwa dhati kabisa visima hivi navyo kama vingeunganishwa katika maeneo hayo ile historia ya kuondoa shida ya maji katika Jimbo la Kijitoupele na majirani ingeondoka.

Kwa mfano, huyu jirani Mhe. Mwenyekiti yule pale Mhe. Mwanaasha Khamis Juma ana kisima cha Ras al-Khaimah Tomondo Kwa Muhindi, hii Kwa Muhindi ndio jina lake nisijeambiwa Muhindi jina aa, hapo ndio asili yake. Kisima hiki kiko mbioni na sasa hivi naona wenzetu wako mbioni kukifanyia matengenezo *inshaallah* kikikamilika maji yake tutapata sehemu zote mbili, naamini kule Kwarara Maduka Sita na huku kwengine watapata kwa sababu maji ni rizki ya kila

mtu sina pingamizi. Hiki kinaendela lakini hivi vyengine Fuoni-Kijitoupele, Kwarara Kandahar huko wanatumia maji ya visima bwana, maji hakuna hadi hii leo tunapozungumza hapa na siku za mvua maeneo haya ndio huwa hatarishi kwa kipindupindu.

Kwa hivyo, niiombe serikali hili liangaliwe Kwarara, Kandahar kisima kipo kimekaa chengine unakuja Kijitoupele Kwarara, *The Home Academic Excellence* yaani Skuli ya *Primary* hiyo na hapo kipo kisima kimekaa, Fuoni Kijitoupele, Mashine ya Maji kipo kimekaa, unakuja zako Meli Nne Uzi, Magirisi kimekaa kizuri, lakini hiki cha Magirisi nitakisemea kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, leo naipongeza *ZAWA*, siku zote naipongeza kwa sababu bila ya wao hatupati maji, lakini leo sijui kulikuwa na taarifa hii kama nitakuja kusema au vipi, leo Mheshimiwa nawapongeza kwa dhati *taskforce* nzima imetoka *ZAWA* wamekwenda Magirisi kuangalia kisima kile, mpaka wananchi wangu wakanipigia simu tunaona gari ya *ZAWA* na wageni wa *ZAWA* wapo hapa. Lakini nasikitika mimi mwenyeji wangenipigia tungeshauriana vizuri. Kwa hivyo, kisima kile cha Magirisi Mheshimiwa naahidi kama kitafanyiwa kazi kitaondoa tatizo la maji katika jimbo zimo au asilimia 80 ya jimbo itakuwa hakuna tatizo la maji kuanzia Meli Nne huko, Meli Nne Uzi, Tomondo, Kwarara mpaka Kijitoupele. Kwa hivyo, niwaombe sana wenzetu *ZAWA* nawashukuru tuwasaidie hizi fedha zilizoombwa na kamati kupitia wizara ni ushauri mzuri fedha zitolewe ili tuviunganishe visima vyetu hivi. *(Makofi)*

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka niongezee hapa hapa pana hospitali kubwa leo pia namshukuru Mhe. Waziri wa Afya na Naibu Waziri wake na Mkurugenzi na *taskforce* yake nao, walikwenda hapo Magirisi ambapo pana hospitali kubwa tunaitegemea ikimalizika wananchi wetu wote pale watapata huduma mana watazalishwa pale, watoto, watu wazima watapata huduma kile kisima kinahitajika muhimu sana.

Kwa hivyo, mimi naomba ushauri maalum kisima hiki kipewe kipaumbele kwa sababu hospitali tunaamini ndani ya muda mfupi na mna wahisani humu humu Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakili kajikubalisha kuutwika mzigo huo na yeye atasaidia hospitali hiyo ili tuikamilisha haraka, na mimi madhali kanipa changamoto hiyo mimi na mbunge tutajitolea vizuri zaidi kuisaidia Wizara ya Afya, kwa sababu tunawafanyia wananchi wetu hasa kinamama , watoto na wazee.

Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya hayo machache naiomba tena *ZAWA* kisima cha Magirisi na vyengine nilivyovitaja lakini Magirisi tukifanyie kazi ya ziada ili kinamama wetu ikimalizika hospitali ile wapate maji saa 24 wapate huduma kwa salama bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja naiomba serikali fedha zitolewe wenzetu wafanye kazi manung'uniko yaondoke. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali kwa mchango wako lakini pia nikushukuru kwa kuona kuna kisima kiko katika maeneo ya Jimbo la Chukwani, natumai Mhe. Waziri amekusikia. Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite Mhe. Mohamed Said Mohamed akifuatiwa na Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakili na Mhe. Suleiman Makame Ali ajiandae.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana kwa imani yako lakini ndani ya sakafu ya moyo wangu. Lakini kubwa nimshukuru Mwenyezi Mungu na nimuombe sana magharibi hii anijaalie nisiwe na tambo, kiburi, wala jazba nikichangia hotuba hii.
Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme tu, nimpongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, lakini na watendaji wote wa *ZAWA*. Kwa nini niseme niwapongeze? Mhe. Waziri yeye ni mtu wa pili baada ya Mwalimu kuona, nikizungumza mwalimu ni Mwalimu Haroun Ali Suleiman sio maalim, mwalimu kuona haja ya hoja yangu ambayo nimeitoa kuleta sheria hizi Barazani. Sasa nataka nimpongeze kwa nia safi kabisa, ingawaje kuna kasoro ndogo ndogo zinaweza kujitokeza za kisheria na hizo lazima huwa tunaweza kusema.

Mhe. Mwenyekiti, wahenga wanasema: "Nazi ina macho matatu lakini haioni". Sasa nini maana yake, nataka kusema nyumba yetu tunayojenga hii ni moja kukumbushana, kutanabahishana lakini na mambo mengine yote ya kuweka wazi lazima tuambizane, lazima tushituane ili kukidhi haja ya sheria. Sheria tunazozitunga sisi hapa ni nyingi sana, kipindi hiki tu cha miaka miwili tumeshatunga sheria 20, leo tumeshapewa nyengine ya 21 tunakuja kwenye kipindi kijacho lakini utekelezaji wake unakuwa mgumu. Sasa tukiwa hatukumbushi tutaendelea kuziweka kwenye makabati lakini tukubaliane tuweze kukumbushana pale linapotokea kosa tukubaliane tuzirekebishe.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye namba 5 imeelezewa miradi mingi sana hapa ya *JICA*, *ADB* na kila kitu, mingi sana na tunawapongeza sana wote ambao wametusaidia, lakini maji bado tatizo. Wananchi hawataki kusikia hata kidogo kuna miradi mingi wananchi wanataka kusikia kuna maji hawataki kusikia miradi hawatufahamu kabisa, lakini penye nia safi na njia ipo Mhe. Waziri akaze buti tutafika.

Jengine tumesema tumekwenda kwenye *pilot area*. *Pilot area* hii ya Makadara, utafiti wangu mdogo tumefanikiwa asilimia mia moja katika ufungaji wa mita, lakini hatukufanikiwa katika ukusanyaji wa mapato, hatukufanikiwa kwa vipi, maji yanatoka kama yanakuwa *seasonable*, ukija upepo yanapatikana, upepo haukuja hayapatikani hayakidhi haja. Sasa lengo letu ni kuona wananchi hawa wanapata maji lakini tujitayarishe *pilot area* iliyokuwa nzuri tuone.

Niliwahi kushauri hebu tuondoke twende kila jimbo kwa pesa hizi tunazozipata kwa miezi mitatu, tuhakikishe kila jimbo limetoka maji, tunaondoka baada ya miezi mitatu tunakwenda katika jimbo jengine, baada ya miezi mitatu tunakwenda jimbo jengine, mwaka mmoja tutakuwa na majimbo manne tumeshapata maji yote ya uhakika na hiyo ndio itakuwa hatua nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, kazi za kawaida ambazo zimezungumzwa hapa nimeziona kazi nyingi sana ambazo mamlaka yenyewe imekiri. Moja umuhimu wa kulipa kwenda kuwashajihisha wananchi, mimi nikubaliane nao. Kwa sababu lazima tutoe elimu hii na wananchi walipe kodi ili tuweze kuwahudumia vizuri, wanapolipa kodi nzuri mashine zitapatikana na vitendea kazi vingi vitaweza kupatikana. Lakini jambo moja tu ambapo tunaweza tukenda tukawaambia wananchi hawatusikii tukiwaambia lipa kodi wakati wao maji hawayapati. Tujitahidi kadiri ya uwezo wetu tubuni basi jinsi gani maji haya yanaweza kupatikana na wananchi wetu wanaweza kufaidika. Zimetajwa sehemu nyingi na hii nataka Mhe. Waziri aje aniambie elimu hii tunayoitoa kila

Jumanne au Alhamisi tunakuwa na katakata, tukikatakata tumefaidika vipi. Je, umuhimu wa elimu ile unapatikana wa katakata au watu hawatishiki, hebu tuone mafanikio yake yako wapi.

Jengine anasema katika ukurasa wa 8 ukusanyaji wa mapato. Ukusanyaji wa mapato hata Mhe. Mwenyekiti wa Kamati alilipigia kelele kwenye ripoti yake na katika mwaka mmoja 2014 *hansard* ninayo Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yule yule alisema hapa mamlaka hii sasa kwa watu wa kawaida haifai na waweze kupewa majeshi. Lakini leo mwenyekiti huyu huyu anasema hapa hakubaliani na makusanyo yaliyopatikana. Mamlaka hii ilikusudia kukusanya 5.1 bilioni lakini bahati mbaya sana imekusanya 2.7 bilioni kwa asilimia 53. Sasa ukienda kitu asilimia 53 hapo hapana kitu.

Mimi nataka Mhe. Waziri anapokuja hebu aniambie *operation coast* ni shilingi ngapi kwa mwezi, lakini vile vile aniambie *revenue* zake kwa mwezi ni shilingi ngapi ili tuweze kuona haja sasa ya wananchi kukishauri chombo hiki muhimu sana cha kuleta maji. Mimi niwapongeze kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya, lakini wamesema kwenye ukurasa wa 8 mafanikio yaliyopatikana kuwasomesha nje, wafanyakazi niwapongeze sana kwa kazi kubwa ambayo wameweza kuifanya.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 9 matengenezo ya mabomba. Utafiti mdogo sana ambapo maji mengi yanapotea kuona mabomba yetu chakavu, miundombinu yetu chakavu. Sasa tufanye basi tuone kwa nini maji yanapotea, wamefanya uchunguzi huo? Kama mabomba chakavu kwa nini tusiende hatua baada ya hatua.

Jengine anasema marekebisho ya umeme. Niwapongezeni sana kwa kazi kubwa ambayo wameifanya na jitihada kubwa ambayo wanaitekeleza. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua kidogo tu deni la umeme la *ZECO* shilingi ngapi ambalo mamlaka inadaiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona unanitizama lakini na mimi nakwenda mbio kweli kweli, nije matengenezo ya *pump*. Hivi karibuni tu nilipata kadhia kubwa sana kama mwezi mmoja na nusu, bahati nzuri sana Mjumbe wa Kamati, Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil alishuhudia jimbo la Mpendae likiwa na kadhia kubwa sana ya maji, lakini nilijitahidi kwenda mbio nyingi sana, nilimpigia Afisa wangu wa Wilaya Njuma mfanyakazi mzuri sana, Mkurugenzi wa Ufundi, lakini wakati nawaambia tunafanya nini njia mbadala wakati hatujapata maji. Mkurugenzi wa ufundi ananijibu, anasema labda mpigie Mkurugenzi Mkuu yeye alipewa dhamana gani, dhamana yake alipewa kibahati mbaya. Lazima tuwe na njia mbadala ya kuinua wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye changamoto nyingi ambazo mamlaka hii imekumbana nazo. Mimi nakubaliana nao...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Said Mohamed una dakika moja naomba umalizie.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na nitaendelea nitaimaliza yote. Changamoto zinazokubaliana nao hebu serikali iangalie kuipa pesa hizi haraka itoe kwenye mfuko mkuu kwa sababu *collection* imeshindikana tuone serikali iipe tuwape wataalamu vifaa vya kufanyia kazi halafu tuwaulize. Mlitaka hichi na hichi hebu tuambieni sasa

tupe maji kwa wapi wananchi wapate maji kwa wapi hapo tutakuwa na kitu cha kusema. Lakini ikiwa wataalamu hawa hatutowapa *tools* hatuwezi kwenda.

Lakini niseme tu Mhe. Mwenyekiti, kelele zinasaidia tulipiga kelele lakini tumegaiwa maafisa katika wilaya tunafanya nao kazi vizuri sana na niipongeze sana mamlaka kwa kazi kubwa ambayo wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru wewe lakini niwapongeze watendaji pamoja na Mhe. Waziri nimwambie *big up*.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ahmada Yahya atafuatia na Mhe. Suleiman Makame na Mhe. Nassor Salim ajiandae.

Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa jioni ya leo kunipatia nafasi ndogo hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ambayo iko mbele yetu.

Awali ya yote mimi niko wazi kwa kuipongeza wizara hii kuwa inafanya kazi vizuri. Mbali na changamoto ndogo ndogo lakini lazima tukiri Baraza hili hali ya upatikanaji maji kwa sasa sio ile ya zamani. Kwa hiyo, serikali kupitia *ZAWA* inafanyakazi nzuri na changamoto ndogo ndogo haya ni mambo ya kawaida. Lakini kazi nzuri inafanywa. Sisi wengine ni wadau sana wa huduma hii kwa *investment* mbali mbali lakini tukiangalia kwa miaka mitano ya nyumba na miaka sasa hivi iko tofauti kubwa sana. Changamoto hazitoacha na ndio safari yenyewe.

Nikija katika nchango wangu ni kwamba Mhe. Mwenyekiti, kuna matatizo ambayo yanotokezea yanaweza kuepukwa naishauri wizara hii tuachane na mfumo wa kizamani wa *Business as usually* kuweko mpango mahususi kwa ongeza kifaa ndani ya mashine ya maji. Hii itasaidia umeme unapopanda na kushuka Mhe. Waziri na timu yake ya *ZAWA* na watalamu wake waweke kifaa kinachoitwa *stabilizer* hii itasaidia kuokoa fedha za serikali, mfumo huu unatumika hata majumbani kwetu vifaa vikizidi vitano, sita, saba inabidi ujiokoe kutokana na umeme kupanda na kushuka. Kwa hivyo, namshauri sana Waziri Salama awe na timu na afanye *pilot* japo mashine 6 kwanza kwa hatua ya awali aangalie namna wakati wa kupanda kwa umeme na kushuka nadhani tutapata matokeo mazuri.

Mimi naamini tukifanya *calculation* ya kununu *stabilizer* ukaweka kwenye *pump* za mashine basi harasa itakayopatikana au faida itakayopatikana ni kubwa zaidi kuliko ile pump yenyewe ikawa ime *bust*. Namshukuru sana Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae kwamba tatizo alivyoliona ilikuwa ni *pump*. Sasa kila mara *pump* imeungua tujenge utamaduni sasa hivi kwenye vituo vyetu kuweka *stabilizer* ili kuokoa hali hii.

Jengine naunga mkono sana hii hali ya *pump* kuweko na utaratibu maalum *ZAWA* wawe na *agency* ambazo wao ndio watakuwa na jukumu la kuhakikisha *pump* zile muda wote zipo na wao ndio watakuwa na mamlaka ya kuingia *contract* na hao *supply* wakubwa *overseas*. Kwa hiyo, *pump* zile zitakuwa zina *guarantee* tuachane na mfumo ukiungua ndio imeingua.

Nchi nyingi duniani wakati zinapouza vifaa kama hivi ghali vya *technician* basi kunakuwa na kitu kinaitwa *guarantee.* Inawezekana *pump* ndani ya mwaka ikaungua wakaja wakala wahusika

pump ile ikabadilishwa ikatiwa *pump* nyengine. Kwa hiyo, fedha za serikali pale itakuwa imelindwa kuliko huu mfano kwamba imeungua tuagize nyengine. Tubadilike kidogo katika hali ya utendaji.

Katika *point* nyengine ninayokuja Mheshimiwa ni kwamba mambo ya asili ya zamani si mabaya kuyafata. Zamani maji yalikuwa yanatiwa dawa kwa hiyo ningeomba sana utaratibu ule uendelee kudumishwa kusudi unaokoa mambo mengi, unaokoa afya zetu, unaokoa vimelea njiani vinakufa na maji yanakuwa yanauhakika katika ule utaratibu tunaotumia maji safi na salama.

Kwa hiyo, ili yawe salama kuweko mpango tena kifungu maalum ambacho kitasaidia kununua dawa za vidonge zitiwe katika mashine zisambae katika mabomba kusudi tuwe na usalama wa maji tunayokunywa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi silaumu hata kidogo *ZAWA* inafanyakazi nzuri tena sana. Naiomba serikali izidishie uwezo zana na nyenzo na utaalamu nimesikia kwenye ripoti yao kuna watu wako masomoni ili waweze kuja kumudu shirika hili au taasisi hii muhimu kwa binaadamu na si binaadamu tu kwa kumbe chochote. Mimi nasema wizara hii inafanyakazi nzuri kupitia *ZAWA* nao wanajitahidi na upatikanaji wa maji kwa miaka ya nyuma si ya miaka hii hapa.

Kwa hivyo, basi mimi naikubali tena naikubali hasa ripoti yao kwa asilimia mia moja. Wapewe uwezo wafanye kazi na wao wabadilike ili nchi yetu iweze kusonga mbele. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ahmada Yahya kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali atafuatiwa na Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira).

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya utekelezaji wa Mamalaka ya Maji Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuchangia kwanza niende kwenye ilani. Mhe. Mwenyekiti, hupenda sana kusimama na ilani cha Chama cha Mapinduzi chama dume, chama imara kwa sababu ndio tunayoitekeza na ndiyo inayokubalika.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 177(b) kazi ya ujenzi wa matangi ya maji ya Ndagoni lita milioni moja lita milioni moja Vikunguni, lita laki tatu Vitongoji Alkhamis Cap, lita laki tatu Kampuni Bahanasa lita laki moja. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ninaposimama na ilani kwamba ndio tunayoitekeleza hii ilani ya Chama cha Mapinduzi na mimi kila siku husema kwamba aliekuwa anaona tabu kutekeleza ilani ya CCM basi aondoke atupishe, kwa sababu hawezi kufanya kazi ambayo kwamba ameidhamiria. Kwa hiyo, kila anaeshindwa kutelekeza ilani hii ya Chama cha Mapinduzi aondoke njia nyeupe.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye masuala ya maji kule Ndagoni. Mhe. Mwenyekiti, kuna tangi hili lililokuweko Gombani lina lita milioni moja Mhe. Suleiman Sarahan amesema kwamba maji yameadimika. Nakubali baadhi ya sehemu nyengine maji hafifu lakini kuna Mhe. Mwenyekiti, maji yapo ya kutosha baadhi ya maeneo Mhe. Mwenyekiti, mfano kama tangi lile lililokuweko

Gombani lililotakikana lipeleka maji Vitondooni, Birikau, Kijangwani, Wesha, Mshangama, Chaoni katika jimbo langu. Mhe. Mwenyekiti wananchi wale maji hawapati tena tangi lile hujaa mpaka maji yakamwagika.

Lakini cha kushangaza maji hayafiki Mhe. Mwenyekiti, tatizo nini Mheshimiwa watu wanahangaika na Mhe. Jaku Hashim Ayoub amesema hapa mpaka akakaribia kutoa aya na ametoa zile aya. Mhe. Mwenyekiti, bila ya maji hapawi kitu. Mhe. Mwenyekiti kukosa maji siku moja tu hapa ikawa kama kuna kikao cha Baraza basi kama tutakosa maji siku moja tu hapa haji mtu humu ndani. Kwa sababu haiwezekani kama mtu amelala usiku wa kucha halafu akaja hapa ikawa bila ya kukoga na kufanya mambo mengine Mhe. Mwenyekiti, maji ni muhimu sana kwa kila kiumbe hai.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika hotuba ya Mhe. Rais katika ufunguzi wa Baraza la Wawakilishi hili tunaloendelea nalo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako nisome kidogo au kunukuu kidogo alisema, 'katika kipindi cha miaka mitano ijayo serikali itaendelea kuimairisha usambazaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi kutoka asilimia 87 mwaka 2015 hadi asilimia 97 ifikapo mwaka 2020 kwa mijini na kutoka asilimia 70 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 85 kwa vijijini ifikapo mwaka 2020'.

Mhe. Mwenyekiti, kilichobakia hapa ni kumuunga mkono Mhe. Rais tukafanya kwa bidii Mamlaka ya Maji wakawa wanajuhudi alau kwamba ikifika ile 2020 hii asilimia 85 iliyowekwa iwe asilimia 100 na uwezekano huu upo. Kwa sababu kamati wamemuomba Mhe. Rais kwamba iongozewe Mamlaka ya Maji shilingi milioni nne. Mimi nina imani kubwa sana kwamba Mhe. Rais anavyowajali wananchi tumepata mafanikio makubwa. Ilikuwa tuna tatizo la usafiri hapa lakini tumeona usafiri ule pale umepatikana.

Kwa hiyo, mimi nina imani kwa Mhe. Rais anapowajali wananchi wake basi bilioni nne hizi ataziizinisha na kuweza kupatikana maji mjini na vijijini. Hasa kilichobakia ni kumuunga nguvu tukamuunga mkono wale waliopewa mamlaka ya kufanya hivyo basi wahakikishe kwamba maji yanafika sehemu zote.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye ripoti hii ukurasa wa 23 kwamba kuna gharama hapa zimelipwa, nimemuuliza Mhe. Waziri hapo nje gharama zile zililipwa kwa ajili gani. Kuna gharama zililipwa kama fidia Mhe. Mwenyekiti. Sasa kilichobakia ni kwamba maji yatolewe ikiwa kuna matatizo madogo madogo Mhe. Mwenyekiti, hayaepukiki. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba waliopewa dhamana hii basi zile dhamana wazichukuwe ili kuondosha usumbufu wanaohangaika ni kina mama, kina mama wanapata tabu usiku hawalali hawana raha kwa kufatilia masuala haya ya maji.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ikiwa kama kina mama wanahangaika kwa kufuata maji baba atakuwaje? Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana kuhakikisha kwamba suala hili la maji linapewa kipaumbele na si suala la kuzembea wala si suala la kufanyia mas-hara.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niwaombe sana Mamlaka ya Maji kwamba na wao Mamlaka ya Maji baadhi ya saa nyengine wanashindwa kutelekeza majukumu yao kutokana na fedha. Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji wanadai pesa nyingi sana ndani ya Taasisi za Serikali na

Taasisi Binafsi. Kwa hivyo, nawaomba zile taasisi ambazo kwamba zinadaiwa na Mamlaka ya Maji walipe kwa sababu kuna mambo mengine madogo madogo hayahitaji fedha nyingi. Lakini watakapokuwa na ile fedha huenda wakayafanya yale.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana taasisi hizo basi waweze kuwalipa Mamlaka ya Maji ili waweze kufanya kazi zao. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Makame kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Nassor Salum Ali. Atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na baadae nitampa nafasi Naibu Waziri na mwishi atakuja Mhe. Waziri kwa majumuisho.

Mhe. Nassor Salum Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuongea machache kuhusiana na ripoti hii ya Mamlaka ya Maji *ZAWA*.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe fursa hii kukupongeza wewe kwa kuendesha kikao hichi kwa uelewa kwa ujuzi kwa ufahamu mkubwa ulionao na Mwenyezi Mungu *inshaallah* akujaalie akupe kila la kheri huko mbele tunakokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii pia kumpongeza Mhe. Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yake kuisimamia wizara hii na Mamlaka hii husika ya maji.

Lakini pongezi za pekee nimpe Mhe. Rais Dr. Ali Mohammed Shein kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuleta maendeleo kwa nchi yetu na wananchi wake wa Zanzibar. Mhe. Dr. Ali Mohd Shein kiongozi mmoja pekee wa mfano na naweza kusema kwamba ni kiongozi anefanana na "lulu" . Lulu haipatikani ovyo ovyo na nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kutengeza viongozi wanofanana na lulu kwa sababu viongozi aina ya lulu kama Mhe. Dr Ali Mohammedd Shein hawapatikani katika vyama vyengine ila Chama cha Mapinduzi CCM.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze msaidizi wake Balozi Seif Ali Idd kwa kazi kubwa anayoifanya katika kusimamia serikali yetu na Baraza lako hili katika kutekeleza majukumu yake. Mhe. Mwenyekiti, mengi yamesemwa Wajumbe wamechangia katika kuizungumza Mamlaka hii ya Maji. Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji naifahamu vizuri sana kwa sababu mimi Mjumbe wa Kamati na bahati nzuri ni Mjumbe wa Bodi kwa Mamlaka ya Maji. Kwa hivyo, naelewa vizuri sana changamoto zinazowakabili Mamlaka ya Maji.

Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu ni sikuvu na bahati nzuri Mhe. Dr Ali Mohd Shein ni Rais ambaye anawajali wananchi wake na anatekeleza vyema Ilani cha Chama cha Mapinduzi nina imani ya wale ambayo yanapendekezwa na kamati yetu chini ya kiongozi wetu mwenyekiti wetu Kamanda Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Mwenyekiti, unajua katika mpira timu isajili wachezaji 30 lakini katika 30 kunakuwa na nafasi 11 na katika 11 kuna na kapteni, sasa kapteni hawezi kupewa tu kama hana sifa 3. Sifa ya

1 awe mpira anaujua lakini sifa ya 2 awe na nidhamu na sifa ya 3 awe ni muongeaji mzuri. Sasa hii Mwenyekiti wetu zote sifa hizi anazo Mhe. Hamza Hassan Juma hongera sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii kamati yetu kupitia Mwenyekiti wetu Mhe. Hamza Hassan Juma ameichangia vizuri sana na yale ambayo yamo katika ripoti hii nina imani kwa Rais wetu tulienae kwa mapenzi yake kwa ghuba zake kwa imani zake nina imani Mhe. Dr Ali Mohammed Shein ataidhinisha bilioni nne ili kuwapa *ZAWA* kukamilisha miradi ya maji ya Ras al-Khaimah.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Dr Ali Mohd Shein kiongozi wa aina yake na msaidizi wake mzee wetu Balozi Seif Ali Idd nina imani kubwa sana atakapokuja kulifunga Baraza hili basi atakuja na maneno matamu na wananchi watayasikia na nina imani kubwa sana atamshauri vyema Rais wetu Dr. Ali Mohd Shein ili kuweza kutoa fedha hizi kumalizia visima vyetu vya miradi hii ya Ras al- Khaimah. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine ambazo zimeelezwa humu Mamlaka ya *ZAWA* uvamizi wa vianzio vya maji. Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na mvamizi mkubwa sana wa vianzio vya maji.

Niombe serekali waziri atakapokuja atoe kauli kubwa au kali kwa wale ambao wanavamia vianzio hivi vya maji. Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa na lazima serikali itoe kauli nzito kwa wale ambao wanavamia vianzio vya maji. Lakini mbali na vianzio vya maji wanaovamia lakini kuna wale ambao wanafanya *sabotage*.

Mhe. Mwenyekiti, hawa ni watu ambao hawaipendi nchi yetu hawana mapenzi na binaadamu mwenzao na waislamu wenzao, kwa sababu wanayafanya mambo haya binaadamu wenzao wanakosa maji Mhe. Jaku Hashim Ayoub kasema maji yanamgusa kila kiumbe. Kwa hivyo, hawa tuwalaani na nina imani serikali itatoa kauli kubwa ili kuwadhibiti na kuwahukumu wale ambao wanaharibu vianzio vya maji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu umenipa dakika 5 na mimi ni Mjumbe wa kamati hii naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Lakini vile vile naiunga mkono ripoti ya kamati kwa asilimia mia moja vile vile. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Nassor Salim Ali kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na yeye nitampa dakika tano, lakini pia nimeombwa dakika tano na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na yeye atoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja, baadae nitampa Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, na Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, atamalizia.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nitasema kwa haraka haraka ili niheshimu muda wako. Mhe. Mwenyekiti, nimewasikia wajumbe wakieleza kwa masikitiko makubwa kuhusu suala la maji kwa ufupi tatizo la maji nchini.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inalielewa kwa kina tatizo la maji na inajua changamoto zake na imejipanga vizuri katika kulitafutia ufumbuzi. Mhe. Mwenyekiti, changamoto kubwa ni

upungufu wa maji ardhini na kuongezeka kwetu kwa idadi ya watu, mahitaji yetu yamekuwa makubwa zaidi ya maji ukilinganisha na miaka ya nyuma na ardhi yetu ndogo na tatizo la msingi ni uharibifu wa mazingira tunayoyafanya. Tunaharibu vianzio vyetu ya maji, tunakata miti na mambo mengine ambayo yana athari kubwa katika upungufu wa maji. Hilo ndio tatizo la msingi ambalo linatukabili.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni miundombinu chakavu ya muda mrefu ya usambazaji wa maji. Tatizo hilo tayari serikali imeliona na iko mipango na mtamsikia Mhe. Waziri husika akieleza kwa kina mipango hiyo ya namna tunavyoshughulikia uchakavu wa miundombinu ya maji, ili kuwa na miundombinu bora itakayoweza kusaidia kutatua tatizo la maji nchini, ili maji yapatikane vizuri zaidi.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, mahitaji makubwa ya kifedha kwa ajili ya miradi hiyo ya usambazaji wa maji. Sote tunaelewa uwezo wetu wa kiuchumi. Kwa hivyo, sio rahisi kwamba tatizo kubwa lenye mahitaji makubwa kama hili la kifedha tukaweza kulimaliza kwa mara moja. Lakini kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe wengine hapa, jitihada kubwa hususan anazochukua Mhe. Rais wetu, zinasaidia sana katika kupambana na hali hiyo na mimi naamini sana jitihada hizo zitatoa matunda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeanza kazi nzuri, imeanza kuchimba visima mbali mbali Unguja na Pemba, imeanza kujenga matenki ya maji katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba, imesambaza umeme katika vituo hivyo ambavyo vinahitaji umeme kwa nia ya kusambaza maji, na bado sasa inachukua hatua kubwa ya kusambaza mabomba mapya ili tuweze kubadili yale mabomba chakavu na hapo tutaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa usambazaji wa maji.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa serikali imeelekeza kukopa zaidi ya milioni 200 za Kimarekani kwa ajili ya mpango huu wa usambazaji wa maji, kuhakikisha kuimarisha miundombinu ya maji, ili sekta ya maji nchini iweze kufanya wajibu wake vizuri. Kwa hivyo, haya yote Waheshimiwa Wajumbe mliyoyasema mipango yake ipo mizuri, ambayo mimi naamini italeta tija katika kutatua tatizo. Naamini sana michango iliyotolewa na kamati na wajumbe, lakini Waheshimiwa Wajumbe nataka tukubaliane, kwamba mipango ambayo serikali imejipanga sio muda mrefu tena matokeo mazuri katika jitihada zetu hizo kwenye suala zima la usambazaji wa maji litajitokeza. Kwa hivyo, nawaombeni sana muivumilie serikali yenu wakati inachukua jitihada hizi kubwa. Hivi sasa tuna mpango wa mkopo wa karibu milioni 100 dola kutoka China, mpango wa mkopo wa karibu dola 92 milioni kutoka India, tuna mpango wa *ADB* zaidi ya milioni 11 dola. Yote hayo ni katika jitihada zetu za kuhakikisha kwamba usambazaji wa maji unafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini tuna wajibu sisi kama viongozi tuwaambie wananchi kuhusu suala zima la kuhakikisha tunayalinda mazingira yetu. Tatizo moja kubwa ni uharibifu mkubwa wa mazingira ambayo yanajitokeza, hasa kwa kuharibu vyanzo vya maji, kujenga katika vyanzo vya maji, kujenga katika njia za asili za maji na ujenzi mzima wa kiholela. Jambo hili linaharibu sana uwezo wetu wa kupatikana kwa maji. Kwa hivyo, ni vizuri sana sisi kama viongozi tuwahimize wananchi tuwache tabia hizi za uharibifu ambazo zina athari kubwa katika upatikanaji wa maji.

Vile vile miundombinu ambayo tayari tunayo kwa makusudi kabisa kuna baadhi ya watu wanaiharibu, wanaivunja. Kwa hivyo, jambo hili linarudisha nyuma jitihada za serikali katika kuendeleza kusambaza maji nchini. Lazima sote kwa pamoja tukubaliane kwamba tuviheshimu vyanzo vyetu vya maji, tuheshimu miundombinu yetu ambayo ndio uti wa mgongo wa kupatikana kwa maji. Kwa ufupi inatubidi sote tuziheshimu sheria zetu tulizoziweka kwa nia ya kutuwezesha ili tuweze kupata maji ya kutosha nchini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la *ZAWA* kuwanzisha *ZAWASCO*. Mimi naona bado umuhimu wa *ZAWA* inaweza kabisa kutekeleza majukumu yake, baada ya hii mipango mizuri ya serikali. Jambo kubwa hapa ni kuwezeshwa *ZAWA* kiuwezo wa kifedha na kiutendaji, na kazi hiyo serikali inafanya. Kama nilivyokwisha kusema kwamba mipango mbali mbali ya mikopo imeandaliwa na jitihada nyengine zinafanywa kwa upande wake serikali kutenga bajeti yake vizuri katika kuhakikisha kutatua tatizo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, bado niwaombeni sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba *ZAWA* ina uwezo mkubwa wa kufanya mambo vizuri, tuipe nafasi serikali yetu na wizara husika ili itekeleze wajibu wake iweze kutekeleza majukumu yake kwa nia ya kuimarisha usambazaji wa maji nchini. Naamini muda sio mrefu tatizo hili litamalizika. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono sana maelezo ya waziri na naamini na wajumbe wenzangu wataunga mkono ili tuipitishe hoja hii bila ya matatizo yoyote. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kusema kwa machache sana kuunga mkono hoja au taarifa aliyoitoa Mhe. Waziri anayehusika na Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze wizara kwanza kwa kuja na taarifa hii. Lakini vile vile niwapongeze sana na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia. Kwa kweli wamechangia kwa uwazi, tatizo sote tumeliona na kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tatizo lipo, lakini serikali haijakaa inalishughulikia tatizo hili, na juhudi kubwa zimechukuliwa. Kwanza za kuwatafuta wafadhili katika kusaidia mradi utakaosaidia kuondosha tatizo la maji katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametaja baadhi ya mashirika ambayo yatatusaidia yakiwemo *JICA* karibu milioni 100, lakini vile vile *ADB* karibu dola milioni 11.9, *Exim Bank* ya India karibu dola milioni 62.18. Lakini pamoja na hayo tuna kazi ya kuifanya kwa kipindi kifupi, kwa taarifa nilizozipata na Waheshimiwa Wajumbe michango yao inaonesha kwamba kuna haja ya kulitatua tatizo hili kwa haraka zaidi, kuliko hata kusubiri utekelezaji wa mipango ambayo inaweza kuchukua muda kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika hilo kupitia visima vilivyochimbwa na mradi wa Ras al Khaimah, ambapo tuna visima kama taarifa zangu sahihi karibu visima 150 vilichimbwa. Katika visima hivyo mwaka jana wa fedha 2016/2017, karibu visima 24 vilikamilika kuwekewa miundombinu yake, na mwaka huu wa fedha tulitenga na bajeti hiyo tulipitisha hapa, tulitenga karibu bilioni 1.5 kwa ajili ya visima 26. Kwa maana hiyo visima vya mwaka jana 24 na hivi ambavyo bajeti

yake ipo ya 1.5 basi tunafanya visima ambavyo vingeweza kukamilika kuwa visima 50. Lakini bado tutakuwa na visima 100 ambavyo bado havija kamilika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi niombe Waheshimiwa Wajumbe, watuachie tukae na wizara inayohusika na kupitia *ZAWA*, kwanza watayarishe mahitaji yao hasa kwa vile visima ambavyo wataona ni *critical* katika kipindi hichi, mahitaji yake yajulikane. Najua kabisa kwamba tunahitaji karibu bilioni 8.8 kwa visima vyote 126. Tukitoa hii bilioni 1.5 ambazo zimo katika bajeti, tunahitaji kuwa na bajeti ya bilioni 7.3. Sasa tutaamua na wao vile visima ambavyo tunahisi ni muhimu na vina mahitaji ya haraka, ili kuweza kujua sasa fedha hizo tutazipata katika maeneo gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaweza tukafanya *reallocation* kwa kupitia bajeti yao. Lakini hayo tunaweza tukayafanya baada ya kujua mahitaji yanayohitajika na ni visima gani ambavyo ni muhimu kuvishughulikia katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018. *(Makofi)*

Kwa hivyo, bila shaka yoyote hayo yatahitaji baada ya sisi kukaa wizara mbili kwa kupitia *ZAWA*, tutahitaji pia muongozo wa serikali katika kukabiliana na tatizo hilo. Upatikanaji wa fedha utaweza tu kupatikana pale itakaporidhiwa, lakini kwa kupitia bajeti ambayo tunayo hivi sasa ambayo tayari imeshapitishwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Sasa ama kufanya *reallocation* ama kufanya *virement* ya kutoa fungu moja kwenda fungu jengine. Hayo ni maamuzi. Nasema tena hayo sasa yatakuwa ni maamuzi ya serikali baada ya kujua mahitaji halisi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwa sasa hivi ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wakakubaliana na rai hiyo, ya kwamba kuna haja ya kulifanyia kazi suala hili la kujua yale mahitaji halisi na baada ya kuyajua hayo tutajua namna ya kuzipata fedha kwa ajili ya kufanya kile ambacho kitakubalika kufanyika katika mwaka wa fedha wa 2017/2018. Ningeomba niseme hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, kumbe ningekunyima hii nafasi, basi ingekuwa sijawatendea haki wajumbe. Nakushukuru sana. Sasa naomba nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi kusema lolote juu ya ripoti hii ya Mamlaka ya Maji katika utekelezaji wa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, sote tumekubaliana ama mawazo yetu yanafanana ya kwamba wananchi wanataka maji na hawataki maneno maneno, lakini wanataka maji. Lakini pia imani yetu ni kwamba tunakubaliana ili maji yapatikane ni lazima hizi changamoto ambazo zimeainishwa zipate jawabu na jawabu yake kama ambavyo imeoneshwa katika ukurasa wa 11 wa ripoti hii na maneno ambayo yameongezwa na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais juu ya upatikanaji wa hii huduma ya maji.

Lakini mimi naomba nikazie kidogo changamoto tatu ambazo zimeainishwa hapa, hasa hii ya uhaba wa maji. Imesemwa kwamba maji kwa sasa yamepungua kutoka ardhini, lakini kwenye

visima inawezekana usiamini kwamba yamepungua kweli na utaona kwamba wataalamu labda wanatumia utaalamu wao katika kupotosha ukweli. Lakini fursa ipo kwa Waheshimiwa Wajumbe, naomba sana hili watenge muda wao wa kwenda kuangalia chemchem zetu mbili ambazo tunazo. Chemchem ya Mtoni na Mwanyanya wakapate maelezo ya kutosha hapo mwanzoni zilipokuwa zinafanya kazi na zinatoa maji na hali halisi ya sasa, bila shaka wataamini kwamba maji kweli yanapungua. Lakini wakati wanakwenda huko niombe watowe taarifa kwa *ZAWA* kusudi *ZAWA* iandae utaratibu wa kutoa taarifa, kule kwa sababu kuna walinzi ili wakapate hayo maelezo wajionee hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto hizi nyengine zinabebwa moja kwa moja na *ZAWA* ama serikali, lakini nyengine ina nafasi kama Waheshimiwa Wawakilishi ama wananchi kwa jumla kuchangia katika kuzipunguza hizi changamoto kusudi maji yapatikane.

Kwa mfano, hili suala la upotevu wa maji, suala hili linachangiwa na miundombinu kama ilivyokuwa imezungumzwa, lakini pia wakati mwengine baadhi ya wananchi ambao sio wazalendo kwa nafasi yao katika kulichangia hili. Nimeshuhudia baadhi ya maeneo mabomba ama mipira imetobolewa kusudi wanyama wapate maji ama mtu anamwagilia shamba lake kwa maji. Sasa sio tabia nzuri kwa kweli kwa sababu inapelekea maji yakosekane katika maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya tatu ambayo imeainishwa hapa ambayo nataka kuielezea ni mabadiliko ya tabia nchi. Hili kwa kweli inatuathiri na mfano mzuri ni jimboni kwa Mhe. Jaku Hashim kulikuwa kuna kisima kikawa kinahudumia kwa wananchi, lakini baadae kikatumbuka chumvi. Ni mfano hai kwamba kweli moja kati ya jambo ambalo linatuathiri ni mabadiliko ya tabia nchi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba serikali inajitahidi kuhakikisha inafanya jitihada mbali mbali ya kuhakikisha wananchi wake wanapata maji.

Kwa mfano, baada ya kutumbuka chumvi katika kisima kile cha Michamvi, ukafanywa mradi wa kuhakikisha wananchi wanapata maji, lakini pia kama ambavyo imeoneshwa jitihada ambazo zinafanyika za kuchimba visima vyengine kusudi maji yafike kwa wananchi. Lakini pia niseme kuhusiana na hili jambo la Michamvi kidogo kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Mwenyekiti, juzi ni kweli nilisema na nikamuomba kwamba tukutane, lakini kwa bahati mbaya hatukukutana. Nilisema tukutane sio tu kwa sababu ya kwamba atakuja kusema hayajafikishwa, bali niliona ipo haja ya kukutana mimi na yeye kwa sababu tukisema kila kitu hapa, basi wajumbe wengine wanaweza wakaona wivu labda kwa nini Mhe. Jaku Hashim anapendelewa na hatukutaka ifanyike hivyo, kwa sababu tunapotaja maji na majimbo mengine pia na wao wanahitaji, tulitaka tukutane lakini kwa bahati mbaya hatujakutana. Ila nilimwambia leo tulipoonana anipatie namba na akanipatia namba ya Mhe. Sheha, nimewasiliana na Sheha juu ya ule mpango ambao tumefanya makubaliano, tulivyokuwa tumekubaliana na uwezo wetu *ZAWA*. Ni imani yangu kwamba tukitoka hapa ukiuliza itakuwa maji yamefika. Lakini Sheha nilimuomba anijulishe kama maji yakifika au hayatofika. Sasa nitapata uhakika zaidi kwa kupitia kwa Bwana Sheha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niseme kwamba maji yetu Zanzibar katika uwasili wake ni masafi, ingawa kunasemwa kwamba ndicho chanzo cha maradhi, lakini kwa historia tunasikia kwamba

hata meli zilikuwa zinachukua maji Zanzibar uthibitisho kwamba maji safi na salama katika uwasili wake. Lakini nini kinasababisha maji yalete madhara ni ile *contamination* ambayo inatokezea kwenye maji, hata leo ukichukua maji ya chupa ambayo tunaamini ni safi *Contamination* na vitu vyengine basi yataleta madhara.

Lakini mwisho nimalizie kutokana na muda kwamba sote tunatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini ahadi ambayo imetolewa ni ya miaka mitano tukumbushane tuvumiliane lakini pia katika maeneo mengine tuwe tunaambizana. Baada ya hayo Mwenyekiti nikushukuru kusudi apatiwe Mhe. Waziri nafasi ya kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nisharti na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Mhe. Wajumbe wa Baraza lako tukufu ambazo nyingi zao tayari zimeshatolewa ufafanuzi, lakini naomba niwashukuru sana kwa wale wote waliochangia kwa njia moja au nyengine najua kwamba kila mtu amesoma hii *document* na kwa sababu maji kila mtu yanamgusa, maji ndio uhai, maji ndio maisha kwa hivyo kulikuwa kuna sababu zote na kuna kila haja ya wachangiaji lazima wawe wengi.

Lakini vile vile naomba nichukue nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, kuwapongeza sana Mawaziri ambao waliochangia na hata wale wasiochangia kwa ufafanuzi ambao wameutoa na ufafanuzi ambao umeweza kumaliza na kukata kiu ya mambo yote ambayo yalikuwa yamejitokeza. Naomba nikiri kusema kwamba Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Afisi ya Makamu wa Pili ametoa ufafanuzi wa kutosha na kufanya *reference* ya kile ambacho kipo hasa tukiangalia *issue* ya upungufu wa maji ndani ya ardhi, lakini na jitihada kubwa ambayo Serikali kupitia mamlaka ya maji *ZAWA* inaichukua katika kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata maji safi na salama.

Lakini vile vile nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango sana kwa ufafanuzi wake mzuri uliojikita katika maeneo yote ambayo Wajumbe walikuwa wameyatoa na wameweza kutoa ufafanuzi mzuri, na bahati nzuri tunafanya kazi kama timu siku zote tunakaa tunashauriana na panapohitajika jambo sisi tunafanya kazi kwa pamoja tunasaidiana na tunashirikiana na kwa hili kama alivyolieleza mimi naamini tutakaa, katika yale maeneo tutakubaliana na tutafanya kazi kwa pamoja.

Lakini sasa Mhe. Mwenyekiti, niombe kuwataja moja kwa moja wale wote waliochangia moja kwa moja na waliochangia kwa maandishi. Waliochangia moja kwa moja.

Kwanza Kamati ya Ardhi na Mawasiliano, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa wangu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuishauri Wizara hii lakini kwa hisia kubwa ambayo wanaona kwamba Wizara hii ina jukumu la kuhudumia wananchi kwa hivyo saa zote wao wako mbioni kuhakikisha mambo yanakaa sawa, kwa kweli wanafanya kazi kubwa na wanastahiki pongezi.

Lakini vile vile nimtaje

1. Mhe. Machano Othman Said ambaye nae alichangia moja kwa moja
2. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy

3. Mhe. Suleiman Sarahan
4. Mhe. Shehe Hamad Mattar
5. Mhe. Bahati Khamis Kombo
6. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
7. Mhe. Ali Suleiman Ali
8. Mhe. Mohammed Said Mohammed
9. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
10. Mhe. Suleiman Makame Ali
11. Mhe. Nassor Ali Salim
12. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed
13. Mhe. Khalid Mohammed Salum ambao hawa wote walichangia moja kwa moja.

Lakini vile vile naomba niwataje Mhe. Mwenyekiti wale waliochangia kwa maandishi.

1. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
2. Mhe. Said Soud Said
3. Mhe. Simai Mohammed Said na
4. Mhe. Yussuf Hassan Iddi hao wote wamechangia kwa maandishi.

Naomba niwashukuru sana kwa kuchangia kwao kumeibua hisia lakini vile vile tumeweza kupata kile ambacho sisi kama Wizara kupitia Mamlaka tunahitaji kukisimamia na kuhakikisha kukitekeleza ipasavyo ili wananchi waweze kufanikiwa, na kupata maji safi na salama na kutimiza lengo na dhamira ya Serikali. Lakini vile vile kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Lakini naomba niseme kwamba mapendekezo ya kamati tumeyapokea tutayafanyia kazi kwa mujibu wa Sheria na taratibu zote za nchi zilizopo, ushauri tumeupokea tutakaa pamoja na taasisi husika kama nilivyosema mwanzo na uwepo ahadi za utekelezaji basi tutazipanga kwa pamoja. Lakini naomba niseme kwa ujumla wake moja kwa moja hizi kwa ujumla wake kwa sababu masuala yamekuwa mengi ambayo mengi yamekuja moja kwa moja *specific* kwenye *issue* za majimbo, *pump*, mabomba hayajaungwa, upotevu wa maji na mabomba.

Naomba niseme kwamba kazi hizi zote ni kazi za kawaida katika kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo yote ambayo mmeyataja. Kwa hiviyo kazi hizi zinaendelea na zitaendelea kuwa endelevu na kila wakati fedha tutakapopata basi kazi hizi zitaendelea kufanyika, na *inshaallah* kila siku tumuombe Mwenyezi Mungu kwamba iko siku hizi kazi zitaisha. Lakini kazi za *rehabilitation* bado zitaendelea kuwepo.

Lakini naomba pia niseme kwamba suali moja ambalo naomba nilitolee ufafanuzi mara nyingi limekuwa likijitokeza hili la visima, utakuta sehemu ya Magharibi mara nyingi kule ndio kwenye maeneo mengi ambayo yenye maji mengi chini kuliko sehemu za mjini ambazo maeneo mengi yana maji ya chumvi, lakini hata maji yake hayako salama. Kwa hivyo katika lengo lile lile la kufanikisha maeneo yanayochimbwa visima ni yale yanayofanyiwa utafiti na pakaonekana panafaa. Kwa hivyo usione wakati mwengine kwamba jimboni kwako pamechimbwa visima lakini visima vile vinafaidisha watu wa jimbo jengine lakini lengo letu ni kuhakikisha kamba

sote tunafaidi, vyengine vinafanya kazi katika maeneo yale lakini vyengine vinafanya kazi katika maeneo mengine.

Mimi naamini kwamba sisi sote lengo letu ni moja la kuhakikisha wananchi wote bila ya kujali huyu wa jimbo gani na huju jimbo gani wananchi wote wapate maji safi na salama kwa hivyo hilo naomba nilitolee ufafanuzi.

Lakini hizi za kazi zote nimeshazisema siwezi kusema mtu mmoja mmoja ambayo mengi yalizungumzwa, lakini pia nizungumze suali la fidia hili ni suali endelevu kwa sababu maeneo mengi yalifanyiwa kazi ambayo hayakulipwa fidia, lakini kila tunapopata fedha fidia inaendelea kulipwa. Naomba tu niwaombe sana wananchi kama waliviyoweza kuvumilia kipindi chote wale ambao bado hawajapata fidia zao basi waendelee kuwa wavumilivu, lakini lengo la Serikali ni kuwahudumia wao kuwapa fidia zao lakini pia na kupatikana maji ndani ya Zanzibar. Kwa hivyo haya yote ni muhimu lakini nawashukuru sna wananchi kwa uvumilivu mkubwa kuona kamba umuhimu wa kupitisha bomba una thamani yake. Kwa hivyo wameweza kuwa wavumilivu na kuweza kusubiri hizi fidia kwa muda mrefu lakini kila haja inapotokea na fedha zinavyopatikana tuataendelea kuwalipa.

Vile vile kulitolewa ushauri hapa wa kuweka matangi katika maskuli yale ambayo vimetengenezwa ushauri umepokelewa na kila tutakapopata nafasi basi kazi hii itafanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba huduma hii inapatikana.

Lakini jengine naomba nizungumze kwamba lilizungumzwa suali la *Pilot project* pale Makadara ni eneo la *pilot project* ambapo wenzetu wa *JIGA* walifanya kuangalia ile miundombinu ya maji katika kubadilisha mabomba lakini pia na kuangalia *issue* za mita katika makusanyo, katika hili naomba niseme katika eneo lile *ZAWA* inatoa bill za jumla shs. 6,575.408/= hizo ndio zile ambazo zinatoka kwa eneo lile la *pilot project* na inakusanya milioni 4,456,000/= sawa na asilimia 67.7 ya mapato ambayo katika lile eneo la *pilot project.* Kwa hivyo unaona kabisa kama ile kazi ni *effective* kwa ababu inaleta tija na watu wamepata hamasa na wanachangia, kwa hivyo zoezi lile tutaendelea kila eneo kwa eneo kila tutakapoweza kupata fedha.

Lakini pia zoezi la uhamasishaji kwa wananchi *ZAWA* imefanikiwa kwa kiwango kikubwa tunajitahidi sana kutoa elimu kwenye Redio, Televisheni lakini mpaka Masheha na Mikutano ya kawaida katika maeneo, lakini hata kupitia katika watu mmoja mmoja. Kwa hivyo na jambo hili pia limeweza kusaidia katika kuongezeka kwa mapato pamoja na kwamba hatujafikia lile lengo lakini kweli mapato yanaengezeka na *inshaallah* Mwenyezi Mungu kwa mwaka huu basi yataendelea kumalizika.

Lakini lilikuja suali la kuulizwa *operation coast* na nilijua kwa nini limeulizwa hili lakini *operation cost* kwa mwezi *ZAWA* wanatumia karibu milioni 700 kuendesha shughuli zao zote, lakini *Revenue commerce* ni milioni 2 mpaka milioni 3 ambayo inakusanywa. Tatizo ni lile lile kwamba bado watu ile ari ya uchangiaji pamoja na kwamba wanapata maji kwa mgao lakini bado ile ari ya uchangiaji haijawa nzuri. Naomba nitoe wito kwa wananchi mbele ya Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kwamba wananchi waendelee kuchangia maji hata kama wanapata kwa mgao lakini bado wanatumia ili tuweze kujiimarisha ipasavyo ndani ya mamlaka.

Deni la umeme ambalo *ZAWA* linadaiwa kutoka April, mpaka Septemba 2017 ni bilioni 2.9 deni hilo linadaiwa ambalo bado tutaweza kulilipa deni la umeme kupitia Serikali, serikali inajitahidi sana katika hili naomba niseme kwamba Serikali inalipa bili zote za *ZAWA* sasa hivi na kwenda kwa *ZECO* na hili deni limekusanyika kwa sababu bado tuna jukumu la Serikali la kulipa deni la *TANESCO* lile la 1 Bilioni na *ZECO* wenyewe wakatoa 2 bilioni, kwa hivyo bado hizi pesa zinadaiwa 2.9 lakini bado serikali inaendelea kulipa kama ilivyoahidi.

Jengine ambalo lilizungumzwa suala la mradi wa India, suala la mradi wa India bado linaendelea vizuri tuko katika *last process* ya kumtafuta mshauri Mwelekezi na sasa hivi katika hatua ya mwisho kwa sababu imeshafikia tushatoka katika wale 27 tushakuja kwenye tisa, tushakuja kwenye saba na sasa hivi alikuwa anatafutwa mmoja ambae sina uhakika sana mpaka leo. Kwa sababu watu wa Exim walikuwepo hapa Zanzibar kama nilivyosema katika suali langu siku tano sita zilizopita huko nyuma kwamba walikuwa wanataka kukamilisha hii kazi kwa hivyo kazi inaendelea vizuri.

Kwa hivyo niombe tu kuwatoa hofu wananchi lakini na wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kwamba hii kazi ya uungaji wa visima ni kazi endelevu na kazi tutakayoifanya kwa udhati na umakini sana na sisi tunajua hisia na joto kubwa tunalolipata hasa ukizingatia hata mimi mwanamke napata *feeling* ya kuwa na maji ndani ya nyumba, kwa hivyo tunajua uzito wake na tunajua thamani yake. Kwa hivyo mimi ninachoamini katika hili tukishirikiana kwa pamoja tunaweza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kuwashukusru sana Mhe. Mwenyekiti, sitaki kusema yale ambayo yameshatolewa ufafanuzi sitaki kuyaongea tena lakini naomba niwashukuru sana, tushirikiane tukumbuke kwamba kila toni moja la maji ni gharama kwa hivyo bado tutaendelea kutumia gharama.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Maji, Nisharti na Mazingira, waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na ripoti hii wanyanyue mikono juu, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.*(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Ahsante sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wako na mimi napenda nichukue nafasi hii au fursa hii kwa kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na watendaji wake wote kwa juhudi wanazozifanya, lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wa ripoti zao, pia niwapongeze wajumbe wote waliochangia ripoti hii kwa haja tu ya Serikali kutekeleza majukumu yake na si kwa vyenginevyo na nina imani Waziri wetu msikivu na anajua shida za maji na hasa zinawakabili

wanawake na Waziri yeye ni mwanamke na nina imani atachukua juhudi hii ili kufanyia kazi changamoto zilizotolewa.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuahirisha kikao tuna tangazo hapa baada ya kuakhirisha kikao Waheshimiwa Wajumbe wote wabakie kuna taarifa muhimu inataka kutolewa, nawashukuru sana kwa usikivu wenu lakini pia kwa utulivu wenu ahsanteni. Naakhirisha kikao mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1.26 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka Tarehe 12/10/2017 Saa 3.00 asubuhi)